# MAFUNDISHO NA MAZOEZI YA KANISA

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Shepherds Global Classroom ipo kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo kwa kutoa mtaala kwa ajili ya kuwaendeleza viongozi wa Kikristo duniani kote. Tunalenga kuongeza programu za mafunzo ya asili kwa kuweka chombo cha mtaala wa kozi 20 mikononi mwa viongozi wa kiroho wanaotoa mafunzo katika kila nchi duniani.

Kitabu hiki kinapatikana bure kwa njia ya kupakua kutoka katika https://www.shepherdsglobal.org/courses

Mwandishi Mkuu: Dr. Stephen K. Gibson

Hakimiliki © 2019 Shepherds Global Classroom

Ilitafsiriwa kutoka Toleo la Pili la Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa.

Nyenzo za wahusika wengine zilizotumika ni hakimiliki ya wamiliki husika ambazo zimeshirikishwa na kutumika humu chini ya leseni mbalimbali.

Tafsiri ya Maandiko "yaliyonukuliwa" kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, "Swahili Union Version Bible" (SUVB®)." Yametumika kwa kibali. Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa kuhusu vibali:**

Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa na kutawanywa bure kikiwa kimechapishwa na katika mifumo ya kidigitali chini ya miongozo ifuatayo: (1) Maudhui yaliyoko kwenye kitabu hiki hayawezi kubadilishwa kwa namna yeyote ile; (2) Nakala zinazopatikana haziwezi zikauzwa kwa ajili ya kupata faida; (3) Taasisi za elimu zina uhuru wa kutumia na kukinakili kitabu hiki, hata kama wanalipisha ada za masomo ya ziada; na (4) Kitabu hiki hakiwezi kufanyiwa tafsiri pasipokuwepo na kibali na usimamizi wa Shepherds Global Classroom.

# Yaliyomo


Mtazamo wa Kozi ........ 5

(1) Mungu Mmoja na Kanisa Moja ........ 7

(2) Umoja wa Kikristo ........ 15

(3) Kanisa la Mahali ........ 23

(4) Mashirika ya Kanisa ........ 29

(5) Uanachama wa Kanisa ........ 37

(6) Kushirikishana Maisha Pamoja ........ 49

(7) Kanisa katika Dunia ........ 57

(8) Msaada wa Kanisa la Mahali ........ 65

(9) Zaka ........ 73

(10) Ubatizo ........ 79

(11) Meza ya Bwana ........ 89

(12) Nidhamu ya Kanisa ........ 99

(13) Tabia ya Kiongozi wa Kikristo ........ 109

(14) Karama za Kiroho ........ 117

(15) Maswali kuhusu ukomavu kwa Kanisa ........ 129

Fomu kwa ajili ya Kumbukumbu ya Kazi za Kufanya ........ 137

# Mtazamo wa Kozi

## Maelezo ya Kozi

Kozi hii inawasilisha dhana ya kibiblia kwa ajili ya kanisa kama kiini cha kazi ya Mungu. Mwanafunzi atapata ufahamu wa Umoja wa Kikristo, uanachama wa kanisa, ushirika, msaada wa kifedha kwa ajili ya huduma, utoaji wa zaka, ubatizo, Meza ya Bwana, nidhamu ya kanisa, na alama za ukomavu wa kanisa. Kozi hii inaelezea kanuni na jinsi ya kuzitumia kwa ajili ya maisha na kazi ya kanisa.

## Malengo ya Kozi

1. Kuelewa utambuzi na maelezo ya Biblia kuhusiana na kanisa.
2. Kuuona mpango wa Mungu kwa ajili ya kanisa, na kazi ya Mungu ndani ya kanisa.
3. Kujifunza majukumu ya mwanachama na Kiongozi ndani ya kanisa.
4. Kuzitumia kanuni kwa ajili ya kutoa msaada, utawala, na uendelezaji wa Kanisa la mahali.
5. Kupatiwa nyenzo kwa yaliyomo na muundo wa kufundisha kuhusu kanisa.

## Maelekezo kwa ajili ya Viongozi wa Madarasa

Maelekezo kwa viongozi wa madarasa yamewekwa katika kozi nzima pamoja na maelekezo kwa ajili ya sehemu maalumu za masomo. Zimeoneshwa kwa *maandishi ya mlalo.*

**Maswali yanayohitajika kujadiliwa** na **shughuli za ndani za darasa** zimeoneshwa kwa alama ►. Kwa maswali yanayohitajika kujadiliwa, Kiongozi wa darasa atapaswa kuuliza swali na kuwapa wanafunzi muda wa kujadili hilo swali. Kama mwanafunzi huyo huyo kwa kawaida anakuwa mtu wa mwanzo kujibu maswali kwanza, au kama wanafunzi wengine hawapendi kuwajibika katika kujibu maswali, kiongozi anaweza kulielekeza swali moja kwa moja kwa kumlenga mwanafunzi yeyote: mf “Petro, unawezaje kujibu swali hili?”

**Maandiko** mengi yametumika katika kozi hii. Vifungu ambavyo vinapaswa visomwe kwa sauti katika darasa vimeoneshwa kwa vichwa vya mishale. Wakati mwingine, marejeo ya maandiko yamekuwa kwenye kifungu kwa kutumia alama za mabano. Kwa mfano: (1 Wakorintho 12:15). Alama hizo ni kwa ajili ya kuunga mkono taarifa iliyoko kwenye kifungu husika. Hakuna ulazima wa kusoma aya zilizoko kwenye alama za mabano.

Kila somo lina angalau **nukuu mbili** kutoka kwa baadhi ya wanatheolojia katika historia. Wakati wanafunzi watakapofika kwenye nukuu hizi, Kiongozi wa darasa anaweza kumtaka mwanafunzi asome na kuelezea nukuu hiyo.

Masomo yote isipokuwa moja yanakamilika kwa kutoa **Taarifa Saba kwa Muhtasari.** Kusudi la somo ni kwa mwanafunzi kuweza kuzielewa mambo haya. Wanafunzi watapaswa kujifunza na kukariri mambo yaliyoko kwenye muhtasari. Wanafunzi wanapaswa kusoma na kukariri taarifa hizi. Wanafunzi lazima **waandike aya moja kuhusiana na kila** taarifa katika muhtasari na kisha kuziwasilisha kwa Kiongozi wa darasa Mwanzoni mwa kipindi kinachofuata cha darasa (zitakuwa aya saba). Kwenye kila aya mwanafunzi atapaswa kuielezea taarifa kama ambavyo ingekuwa anamwelezea mtu ambaye hayuko darasani, Pamoja na sababu inayoeleza kwa nini hii ni dhana muhimu. Mwanzoni mwa kipindi kinachofuata, Kiongozi wa darasa anatakiwa aandaye baadhi ya wanafunzi ambao watashirikishana aya zao walizoandaa pamoja na kikundi chote cha darasa.

Pia mwanzoni mwa kipindi kinachofuata, wanafunzi watapaswa **kuandika Taarifa Saba kwa Muhtasari kwa kumbukumbu kutoka kichwani tu** kama mtihani wa kuandika wa majaribio ya ufahamu wao. Kiongozi wa darasa atahakikisha kwamba wanafunzi hawafanyi nukuu kutoka kwenye kumbukumbu zao walizoandika, au mwanafunzi mmoja kumsaidia mwingine wakati wa kufanya mtihani. Kama mwanafunzi atakuwa hana uwezo wa kuandika hiyo orodha, anaweza akatakiwa kujaribu kuiandika tena baadaye.

Mojawapo ya kusudi kubwa la kozi hii ni kuwaanda wanafunzi waweze kuwa waalimu. Kiongozi wa darasa anapaswa kuwapa wanafunzi nafasi ya kuinua viwango vyao vya kufundisha. Kwa mfano, kiongozi wa darasa mara kwa mara atapaswa kumpa mwanafunzi nafasi ya kufundisha sehemu fupi ya somo katika darasa.

**Kazi ya kufanya ya zoezi la kufundisha:** Wakati kozi hii ikiwa inaendelea, mwanafunzi atapaswa afundishe somo, au sehemu ya somo, kwa mtu binafsi au kikundi ambacho siyo sehemu ya darasa. Mwanafunzi anaweza akachagua somo la kufundisha. Zoezi hili linatakiwa lifanyike mara tatu, akiwa na masomo tofauti. Kazi hii ya kufanya haijawekewa utaratibu. Mwanafunzi atapaswa atafute nafasi yake mwenyewe na ahakikishe kwamba kazi za kufanya zinafanyika. Mwanafunzi anapaswa atoe taarifa kwa kiongozi wa darasa kila amalizapo kipindi cha kufundisha.

**Kazi nyingine za kufanya** zitajumuishwa kwenye kozi nzima: mahojiano, kujifunza Maandiko, kuandika au mitihani. Kazi yeyote ya kufanya iliyoandikwa inapaswa iwakilishwe kwa kiongozi wa darasa kwenye kikundi kinachofuata cha darasa. Kiongozi wa darasa siku zote atapaswa aongoze majadiliano ya kazi ya kufanya na awe na baadhi ya wanafunzi ambao watashirikishana yale waliyojifunza au yale ambayo wameandika.

Kama mwanafunzi atahitaji kupata **cheti cha kufuzu mafunzo kutoka Shepherds Global Classroom**, atapaswa ahudhurie vipindi vyote vya darasa na amalize kufanya kazi zote zilizotolewa. Fomu imetolewa mwisho wa kozi hii kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya kazi za kufanya zilizomalizika.

# Somo la 1
# Mungu Mmoja na Kanisa Moja

## Utangulizi

► Kwa nini unaenda Kanisani?

Wakati watu wanapozungumzia kuhusu “kwenda kanisani” wanamaanisha kwenda kwenye nyumba ya ibada kwa ajili ya ibada iliyopangwa.

Watu wengi Wanasema wanatenda kanisani kwa ajili ya kujifunza kuhusu Mungu. Watu wengine wanaojisikia wako mbali na Mungu huenda kanisani wakitegemea kuusikia uwepo wa Mungu. Watu wanaomjua Mungu huenda kanisani wakitegemea kuusikia na kuupata uwepo wake Mungu kwenye sifa. Kanisa ni kuhusiana na Mungu. Watu wanapaswa waweze kuusikia na kupata uwepo wa Mungu kwenye ibada za kumsifu Mungu za kanisa.

Lakini kanisa siyo jengo, na vile vile siyo mahali pa makutaniko ya kusifu. Kanisa ni kusanyiko la waumini ambao wamedhamiria kwa pamoja kuwa kanisa. Kwa hiyo, Tunaposema kuhusu watu kuliona kanisa au kwenda kanisani, tunamaanisha ni kikundi cha watu walioamini. Tunaposema kwamba kanisa ni kuhusiana na Mungu, hatumaanishi tu kwamba jengo na ibada ya kusifu ni kuhusiana na Mungu. Maisha ya kikundi cha watu waliodhamiria waliyo nayo kwa pamoja ndiyo kuhusiana na Mungu.

## Asili ya Neno

Msamiati wa kigiriki *ekklesia* (G1677)[1] ni neno ambalo kwa kawaida hutafsiriwa “kanisa” katika Agano Jipya. Wakati likitolewa tangazo la watu wakusanyike pamoja katika jiji kwa ajili ya kukutana, mkusanyiko huo ulikuwa unaitwa *ekklesia.*

*Ekklesia* ni neno linalotumika kwa ajili ya kanisa katika Agano Jipya. Neno hili limetumika mara 117 kwenye Agano Jipya, lakini siyo matukio yote yanayorejea kanisa. Baadhi yanarejea kwenye aina nyingine za mikusanyiko (Matendo 19:32, 39, na 41).

Injili inatolewa kwa watu wa rangi zote, jamii zote, maeneo yote na kazi zote. Kama ambavyo kila mtu kwenye jiji anaweza kusikia tangazo la kukusanyika, hakuna kikundi cha watu kinachotengwa katika kupokea injili.

Kanisa ni kikundi cha watu ambacho kimekubaliana na wito wa injili. Watu wake wanatoka katika makundi mbalimbali ya watu ili kuunda kikundi maalumu chenye watu tofauti ambao wamejiachilia kabisa kwa ajili ya Kristo na kanisa lake.

[1] Hii ni namba ya Strong’s Concordance kwa neno la kigiriki.

## Mungu Baba katika Kanisa

Nafsi za Utatu Mtakatifu wa Mungu – Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu – zinahusiana na waumini kwa njia za kipekee katika kanisa.

**Mungu atatukuzwa milele kwa ajili ya kazi anazozifanya ndani ya kanisa.**

> Naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina (Waefeso 3:21).

Kwa kuwa kanisa lipo kwa ajili ya utukufu wa Mungu, hakuna jambo lolote linalotakiwa lifanyike ambalo siyo la kumpa Mungu heshima. Kanisa halipaswi kufanya jambo lolote litakalowapa watu ufahamu usiotakiwa kuhusiana na Mungu alivyo, au jambo la kumfanya mtu awe ndiyo dira badala ya Mungu.

**Kanisa ni familia ya Mungu**

> Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na **hasa jamaa** ya waaminio (Wagalatia 6:10).
>
> Basi ninyi salini hivi: "**Baba yetu** uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe" (Mathayo 6:9).

Kwa kuwa kanisa ni familia ya Mungu, haiwezekani kwa ukweli mtu kuwa katika kanisa isipokuwa awe ana mwamini Mungu na yuko kwenye uhusiano na yeye. Mtu haingii katika kanisa tu kwa kuwa anawajua watu waliomo ndani ya kanisa. Mtu anaingia katika kanisa kwa kuingia kwenye uhusiano na Mungu, na kisha, kuingia kwenye uhusiano na watu wa Mungu waliopo.

► Je inamaanisha nini kuwa na Mungu kama Baba?

## Kristo katika Kanisa

**Yesu ndiye aliyelianzisha na kulijenga kanisa.** Yesu anaahidi mafanikio ya mwisho ya kanisa.

> Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda (Mathayo 16:18).

**Yesu anaahidi kuwa na kanisa.**

> ...Mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari (Mathayo 28:20).
>
> Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao (Mathayo 18:20).

"Kifungu binafsi cha 'kanisa langu' kinaonesha kwamba Yesu, kwa mujibu wa Mathayo, kwa makusudi alionesha kutaka kutengeneza jamii endelevu ya maombi, kuhubiri, na nidhamu. Aliwaita na kuwafundisha wanafunzi wake na kuwapa ahadi ya kuja kwa Roho Mtakatifu ili kuwaongoza baada ya yeye kuondoka na kupaa mbinguni."

- Thomas Oden, *Life in the Spirit*

**Kristo ndiye kichwa cha Kanisa.** Kanisa ndiyo mwili wake hapa duniani. Uhusiano binafsi wa Yesu alio nao na kanisa ni wa kina sana kuliko tunavyoweza kuelewa.

> Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote (Waefeso 1:22-23).
>
> Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake (Waefeso 5:30).

Kwa kuwa mshirika wa kanisa ni sehemu ya mwili wa Kristo, haiwezekani kihalisia mtu kuwa sehemu ya kanisa isipokuwa yeye binafsi awe ameiweka imani yake kwa Yesu kama Mwokozi na amekubaliana na mamlaka ya Kristo kama Bwana.

► Je, ni aina gani ya mtu anayeweza kuitwa sehemu au mjumbe wa mwili wa Kristo?

> "Mahali popote Yesu alipo, kuna kanisa katholiko [la ulimwengu wote]."
>
> - Ignatius
> (katika barua yake kwa Smirna)

## Roho Mtakatifu katika Kanisa

Kitabu cha Matendo kinaonesha kwamba kanisa la kwanza lilikuwa linatambua uwepo wa Roho Mtakatifu pamoja na nguvu zake. Roho Mtakatifu alitoa uvuvio na nguvu kwa ajili ya kuhubiri (Matendo 2:11). Aliwaita watu kwenye wito wa huduma maalumu (Matendo 13:2). Aliwaongoza watu kuwa kwenye maeneo sahihi ya huduma zao (Matendo 16:6-10). Alitoa ufumbuzi masuala yaliyohusu fundisho la imani (Matendo 15:28).

**Roho Mtakatifu ni mwongozaji mkuu wa kanisa katika kukamilisha umisheni wake wa dunia nzima.**

Hakuna shirika lolote binafsi la kibinadamu linaloweza kutegemea kukamilisha kazi yote. Mungu amewaita na kuwatuma wamisionari, na anajua vigezo vya kila eneo la kijiografia.

Mtu ataingia katika kanisa kwa kuona miujiza ya kuzaliwa upya inayotokana na Roho Mtakatifu. Kwa kuwa uwepo wa miujiza ya kuzaliwa upya ni uzoefu unaopita ufahamu wa kawaida, uinjilisti unaongozwa katika njia isiyokuwa ya kawaida na kuwezeshwa na Roho Mtakatifu. Matokeo ya uinjilisti hayawezi kuelezeka kwa njia za kawaida.

**Uhai wa kanisa unategemea Roho Mtakatifu.**

Kuabudu kwa kanisa la kwanza kullkuwa kunaongozwa na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu alizungumza kupitia watu wake mbalimbali (Matendo 4:30-31). Utaratibu wa ibada ulikuwa unaweza kubadilishwa wakati wowote na Roho Mtakatifu.

Kanisa ni tofauti na shirika la aina yeyote ile la kibinadamu. Washirika wa kanisa wanakuwa kwenye ushirika wa kila mtu na mwenzake kwa sababu wako kwenye ushirika na Mungu na wana maisha ya kiroho. Mtu ambaye hajaokoka kiuhalisia hayuko kwenye huo ushirika hata kama atalipenda kanisa na rafiki wa watu walioko katika kanisa hilo.

Roho Mtakatifu hugawa karama za kiroho ili kwamba watu wanaohusika nazo waweze kuzitumia katika kuhudumiana mmoja kwa mwingine (1 Wakorintho 12:4-7). Kwenye siku za kwanza za kanisa la kwanza katika Yerusalemu, kuwajibika kwa washirika pamoja na umoja wao kulikuwa ni kwa nguvu sana kiasi kwamba ni vigumu kwa waumini wa wakati huu kuweza kufikiria ilivyokuwa. Watu waliuza mali zao na kuzikabidhi hizo fedha kwa kanisa ili washirika wa kanisa waweze kushirikishana maisha kwa pamoja. Wakati Anania na Safira walipoamua kusema uongo, waliuawa kwa sababu dhambi yao haikuheshimu kazi ya ajabu ya Roho Mtakatifu aliyokuwa anaifanya kwa kanisa (Matendo 4:32-35, Matendo 5:1-4).

**Umoja wa kanisa unakamilishwa kwa uwepo wa uhai wa Roho Mtakatifu.**

Kanisa (ambalo siyo jengo, bali kundi la watu alioamini) linaitwa "hekalu la Mungu" kwa sababu Roho Mtakatifu huishi ndani ya kanisa kwa njia maalumu (2 Wakorintho 6:16). Hukumu iliyo kali hutangazwa kwa mtu yeyote anayeliletea madhara kanisa la kiroho mahali ambapo umoja wa Kikristo unakaa (1 Wakorintho 3:16-17).

► Je, utasemaje kwa mtu anayedai kwamba amewezeshwa nguvu na Roho Mtakatifu lakini analipiga vita kanisa pamoja na kuligawa?

## Mungu hudhihirishwa na Kanisa

Kanisa lina msaada kwa watu katika kumkumbuka Mungu, kumwelekea Mungu, na kuwa na uzoefu wa mabadiliko yanayofanywa na Mungu.

Kanisa limeundwa na kuanzishwa na Mungu. Zaidi ya mahali pengine popote ulimwenguni, kanisa ni mahali ambapo mapenzi ya Mungu hufanyika kwa makusudi na watu wanaompenda Mungu. Kwa hiyo, kanisa linauonesha ulimwengu ni kwa jinsi gani Mungu alivyo.

► Je, ni mambo gani kadhaa ambayo watu wanapaswa kuyaona kuhusiana na Mungu wanapoliangalia kanisa?

Kwa kuliangalia kanisa, watu wanapaswa wamwone Mungu kwamba ni wa upendo na mwenye huruma, anawajali watu wote, anasamehe, anapenda ukweli, anatimiza ahadi zake, na anachukia dhambi wakati anawapenda wenye dhambi.

► Je, ni makosa gani ambayo watu wanatakiwa wayaepuke kwa kukumbuka kwamba kanisa ni kuhusiana na Mungu?

## Kuabudu

Kwa kuwa kanisa lipo kwa ajili ya Mungu, kuabudu kwa kanisa kunapaswa kuwe katika kumlenga Mungu. Wakati kuabudu kunapofanyika kwa kuwalenga viongozi wa kibinadamu au watendaji, inakuwa ni ya kibinadamu, ambayo ni ibada ya sanamu. Kuabudu kubaya kunafanyika kimwili, kwa kuwatukuza baadhi ya watu na kuvutiwa na tamaa za mwili. Kuabudu kuliko kubaya kunaweza hata kufikia kuwa ni ibada za kishetani kwa sababu

wanaokuwa katika kuabudu wanajiachilia wenyewe kuwa katika hisia na roho zisizotoka kwa Mungu.

## Kanisa Moja la Ulimwengu wote

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Waefeso 4:1-6. Je, kuna jambo gani la muhimu ambalo kifungu hiki kinataka kuonesha kuhusu kanisa?

Paulo aliwataka waumini wawe katika umoja. Sababu za kuwa katika umoja ni kwamba kuna kanisa moja tu, kama na ambavyo Mungu ni mmoja na injili ni moja tu. Wakristo wote wa kweli wako katika mwili mmoja. Kuna ukristo mmoja na kanisa moja kwa sababu kuna Mungu mmoja.

Ukweli kwamba kuna kanisa moja la ulimwenguni kote kunawekewa msisitizo katika 1 Wakorintho 12:13, wakati Paulo aliposema kwamba watu wote wa Mataifa wanaoamini wawe mwili mmoja.

Ukiri wa imani ni kanuni ya imani za msingi za Ukristo. Ukiri wa imani ya Ukristo wa kwanza ulioitwa "Imani ya Mitume" ulihusisha taarifa iliyokuwa inasema "Ninaamini katika kanisa moja la katholiko." Neno *katholiko* katika kanuni ya imani halina maana ya kurejea Kanisa Katoliki. Ilimaanisha "mahali pote" au "mzima." Ukiri wa imani ulikuwa unasema kwamba kuna kanisa moja tu linalowakilishwa na Wakristo kila mahali.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Waefeso 2:20.

Kanisa limejengwa juu ya msingi mmoja: huduma na ukweli vilivyofunuliwa na mitume na manabii; na huduma, ujumbe, upatanisho, na maisha endelevu ya Yesu Kristo. Kuna msingi mmoja na kanisa moja.

Kuna dini moja iliyoko katika nchi ya China inayoitwa Mwangaza wa Mashariki, (*Eastern Lightning).* Wanaamini kwamba kazi ya Yesu ilishakwisha, na kwamba Mungu amemtuma masihi mpya wa wakati huu wa sasa. Huyu masihi ni mwanamke wa Kichina ambaye anafundisha mafundisho mapya ya imani.

► Je, utakuwa na jibu gani la kumjibu mtu aliyetoka katika dini ya Mwangaza wa Mashariki?

Umoja wa kanisa la ulimwengu haimaanishi kwamba shirika moja ndilo kanisa lote. Hakuna shirika moja linaloweza kufikia ukaribu wa kukamilisha kusudi la Mungu kwa ajili ya kanisa kila mahali ulimwenguni. Yesu aliwaambia mitume wake wasitegemee kwamba Wakristo wote watakuwa kwenye shirika moja (Marko 9:38-39).

Kanisa Katoliki linadai kuwa ndilo kanisa lote la Mungu. Wamomoni na Mashahidi wa Yehova wanadai jambo linalofanana na hilo.

► Je, utasema nini kwa mtu ambaye anadai kwamba shirika lake ndilo kanisa lote la Mungu hapa ulimwenguni?

## Uwajibikaji wa Kanisa la mahali kwa Kanisa Moja

Kanisa la mtaa halipaswi na au halitakiwi kujiona kwamba liko huru kutengeneza mafundisho ya imani kwa ajili yake lenyewe. Kwenye eneo moja, Paulo alitoa maelekezo, kisha akasema ilifanyika kwa njia hiyo katika makanisa yote ya Mungu (1 Wakorintho 11:16). Aliliambia kanisa kwamba wanapaswa wawakubali baadhi ya wahudumu wa huduma kwa sababu wanawakilisha makanisa mengine (2 Wakorintho 8:23-24). Alikuwa anamaanisha wazi kwamba itakuwa ni makosa kwa kanisa kuamua kushikamana na mafundisho ya imani yanayotofautiana na makanisa mengine yote.

Kanisa la Wakorintho lilikuwa limebarikiwa kuwa na karama za kiroho. Walianza kujifikiria wenyewe kama walio huru, wasiokuwa na hitaji la kumsikiliza mtu mwingine yeyote. Paulo alifanya masahihisho ya fikra zao na utendaji wao na akawakumbusha kwamba wao hawakuwa chanzo cha asili cha Neno la Mungu; lilikuja kwao kutoka kwa watu wengine na halikuwa limekuja kwao kwa ajili yao pekee (1 Wakorintho 14:36). Aliendelea kusema kwamba wale waliokuwa katika kanisa lao ambao walikuwa na ufahamu wa kiroho wangetambua maelekezo ya Paulo kwamba yamevuviwa na Mungu.

Kanisa la mahali linapaswa lijiongoze na liwe na uwezo wa kujiendesha lenyewe; lakini linahitaji liwe na uhusiano na kanisa la ulimwengu kwa ajili ya kuimarisha mafundisho ya imani, vianzo vya mafundisho, na mtazamo wa ulimwengu wa umisheni.

Wakati wa leo kuna makanisa mengi na mchanganyiko mbalimbali wa mafundisho ya kiimani, ingawaje wanadai kwamba yanafuatana na Biblia. Kwa kanisa kuwajibika kwa ajili ya kanisa la ulimwengu haimaanishi kwamba ni lazima lijitahidi kufanana na makanisa mengine yote yanayolizunguka. Kinachohitajika hapa ni kushikamana na mafundisho yote ya imani kwa ajili ya Ukristo ambayo yalikuwa ni muhimu wakati wa kuanza kwa kanisa la Agano Jipya. Ni lazima kanisa pia liwe sehemu ya jumuiya ya makanisa ambayo yanawajibika kwa ajili ya kila mmoja na mwenzake.

Kwa ajili ya kuwa na uthabiti wa mafundisho ya imani, Kanisa la mtaa linapaswa lizingatie mambo matatu:

1. Kuwa na imani kwamba Biblia ndiyo mamlaka iliyo kamili.
2. Mafundisho ya imani yaliyokuwa muhimu katika historia ya Ukristo.
3. Kuwa na ushirika na jumuiya ya makanisa yaliyo na teolojia nzuri inayokubalika.

Katika somo hili tunajifunza kipengele cha pili kutoka katika vipengele vitatu vilivyooanishwa katika orodha ya hapa juu. Tutazungumzia kuhusu jumuiya za makanisa kwenye somo lingine.

Kanisa la mtaa halipaswi kujiona kwamba liko huru kukubaliana na mafundisho yeyote ya imani yaliyo kinyume na mafundisho ya imani ya Ukristo ambayo yalikuwa ni muhimu wakati wa kanisa la kwanza. Mafundisho hayo yameelezwa kwenye ukiri au unaweza kusema matamko ya Imani ya mwanzoni. Imani ya Mitume, Imani ya Nikea, na imani ya Kalsedonia zinaelezea mafundisho ya imani ambayo yalikuwa ni muhimu kwa Ukristo tangu

mwanzo. Hii ni pamoja na imani ya mafundisho ya Utatu Mtakatifu wa Mungu, uungu wa Kristo na kuhusu Roho Mtakatifu. Endapo kuna kanisa linalokataa mafundisho haya ya mwanzo ya imani, halipaswi kujiita lenyewe kuwa ni la Kikristo, kwa sababu hilo litakuwa ni dini tofauti.

### Imani ya Nikea

> Nina mwamini Mungu mmoja, Baba Mwenyezi, Muumba wa mbingu na nchi na vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana.
>
> Na katika Bwana mmoja, Yesu Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu, Mwana pekee wa milele wa Baba; Yu Mungu kutoka Mungu, Yu nuru kutoka nuru, Yu Mungu kweli kutoka Mungu kweli; Mwana wa milele asiyeumbwa, mwenye uungu mmoja na Baba: Kwa yeye huyu vitu vyote viliumbwa. Aliyeshuka mbinguni kwa ajili yetu wanadamu na kwa wokovu wetu; akatwaa mwili kwa uweza wa Roho Mtakatifu katika Bikira Mariamu, akawa mwanadamu; Akasulubiwa kwa ajili yetu zamani za Pontio Pilato; Aliteswa, akazikwa. Siku ya tatu akafufuka kama yanenavyo Maandiko Matakatifu: Akapaa mbinguni; ameketi mkono wa kuume wa Baba; Naye atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio hai na wafu. Na ufalme wake hauna mwisho.
>
> Na nina mwamini Roho Mtakatifu Bwana mtoa uzima, atokaye katika Baba na Mwana; anayeabudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana; aliyenena kwa vinywa vya manabii. Na nina aamini kanisa moja, takatifu, (katholiko) la Kikristo la ulimwengu wote na la kimitume. Nina kiri ubatizo mmoja na ondoleo la dhambi. Nina tazamia ufufuo wa wafu na uzima wa ulimwengu ujao. Amen.

Je, itakuwaje kama mtu ataamua kutokukubaliana na mojawapo ya maelezo yaliyoko kwenye Imani ya Nikea? Kwa kuwa imani hizi zimeshikiliwa na kanisa tangu mwanzo, kama ataamua kukataa mojawapo ya hizi, atakuwa anajinadi kuwa ana uelewa wa kweli ambao kanisa halikuwahi kuwa nao kwa miaka 2000. Kama kanisa au mtu binafsi hawezi kushikamana na imani zilizoko kwenye Imani ya Mitume, Imani ya Nikea, na Imani ya Kalsedonia, imani yake haistahili kuaminika. Imani zote zilizoko hapa zinaunga mkono injili. Ikiwa mtu anakataa mojawapo ya mafundisho haya, anaweza kuwa anaichanganya injili.

► Je, utasema nini kwa mtu anayesema kwamba yeye ni Mkristo lakini hakubaliani na maelezo yaliyoko kwenye Imani ya Nikea?

**Taarifa Saba kwa Muhtasari**

1. Kanisa la mahali ni kundi la waumini ambao wamejitoa kuwa pamoja kuwa kanisa katika eneo waliko.
2. Kanisa linadhihirisha asili ya Mungu kwa ulimwengu.
3. Maisha ya Roho ni maisha na umoja wa kanisa.
4. Uanachama wa kanisa una msingi wake kwenye uhusiano na Mungu na kujitoa kwa ajili ya kundi la waumini.
5. Kuna kanisa moja tu la ulimwengu wote linalofuata Ukristo wa aina moja kwa sababu kanisa ni kuhusiana na Mungu mmoja.
6. Hakuna shirika lolote la kibinadamu ambalo linaweza kuwa ni kanisa lote la Mungu katika ulimwengu.
7. Kanisa la mahali ni lazima lishikamane na imani zote muhimu na za kihistoria za kanisa la ulimwengu wote.

**Kazi za kufanya Somo la 1**

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 1. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Wakati wa kozi hii, utahitajika kufundisha somo, au sehemu ya somo, kwa mtu binafsi au kikundi ambacho siyo sehemu ya darasa lako. Unaweza kuchagua maudhui ya kufundisha. Itakupasa ufanye hivyo mara tatu, kwa kutumia mafundisho tofauti. Fanya mpangilio wako mwenyewe wa nafasi za kufundisha na toa taarifa kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.

# Somo la 2
# Umoja wa Kikristo

## Utangulizi

► Itampasa mwanafunzi asome hadithi ifuatayo ya kufikirika kwa ajili ya darasa.

Wakati mmoja kulikuwepo na jiji ambalo lilikuwa hatarini kukumbwa na mafuriko ya mto. Watu wa jiji hilo walijipanga katika vikundi mbalimbali vya kujaza mifuko ya mchanga na kuiweka kwenye kingo za mto huo. Watu walifanya kazi kwa shauku kubwa, na hamasa ya kila kikundi iliongezeka. Baadaye vile kikundi vilijipa majina. Kulikuwa na kikundi cha waokoaji wa jiji, Wasawazishaji Mchanga, na Wathibiti Mto. Utambulisho wa kikundi ulikuwa jambo muhimu sana. Wanachama wa kila kikundi walivaa fulana zinazofanana. Walizungumzia ni kwa jinsi gani kikundi kimoja kilikuwa ni bora kuliko kikundi kingine. Kila kikundi kililaumu kazi ya kikundi kingine.

Wakati kikundi cha wathibiti Mto kilipokwenda kuomba toroli kutoka kwenye kikundi cha Waokoaji wa Jiji, hawakuwaruhusu kulichukua toroli hilo, kwa sababu walidhania kwamba wanaweza wakalihitaji tena baadaye. Wakati kikundi cha Wasawazishaji Mchanga walipopungukiwa na mifuko ya kuwekea mchanga, ilibidi wasubiri kwa takribani saa moja kwa ajili ya mifuko kuletwa, ingawaje vikundi vingine vilikuwa na mifuko ya ziada. Vikundi vyote vilikuwa vimejisahau kwamba wote kwa pamoja walikuwa na jukumu moja. Mafanikio ya kila kikundi yalionekana ni muhimu zaidi kuliko matokeo ya ujumla ya jukumu lote lililokuwepo.

► Ni kwa jinsi gani makanisa yanafanya kama ilivyokuwa kwa vikundi vilivyoko kwenye hadithi hii?

Biblia inasisitiza kwa kina sana kuhusu thamani ya umoja wa Kikristo. Paulo alikemea utengano au mafarakano ya kanisa la Korintho kwa kuuliza swali, "Je! Kristo amegawanyika?" (1 Wakorintho 1:13). Aliwaambia Waefeso kudumisha umoja wa Roho. Akionyesha kwamba, "Mwili mmoja... Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja" (Waefeso 4:4-5). Yesu aliomba kwa bidii sana ili kwamba waumini kuwa kitu kimoja, ili ulimwengu upate kuamini kwamba Yesu alitoka kwa Baba (Yohana 17:21).

Tangu mwanzo, kanisa lilijifikiria lenyewe kuwa ni moja. Imani ya Mitume inahusisha pamoja na taarifa hii: "Naamini… kanisa takatifu la Kikristo (katholiko) lililo moja tu; ushirika wa watakatifu." Imani ya Nikea inahusisha pamoja na taarifa hii: "Twaamini Kanisa moja (katholiko) la Kikristo la ulimwengu wote na la kimitume." Neno *katholiko* lina maana ya kamilifu na ulimwengu wote. Neno *kimitume* linamaanisha kwamba kanisa lilianzishwa na mitume na hata sasa linafuata mafundisho ya mitume.

Matamko ya imani ya awali yalionyesha imani muhimu za mafundisho ya Kikristo. Kanisa halikuhusika na mtu yeyote ambaye hakukubaliana na matamko haya ya imani, kwa kuwa yalikuwa yamekusudiwa kutoa ufafanuzi wa mambo muhimu ya Ukristo. Kwa hiyo, mtu alionekana kuwa ni mwenye ukengeufu kama alikuwa anafikiria kwamba kuna makanisa ya kweli ambayo siyo sehemu ya kanisa moja la ulimwengu wote.

## Madhehebu

Kanisa duniani halijawahi kuundwa likawa shirika moja kwa karne nyingi. Badala yake, kuna makundi mengi ya makanisa yanayotofautiana. Kundi moja la makanisa linalounda shirika moja linaitwa dhehebu.

Katika mwaka 451 B.K. Othodoksi ya Mashariki lilijiengua kutoka katika Ukatoliki wa Kirumi kwa sababu ya kutokubaliana katika mafundisho ya imani. Leo hii kuna mashirika mengi ya makanisa katika Othodoksi ya Mashariki: Koptiki, Othodoksi ya Ethiopia. Othodoksi ya Eritrea, Malankara ya Syria, Syriaki, na dhehebu la kitume la Armenia.

Katika mwaka 1054 B.K. Othodoksi ya Mashariki lilijiengua kutoka katika Ukatoliki wa Kirumi. Leo hii kuna mashirika kumi na tano ya makanisa katika Othodoksi ya Mashariki ikiwa ni pamoja na Kanisa la Kiothodoksi la Urusi, Kanisa la Kiothodoksi la Serbia, na Kanisa la Kiothodoksi la Syprusi.

Mbali na mgawanyiko huu mkubwa, makundi mengine ya makanisa katika karne zile yalijiengua kutoka katika kanisa Katoliki.

Matengenezo ya Kanisa la Kiprotestanti yalitokea mnamo miaka ya 1500. Makanisa mengi yalijiengua kutoka katika Ukatoliki wa Kirumi kwa sababu waliamini kwamba Kanisa Katoliki halihubiri tena wazi wazi injili ya kweli. Kulikuwa na mambo mengine mengi, yakiwemo mambo ya kisiasa, lakini mafundisho ya imani ndiyo yaliyokuwa muhimu zaidi.

Madhehebu mengi yaliundwa kutoka katika Matengenezo. Kanisa la Uingereza liliundwa na makanisa mengi yaliyokuwepo katika nchi ya Uingereza. Ilipotokea kuanzishwa kwa makanisa yao katika nchi nyingine nje ya Uingereza, yalijulikana kama Kanisa la Kiangilikana.

Makanisa ya Wapresibiteri yalitokana na ushawishi wa wana Matengenezo: Yohana Calvin nchini Switzerland, Yohana Knox nchini Scotland, na wengineo. Siku hizi kuna madhehebu mengi ya Wapresibiteri.

Kanisa la Kilutheri lilianzishwa nchini Ujerumani kutokana na huduma ya Martin Luther. Kuna makanisa mengi ya Kilutheri kwa sasa katika nchi mbalimbali duniani.

Wafuasi wa Anabaptisti waliamini kwamba matengenezo hayakukamilisha urejeshwaji wa injili ya kimaandiko. Waliamini kwamba kuabudu hakupaswi kuwa ni sherehe zisizokuwa za kimaandiko na kwamba ubatizo ulipaswa uwe tu ni kwa ajili ya watu waliookoka na siyo kwa watoto wadogo. Kutokana na wao, kumejitokeza madhehebu mengi ya Kibaptisti katika nchi mbalimbali duniani.

Makanisa ya Kipentekoste yalianza kutokana na Uamsho mkubwa uliofanyika Los Angeles Marekani mnamo mwaka wa 1906. Mchanganyiko mkubwa wa madhehebu ya Kipentekoste na Karismatiki yapo katika maeneo mengi ya dunia. Madhehebu haya yana mchanganyiko wa aina nyingi za mafundisho ya imani.

Yako madhehebu mengi kwa maelfu ambayo yanajinadi kwamba wao ni Wakristo. Yako makanisa mengi yaliyo huru ambayo siyo sehemu ya madhehebu.

Mara nyingi madhehebu yanaanza na kikundi cha watu ambao wanaamini kwamba ukweli fulani umekataliwa au umepuuzwa na kanisa wanaloshiriki. Wanaanza na dhehebu dogo kwa nia ya kutaka kuwa sahihi katika mafundisho ya imani. Wakati mwingi wanaendelea kutengeneza mafundisho yao ya imani, na wanakuwa tofauti na madhehebu mengine. Pia wanatengeneza mila tofauti kuhusu namna sahihi ya ibada na mambo ya kina yanayohusiana na jinsi ya kuishi Kikristo.

Wakati mwingine madhehebu huanza kwa kufanywa huduma ya uinjilisti. Kama kutatokea kuwepo na watu wengi waliookoka katika eneo hilo na hakuna dhehebu litakaloweza kuendelea kuwatunza, dhehebu jipya linaweza kuanzishwa. Dhehebu linaweza kuanza kutokana na kazi ya shirika la umisheni katika nchi maalumu husika.

Madhehebu mengi ya Kikristo hayajinadi kama ndiyo pekee Wakristo wa kweli. Kama shirika litajinadi kwamba ndilo kanisa lote la Mungu katika ulimwengu, halipaswi kuwa la kuaminika.

► Je, kuna aina ngapi tofauti za majina ya makanisa na madhehebu unazozifahamu?

Watu wasioamini wanapingana na Ukristo kwa sababu ya mgawanyiko wake mwingi uliopo na aina nyingi zilizopo. Watu wengi wasioamini wanafikiri kwamba aina mbalimbali za vikundi vyote vya Kikristo vinajichanganya kimoja kwa kingine. Watu wengi wa dunia wanafikiri kwamba hakuna aina ya umoja unaoeleweka miongoni mwa Wakristo.

► Je, kuna tabia gani ambazo zinaonekana kama zinakataa umoja miongoni mwa makanisa?

Makanisa yanaonekana kuwekea mkazo mambo ambayo yanafanya yaonekane kuwa tofauti na makanisa mengine, hata kama mambo hayo siyo mafundisho ya msingi ya imani. Wakati mwingine makanisa huharakisha kulaumu makanisa mengine kwa ajili ya unafiki na kukubaliana katika mambo yasiyotakiwa kukubaliana, au dhambi nyinginezo, bila ya kuelewa kwa uhakika. Baadhi ya makanisa husema kwamba makanisa mengine siyo ya Kikristo, ingawaje yanaamini kwenye msingi wa mafundisho ya imani ya Ukristo.

Makanisa hayaonekani kuwa yenye umoja katika kuendelea Agizo Kuu la Yesu. Makanisa yanaonekana kushindana kama yanayofanya biashara. Viongozi wengi hudhania kwamba ni kupoteza nguvu na mapato yao kama watajihusisha katika kusaidia huduma ambazo hazina majina ya mashirika yao.

Labda Wakristo wote watakubaliana kwamba Wakristo wote wanapaswa wawe na umoja, lakini wanaweza wasijue ni aina gani ya umoja unaotakiwa. Kwanza, tutazungumzia kuhusu umoja wa kanisa la duniani kote; kisha, tutazungumzia kuhusu umoja wa Kanisa la mahali/mtaa.

## Umoja wa Kanisa la Duniani Kote: Siyo Muungano wa Mashirika

Baadhi ya watu wanafikiri kwamba makanisa yote yanapaswa yaungane yawe shirika moja. Wanafikiri kwamba uwepo wa mashirika mengi yaliyojitenga yenyewe inamaanisha kwamba kanisa haliko katika umoja. Hawatofautishi kati ya kiini au kitovu cha kanisa na mashirika ya kanisa; kwa hiyo, kwao inamaanisha umoja ni kuungana kwa mashirika.

► Je, utasema nini kwa mtu anayefikiria kwamba Mashirika na Makanisa yote ye Kikrsto yanapaswa yaungane yawe shirika moja?

Mashirika hayawezi yakaunganika bila ya kuamua kwamba tofauti zao za mafundisho ya imani siyo kitu cha kuzingatia. Kuwa na umoja ni lazima kuwepo na kukubaliana kwenye baadhi ya mafundisho ya misingi ya imani, na iamuliwe kwamba wingi wa mafundisho yao mengine ya imani hayana umuhimu sana wa kutosha kuwatenganisha kutokana na wale wasiokubaliana nao.

Jaribio lote zima la kutaka kuunganisha makanisa yote yawe katika shirika moja yako kwenye msingi kwamba umoja wa Kikristo ni umoja unahusiana na Mashirika. Yesu mwenyewe hakuwahi kudai kwamba wafuasi wake wote wawe kwenye shirika moja linalofanana wakati wa huduma yake hapa duniani, kama inavyoonekana katika tukio hili hapa chini:

> Yohana akajibu akamwambia; Bwana mkubwa, tuliona mtu anatoa pepo kwa jina lako; tukamkataza, kwa sababu hafuatani na sisi. Yesu akamwambia, Msimkataze, kwa kuwa yeye ambaye si kinyume chenu yu upande wenu (Luka 9:49-50).

Maneno haya ya Yesu yanaonyesha kwamba mtu anaweza akawa "hafuatani na sisi" (siyo sehemu ya shirika letu), lakini bado akawa "yu upande wetu." Ni wazi kwamba, kuna umoja wa Kikristo ambao hauoneshi kwamba kuna uwepo wa kuwa katika shirika moja.

Kwa karne nyingi tangu wakati wa huduma ya Yesu hapa duniani kumekuwepo na mashirika mengi yaliyojinadi kwamba ni kanisa la dunia nzima, wakisema kwamba hakuna mashirika mengine yasiyokuwa pamoja nao yanayopaswa kudai kwamba wao ni Wakristo. Yesu hakuwahi kudai kwamba kundi lake la wanafunzi ndilo kanisa lote hata wakati ambapo alikuwa pamoja nao kimwili akiwaongoza.

Wakati mwingine watu hutumia neno *kanisa lisiloonekana*. Neno *kanisa lisiloonekana* linarejelea kwenye ukweli kwamba hakuna shirika linaloonekana kuwa na orodha ya wanachama yenye kujumuisha wakristo wote. Pia, mashirika ya Kikristo yana wanachama ambao siyo Wakristo wa kweli. Kwa hiyo, hatuwezi kuelekeza kwa shirika lolote maalumu na kusema kwamba hili ndilo kanisa la ulimwengu wote.

Ingawaje kanisa la dunia siyo shirika moja, umoja miongoni mwa Wakristo wote unapaswa uwe unaonekana. Yesu aliomba kwamba waumini wawe na umoja na akasema kwamba matokeo yatakuwa kwamba dunia itamwamini yeye (Yohana 17:21). Hii inamaanisha kwamba umoja wa Kikristo unapaswa kwa namna fulani uwe unaonekana kwa Wakristo na ulimwengu wote.

► Je wakati unapokutana na mtu anayejinadi kwamba mimi ni Mkristo, ni mambo gani muhimu kwako unayoweza kushirikishana naye kuhusiana na umoja wa Kikristo?

### Msingi wa Umoja wa Kikristo

Umoja wa Kanisa la mahali uko kwenye msingi wa mafundisho ya imani ya Biblia, uzoefu wa neema, na maisha ya Roho Mtakatifu. Umoja wa Wakristo mbali na Kanisa la mahali una msingi unaofanana, ingawaje undani wake ni mdogo.

Njia nyingine ya kuweza kuelezea msingi wa umoja ni hii: Kama mtu atashuhudia kwamba ameokoka, ikaonekana ana maisha ya kiroho, na ikaonekana anaamini katika misingi ya Ukristo wa kweli, basi ushirika wa Kikristo unawezekana. Ushirika unaweza ukaendelea kwa muda wote ali mradi mtu anaonekana kuishi kwenye ushirika na Mungu na katika kuitii Biblia.

Umoja wa Kikristo hautegemei kuwepo na kukubaliana na kila kipengele cha mafundisho ya imani. Siyo jambo rahisi kwa Kanisa katika maeneo yote kukubaliana mambo yote kwa undani yanayohusiana na mafundisho ya imani. Hata mitume walikuwa na mambo ambayo hawakukubaliana (Wagalatia 2:11-14).

Makundi ya waumini hujifunza Biblia na kujadiliana katika yale wanayoamini, wakijaribu kuhakikisha kwamba yako sahihi. Wanatambua kwamba hawakubaliani na mafundisho ya imani ya baadhi ya makundi mengine ya Wakristo.

Yapo baadhi ya mafundisho ya imani ambayo ni ya msingi na ya muhimu kwa imani ya Mkristo. Kama mtu hataamini haya mafundisho ya imani, hawezi akaelewa na kuiamini injili.

Kisha kuna orodha ndefu ya mafundisho ya imani ambayo kanisa fulani huamini. Makanisa mengi yanaelewa kwamba, siyo Wakristo wote katika maeneo yote wanaokubaliana na mafundisho yote ya imani. Hata kama fundisho la imani liko katika Biblia, siyo kila mtu atakayeweza kuielewa Biblia kwa njia inayofanana.

► Je, mifano ya msingi ya mafundisho ya imani ni ipi? Kuna mifano gani mingine ambayo siyo ya msingi?

> " Kama moyo wako uko sahihi, kama moyo wangu na wako ulivyo, basi nipende kwa upendo wa moyo wako, kama rafiki wa karibu kuliko kaka mtu; kama kaka katika Kristo, raia mwenzako wa Yerusalemu mpya, askari mwenzako anayepigana vita vinavyofanana, chini ya akida yule yule wa wokovu wetu. Nipende kama mshiriki mwenzako katika ufalme na subira ya Yesu, na mrithi wa pamoja wa utukufu wake."
>
> - John Wesley,
> "Roho ya Umoja" *("The Spirit of Unity")*

Baadhi ya misingi ya imani ni kuhusiana na asili ya Mungu, Uungu wa Yesu na Roho Mtakatifu, Kufa na kufufuka kwa Kristo, na wokovu ni kwa neema kwa njia ya imani.

Baadhi ya mafundisho ya imani ambayo siyo ya msingi ni imani kuhusiana na aina za kuabudu na undani wa maisha ya Kikristo. Ni muhimu kwetu kuwa watu wa kibiblia zaidi katika kufanya mambo yote, lakini tunapaswa tutambue kwamba siyo Wakristo wote wa kweli watakaoweza kukubaliana na undani wa mambo haya yote.

## Ishara za Kanisa la Kweli

Mtazamo wa ishara za kanisa la kweli ulishikiliwa kwa pamoja na Kanisa Katoliki na wanamatengenezo. Kwa karne nyingi Wakristo walikuwa wakiamini kwamba ishara nne za kanisa la kweli ni umoja, utakatifu, ukatoliki, na utume. Maneno haya manne yamekuwa yakitafsiriwa kwa njia tofauti.

Hapa kuna tafsiri chache rahisi. *Umoja* inamaanisha kwamba kanisa linahusisha Wakristo wote wa kweli, ingawaje siyo lazima wawe kwenye orodha rasmi. *Utakatifu* inamaanisha kwamba kanisa linasimama kinyume na dhambi na linaamini kwamba wokovu ni kuachana na mambo ya dhambi. *Ukatoliki* inamaanisha kwamba linaweza kuchukua muundo unaofaa kwenye utamaduni yeyote mahali popote, wakati likiendelea kushikilia kwenye ukweli muhimu. *Utume* inamaanisha kwamba kanisa linashikilia kwenye imani yake ya asili iliyoanzishwa na mitume.

## Kosa la Kanisa Kushindana

Wakati mwingine makanisa katika maeneo yanakuwa karibu karibu sana kiasi kwamba watu wanaweza wakachagua ni kanisa gani la kwenda. Watu katika kanisa moja wanaweza kujaribu kuonyesha kwa jamii kwamba kanisa lao ni bora zaidi kuliko makanisa mengine yote. Wanashindana na makanisa mengine, wakijaribu kulifanya kanisa lao liwe la kuvutia zaidi kuliko makanisa mengine. Wanafikiri kwamba kanisa lao lina mafanikio zaidi kama idadi ya watu itakuwa inaongezeka.

Mashindano baina ya makanisa yako kwenye msingi wa kukosa uelewa wa kanisa. Watu wengi wanaelekea kufikiri kwamba kanisa ni kama biashara ambayo inapaswa iwe kivutio kwa watu wengine au wateja wake. Au, ni kama eneo la maonyesho ambalo linapaswa liweze kuwa kivutio kwa hadhira. Haya yote ni mitazamo potofu kuhusiana na kanisa.

Kanisa ni familia ya kiroho. Wanachama wa familia nzuri kila mmoja hujaribu kuchukua jukumu la kumjali mwenzake. Wanafanya kazi pamoja kwa ajili ya kupata vigezo vya familia. Wanatumia muda wao wakiwa pamoja kwa sababu ya uhusiano wao.

Kanisa ni familia ya watu wenye imani, yenye msingi wake kwenye uhusiano na Mungu pamoja na wao wenyewe. Wanahitaji wanachama wapya ambao watakuwa wamevutiwa na injili na maisha ya kiroho ya familia hiyo. Kanisa linapaswa liwe na mwelekeo wa kushirikisha injili na kudhihirisha uhai wa kanisa. Kisha watawavutia watu walio sahihi, watu ambao wako tayari kuwa sehemu ya familia hiyo.

► Je, kama kanisa linajaribu kushindana na makanisa mengine yaliyoko kwenye eneo moja, ni kwa jinsi gani mashindano hayo yataweza kulibadilisha kanisa?

## Umoja wa Kanisa la mahali.

► Je, ni kwa nini Kanisa la mahali linahitaji makubaliano ya mafundisho mengi zaidi ya imani kuliko umoja wa Kikristo wa dunia?

Mkristo anaweza akakubaliana na ushuhuda wa Wakristo wengine ambao hawashikamani na mafundisho yake yote ya imani, ali mradi yawe yanashikamana na msingi wa mafundisho ya imani ya Kikristo na yanadhihirisha maisha ya Kikristo. Hata hivyo, kwa kuwa Mkristo ni lazima yeye binafsi ayafanyie kazi yale anayoamini kwamba ni sahihi, hawezi akajiunga katika huduma ya Wakristo wa aina zote. Kwa mfano, kama mchungaji anaamini kwamba Biblia inamwambia abatize watu waliookoka, hawezi akawa mchungaji wa watu ambao wanafundisha kwamba watu wanaookoka hawatakiwi kubatizwa.

Mfano mwingine: Kama mtu anaamini kwamba karama ya kunena kwa lugha siyo ushuhuda wa mtu kuwa amejazwa na nguvu za Roho Mtakatifu, itakuwa ni vigumu kwake kushikamana na huduma ya watu ambao wanaamini kwamba mtu ambaye hazungumzi kwa lugha hana nguvu za Roho Mtakatifu. Kutakuwepo na matatizo katika ushirika wao kwa sababu hawatakubaliana na ushuhuda wake. Kutakuwepo na matatizo katika ushirikiano kihuduma kwa sababu watakuwa wanajaribu kuwaongoza watu wapya waliookoka kwenye uzoefu wa kuzungumza kwa lugha.

Kama mtu atakuwa anafanya mambo ambayo anajua kwamba kibiblia ni makosa, atakuwa anakiuka dhamira yake mwenyewe. Anakuwa amejiweka mwenyewe chini ya hukumu ya Mungu kwa sababu amechagua kufanya jambo fulani ambalo anaamini kabisa kwamba Biblia imelikataza (tazama Warumi 14:22-23).

Mkristo anaweza akaamini kwamba watu wanaoamini mafundisho ya imani mbali mbali, ndiyo Wakristo wa kweli na sahihi, lakini ni lazima awe kwenye ushirika na kufanya huduma kwenye kundi la watu wanaokubaliana na mafundisho mengi zaidi ya imani. Hii inamaanisha kwamba Kanisa la mahali ni lazima liwe na tamko la fundisho la imani litakalokuwa zaidi ya mafundisho ya msingi ya kanisa la ulimwengu wote.

► Je, kwa nini inakuwa ni makosa kwa mtu kujaribu kuamini kila mafundisho ya imani ya makanisa?

## Hitimisho

Mkristo ni lazima aweke uwiano wa tabia yake dhidi ya watu wengine. Hawezi akasema kwamba Wakristo wengine siyo Wakristo wa kweli kwa sababu ya kutofautiana kwenye mafundisho ya imani madogo madogo ambayo siyo yale ya msingi. Hata hivyo, Mkristo ni lazima awe na ushirika wa karibu na Kanisa la mahali ambalo linasimamia mafundisho ya imani kwa pamoja ambayo yanawawezesha kufanya ushirika na huduma pamoja.

## Taarifa Saba kwa Muhtasari

1. Biblia imeweka mkazo kuhusu Umoja wa Kikristo.
2. Kanisa la kwanza liliamini katika umoja wa kanisa kama fundisho la imani la msingi.
3. Kanisa haliwezi kukamilisha umoja kwa kuwaweka Wakristo wa mashirika yote katika shirika moja.
4. Umoja wa Kikristo una msingi wake kutoka katika fundisho la Biblia, uzoefu wa neema, na maisha ya Roho Mtakatifu.
5. Wakristo mahali popote wanakubaliana kwenye baadhi ya mafundisho ya imani ya msingi ya Ukristo.
6. Wakristo katika makanisa mbalimbali hawatakubaliana juu ya maelezo ya kina ya mafundisho ya imani.
7. Kanisa la mahali ni lazima likubaliane na maelezo ya kina ya mafundisho mbalimbali ya imani.

## Kazi za Kufanya Somo la 2

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 2. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Wakati wa hii kozi, utahitajika kufundisha somo, au sehemu ya somo, kwa mtu binafsi au kikundi ambacho siyo sehemu ya darasa lako. Unaweza kuchagua maudhui ya kufundisha. Itakupasa ufanye hivyo mara tatu, kwa kutumia mafundisho tofauti. Fanya mpangilio wako mwenyewe wa nafasi za kufundisha na toa taarifa kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.
3. Masailiano: Ongea na washirika wa makanisa matatu tofauti na uwaulize ni kwa jinsi gani wanavyoyaona makanisa mengine. Je, ni umoja gani wanaofikiria kwamba utafaa kuwepo miongoni mwa Wakristo wote? Andika ibara moja inayohusiana na mazungumzo uliyoyafanya na kila mmoja wa watu hawa watatu.

# Somo la 3
# Kanisa la Mahali

## Utangulizi

► Je, kanisa la mahali ni kitu gani? Je, lina tofauti gani na aina nyingine zote za vikundi?

Tafsiri hii ya kanisa la mahali inaweza kugawanywa kwenye maeneo makuu saba muhimu. Maeneo haya yanaelezewa kwa uwazi zaidi katika kozi hii yote.

**Ufafanuzi ya Kanisa la mahali**

Kanisa la mahali ni kikundi cha waumini ambacho kinafanya kazi kama familia ya kiroho na jamii ya imani; wakitoa injili na ushirika wa kanisa kwa kila mtu anayetubu; wakitekeleza tendo la ubatizo na ushirika wa meza ya Bwana, wakishirikiana katika kumwabudu Mungu, ushirika, uinjilisti, uanafunzi, na kukamilisha kazi ya mwili wa Kristo kwa karama za Roho Mtakatifu; waliojitoa kabisa kwa ajili ya Neno la Mungu; wakiwa na umoja ulio katika msingi wa mafundisho ya imani ya kibiblia, wakiwa na uzoefu wa neema, na maisha ya Roho Mtakatifu.

Hapa chini sehemu za tafsiri hiyo zimerejewa zikiwa na maelezo yaliyofuatana nazo.

> "Watu walioamini hawajaitwa kibinafsi kuishi tu kwa kuwa na uhusiano binafsi na Mungu bali wameitwa kwa pamoja na kushikamanishwa kwa pamoja kama watu."
>
> - Thomas Oden, *Life in the Spirit*

► Kwa kila kipengele kinachofuata, jadili ni kwa nini ni muhimu kuwepo na tabia hii ya kanisa. Je, ni matokeo gani yatakayoonekana kama kanisa litakosa kuwa na tabia hii?

**Kanisa la mahali ni kikundi cha waumini ambacho kinafanya kazi kama familia ya kiroho na jamii ya imani…**

Kanisa ni kikundi kilichoanzishwa kutokana na imani ya Kikristo. Kina mahusiano mazito kuliko hata kikundi kingine katika dunia.

> "Kanisa la Kristo linaloonekana ni mkusanyiko wa watu waaminifu ambao Neno kamilifu la Mungu linahubiriwa na sakramenti zinatolewa kwa mujibu wa agizo la Kristo…"
>
> - *Kanuni za Dini za Kanisa la Methodisti*

**…wakitoa injili na ushirika wa kanisa kwa kila mtu anayetubu…**

Kanisa haliwezi kuwatenga watu wa kikundi cha utamaduni fulani au kabila fulani au kwa madaraja ya watu na bado likandelea kuwa mwaminifu kwa injili. Hakuna umuhimu wa mambo ya utamaduni au kabila, au madaraja ya kijamii. Pia, kanisa haliwezi kukataa

kusamehe baadhi ya dhambi kama limesimama kwenye uaminifu wa injili.

**…wakitekeleza tendo la ubatizo na ushirika wa meza ya Bwana…**

Yesu alitoa maagizo kwa kanisa kwa ajili ya kutekeleza sherehe hizi. Ubatizo unawakilisha kuingia katika kanisa kwa kuokoka. Ushirika wa meza ya Bwana unamaanisha neema inayodhihirishwa kutoka katika injili.

**…wakishirikiana katika kumwabudu Mungu, ushirika, uinjilisti, na uanafunzi…**

Haya ni makusudi ya msingi ya kanisa. Ushirikiano ni muhimu kwa ajili ya kanisa kukamilisha makusudi muhimu.

**…kukamilisha kazi ya mwili wa Kristo kwa karama za Roho Mtakatifu…**

Majukumu ya kiroho ya kanisa kamwe hayawezi kukamilishwa kwa uwezo wa kibinadamu peke yake.

**…waliojitoa kabisa kwa ajili ya Neno la Mungu…**

Kanisa linaitegemea Biblia kwa ajili ya injili yake, mafundisho ya imani, na mamlaka. Kama kanisa litachagua kutokuitii Biblia, kanisa litakuwa limepoteza mamlaka yake kwa ajili ya kufundisha.

**…wakiwa na umoja ulio katika msingi wa mafundisho ya imani ya kibiblia, wakiwa na uzoefu wa neema, na maisha ya Roho Mtakatifu.**

Washirika wa kanisa wanaweza wakajikabidhi mmoja kwa ajili ya mwingine kwa sababu wanayo haya mambo matatu kwa pamoja. Bila ya haya mambo matatu, ushirika wa kweli wa Kikristo hautawezekana kuwepo.

## Uwekezaji wa Mungu kwa Kanisa

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Waefeso 3:1-10 kwa ajili ya kikundi. Je, kuna baadhi ya mambo gani ambayo Paulo aliyasema kuhusiana na huduma yake?

Paulo alisema kwamba sehemu muhimu ya huduma yake ilikuwa ni kuelezea kuhusu kanisa, kwa hiyo tunaelewa kwamba kuelezea kanisa kunapaswa kuwe ni sehemu muhimu ya huduma kwa wakati wa sasa. Mungu alipanga kwamba watu wanaoamini kutoka kwa Mataifa waletwe kwenye nyumba ya Bwana (Kanisa) na kwamba kanisa litapaswa lidhihirishe hekima ya Mungu kwa ulimwengu.

Tunapaswa tukumbuke kwamba kanisa siyo jengo. Wakristo hawakuwa na majengo kwenye vizazi kadhaa vya mwanzo vya kanisa. Hii ina maana kwamba wakati kitabu cha Agano Jipya kinapokuwa kinazungumzia kuhusu kanisa, kinazungumzia kuhusu watu.

Waefeso hueleza jinsi kanisa lilivyo muhimu kwa mpango wa Mungu.

> …Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote (Waefeso 1:22-23).

Aya hii inasema kwamba Yesu ni kichwa cha kanisa, na kwamba kanisa ndiyo mwili. Inasema kwamba kanisa lina ukamilifu wote wa Mungu.

Jaribu kufikiria kuhusu mto ambao unatoa maji yake yote kwa ajili ya jiji kubwa. Mamilioni ya watu wanayatumia maji hayo, lakini kiasi cha maji wanachotumia ni kidogo kuliko kiasi cha maji kinachotiririka kwenda katika mto. Ni vigumu sana kuweza kufikiria ni kiasi gani cha maji kilichopo.[2]

Lakini inakuwaje kuhusu ukamilifu wa Mungu? Kama ingekuwa Mungu angetengeneza konteina au mfereji wa kumwagia baraka zake na neema yake na nguvu zake kwa ajili ya ulimwengu, ni konteina ya aina gani ambayo ingeweza kushikilia ukamilifu wa Mungu? Aya hii inasema kwamba kanisa ndiyo hiyo konteina. Kanisa lina baraka za Mungu kwa ajili ya ulimwengu.

Kumbuka kwamba, kanisa lililo na baraka za Mungu siyo jengo, bali kundi la watu lililo katika ushirika wa Kikristo.

Mpango wa Mungu kwa ajili ya kanisa ulikuwepo tangu mwanzo wa dunia. Kwa ajili hiyo, Mungu alikuwa na kusudi gani katika ufahamu wake kwa ajili ya kanisa?

Angalia tena Waefeso 3:10-11.

> Ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu.

*Namna nyingi* inamaanisha “aina zote.” Mungu anazo hekima kwa kila hali na kwa kila kipengele cha maisha. Hekima ya Mungu inapaswa idhihirishwe kwa ulimwengu wote, ikiwa ni pamoja na ulimwengu wa kiroho, kwa yale ambayo Mungu anayafanya kupitia kwa kanisa. Mtu hupata ufahamu wake kuhusiana na Mungu kwa kile anachokiona katika kanisa. Kwa kuliona kanisa kunamfanya mtu amwabudu Mungu. Anapaswa aione hekima ya Mungu ikitenda kazi ndani ya kanisa. Dunia haiwezi kuyaona haya yote kutoka kwenye ibada za Jumapili. Wanayaona yote kupitia matendo ya kanisa ya kila siku na kwenye kila hali ya maisha.

► Je, kuna baadhi gani ya mifano ya hali za maisha ambapo hekima ya Mungu ni muhimu?

Je, hekima ya Mungu kuhusu “namna nyingi” inahusisha pamoja na matatizo ya familia, umaskini, ukosefu wa kazi, uhaba wa nyumba za kuishi, Elimu duni, uhalifu wa vijana,

---

[2] Kielelezo kingine: Kuna kampuni inayoitwa Carbonite ambayo huhifadhi taarifa zote za kompyuta za watu binafsi. Wanaweza kuhifadhi kila kitu kilichoko kwenye kompyuta yako endapo itatokea lolote la uharibifu katika kompyuta hiyo. Jaribu kufikiria aina ya chombo cha kuhifadhia wanachotakiwa kuwa nacho kuhifadhi maudhui yaliyomo katika maelfu ya compyuta hizo.

kuwatupa watoto, matatizo ya kiafya, na matatizo mengine ya kibinadamu? Kwa hakika jibu ni ndiyo, kwamba inahusisha. Je, dunia itawezaje kuiona hekima ya Mungu? Wanapaswa waione ikidhihirishwa na kanisa, kama nalo kanisa linavyodhihirisha jinsi mambo yanayotatuliwa na Mungu jamii ya imani inavyoyaishi.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Waefeso 3:20-21 kwa ajili ya kikundi.

Kusudi la kila kitu Mungu alichokifanya ni ili kimtukuze Mungu. Kwenye kanisa, ndiko mahali ambapo Mungu anatukuzwa hasa, kwa sababu:

- Ndiko mahali ambapo upendo na ukombozi unadhihirishwa.
- Ndiko mahali ambapo viumbe walioumbwa kwa mfano wake kwa hiari yao wenyewe wanamwabudu na kumtii Mungu.
- Ndiko mahali ambapo familia ya watu wenye imani hudhihirisha maisha ambayo yamebarikiwa na Mungu.
- Ndiko mahali ambapo watu waliokombolewa wanashiriki kwenye ukombozi wa watu wengine kwa njia ya uinjilisti.

Mungu atatukuzwa ulimwenguni kote na kwenye umilele kupitia kile ambacho kanisa linafanya kwa sasa. Kazi ambayo kanisa lako la mtaa linafanya itasimama kama mnara wa milele kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

## Utoshelevu wa Kanisa la mahali

Biblia inazungumzia kuhusu kanisa moja, lakini pia inazungumzia kuhusu makanisa ya mahali. Kwa mfano, Mtume Yohana aliandikia makanisa saba ya Asia (Ufunuo 1:4). Paulo alitaja kuhusu "makanisa ya Mungu" (1 Wakorintho 11:16).

Kusanyiko la mahali ni sehemu ya kanisa lililo moja, lakini bado linaitwa ni kanisa. Takribani nyaraka nyingi katika kitabu cha Agano Jipya zimeelekezwa kwa makanisa yaliyokuweko kwenye maeneo maalumu.

► Je, ni kipi kinaweza kuitwa hekalu la Mungu, kanisa la ulimwengu wote au kanisa la mahali?

Katika Waefeso 2:20-21, Paulo alisema kwamba kanisa moja, kwenye msingi wake wa asili, ni hekalu la Mungu. Katika aya ya 22, alisema kwamba waumini wa Efeso walikuwa maskani ya Mungu. Kwenye mstari mwingine aliwaambia waumini wa Korintho kwamba walikuwa ni hekalu la Mungu (1 Wakorintho 3:16). Kwa hiyo, tunaona kwamba kanisa la ulimwengu ni hekalu la Mungu; na hata kanisa la mahali pia ni hekalu la Mungu.

> "Mambo yote muhimu kwa ajili ya kanisa ni kiini tete kilichoko katika maelezo ya haya mambo manne yaliyoko kwa ajili ya kanisa [Matendo 2:42]: fundisho la mitume, ushirika, kuumega mkate, na kusali."
>
> - Thomas Oden,
> *Life in the Spirit*

► Je, ni kipi kinaweza kuitwa mwili wa Kristo, kanisa la ulimwengu wote au kanisa la mahali?

Paulo alizungumzia kanisa moja kama mwili wa Kristo (Waefeso 1:23). Hata hivyo, akiandika kwa kanisa la Korintho, Paulo alisema, "Ninyi mmekuwa mwili wa Kristo" (1 Wakorintho 12:27). Hakusema kwamba waumini wa Korintho ni sehemu tu ya mwili wa Kristo. Walikuwa ni mwili wa Kristo kwa ajili ya eneo lile.

Mungu anakusudia kila kusanyiko litende kazi kama kanisa lililokamilika, ikiwa ni pamoja na chochote wanachohitaji ili kuweza kufanyika ni mwili wa Kristo katika eneo husika.

Paulo alilinganisha washirika wa kanisa la mtaa na viungo vya mwili wa Kristo, kama macho, miguu na mikono, Bila shaka, viungo vya mwili vinapaswa viwe pamoja kwenye eneo moja ili viweze kufanya kazi. Hakuwa anasema kwamba vilikuwa viungo vya mwili na kwamba viungo vingine vya mwili vilikuwa vimetawanyika katika dunia yote. Vilikuwa ni mwili kamili uliokuwa umekamilika katika eneo husika.

Paulo alisema kwa Wakorintho kwamba baadhi ya mambo yalipaswa yafanyike "wakati kanisa lote linapokuwa pamoja katika eneo husika." Bila shaka hakuwa anazungumzia kanisa la ulimwengu wote, bali kanisa la mahali. Kusanyiko la mahali pamoja lina mamlaka maalumu linapokuwa linafanya kazi zake kama kanisa.

Mungu hutoa karama za Roho Mtakatifu zinazohitajika kwa ajili ya kanisa la mahali. Washirika huwajibika kwa pamoja wakiwa na karama za kukidhi vigezo ya kusanyiko la mahali pale.

Kwa kuwa kusanyiko la mahali pamoja ni mwili wa Kristo, hekalu la Mungu, na kanisa, inatosha kuwa ni kanisa mahali lilipo.

Utoshelevu wa kanisa la mahali inamaanisha kwamba kanisa la mahali lina karama na vianzo vya kufanyia kazi vinavyohitajika kwa ajili ya huduma katika eneo lake husika. Kanisa la mahali linaweza likafanya kazi kama kanisa kamili hata kama halina msaada kutoka mahali pengine. Viongozi wa kanisa la mahali wanasaidia washirika kuendeleza maono na malengo kwa ajili ya huduma. Kusanyiko la mahali pamoja huwajibika kwa pamoja katika kutoa ufadhili wa kifedha kwa ajili ya kusaidia huduma na kuwatunza washirika wa hilo kusanyiko la mahali pamoja.

## Umuhimu wa Kanisa

Ni vigumu sana kuwakuza watu wapya waliookoka kama hawataletwa kwenye maisha ya kanisa. Mtu aliyeokoka hawezi akafanyiwa uanafunzi ulio mzuri kama hataweza kushiriki kwenye kusanyiko la mahali pamoja. Mtu hawezi akafundishwa kwa ajili ya huduma bila ya kupata uzoefu wa kanisa.

Injili haina aina inayoweza kuonekana kwenye jamii hadi pawepo na kanisa. Aina hiyo ya muonekano haihusiani na jengo la kanisa, bali utendaji wa familia ya watu wenye imani unaodhihirisha maisha yenye kuonyesha ushirika na Mungu. Hadi hapo kanisa litakapokuwa

lipo eneo husika, dunia haiwezi ikaona maana ya kuwa Mkristo. Jamii haiwezi ikafikiriwa kwamba imefikiwa kikamilifu na uinjilisti hadi kanisa litakapokuwa katika eneo hilo husika.

## Taarifa Saba kwa Muhtasari

1. Mtu aliyeokoka hapaswi kuondolewa katika kanisa kwa sababu za ukabila, daraja lake katika jamii au kwa ajili ya dhambi zake alizozitenda wakati wa nyuma.
2. Majukumu ya kanisa yanaweza kukamilishwa tu kwa kazi ya Roho Mtakatifu kupitia kwa kanisa.
3. Umoja wa kanisa una msingi wake katika mafundisho ya imani ya kibiblia, uzoefu wa neema, na maisha ya Roho Mtakatifu.
4. Hekima ya Mungu hudhihirishwa katika ulimwengu kwa yale ambayo Mungu anayafanya kupitia kwa kanisa.
5. Utoshelevu wa kanisa la mahali inamaanisha kwamba kanisa la mahali lina karama na vianzo vya kufanyia kazi vinavyohitajika kwa ajili ya huduma katika eneo lake husika.
6. Kanisa ni muhimu kwa ajili ya kuwalea watu waliookoka, kuwafanyia uanafunzi waumini, na kutoa mafunzo kwa wahudumu.
7. Jamii haiwezi ikafikiriwa kwamba imefikiwa kikamilifu na uinjilisti hadi kanisa litakapokuwa katika eneo hilo husika.

## Kazi za kufanya Somo la 3

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 3. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.
3. Kazi ya Kuandika: Soma Waefeso 5:25-32. Andika aya kadhaa zinazohusiana na uhusiano kati ya Kristo na kanisa.

# Somo la 4
# Mashirika ya Kanisa

## Elekezo kwa kiongozi wa darasa

*Vifaa vinahitajika katika maandalizi ya somo hili. Somo hili linajadili kuhusu uhusiano kati ya makanisa na shirika lao. Kama wanafunzi wanatoka katika kanisa ambalo liko ndani ya shirika, kiongozi wa darasa atapaswa alete nakala ya mambo yanayohitajika katika shirika huo kwa ajili ya kufanya marejeo au tafakuri darasani.*

## Ufafanuzi kuhusu mashirika ya Kanisa.

► Je, jina la shirika la kanisa au dhehebu lako ambalo uko linaitwaje?

Wakati Mkristo anapokutana na Wakristo kutoka katika makusanyiko mbalimbali ya makanisa ya mahali  maswali hujitokeza. Anauliza ni kwa nini yale anayoyaamini na matendo yake yanatofautiana na wengine? Anagundua kwamba kuna tofauti za mafundisho ya imani kati ya aina mbalimbali za makanisa. Kuna tofauti kubwa sana za aina za kuabudu na au ibada.

Mshirika wa kanisa anaweza akaangalia utambulisho wa kidini ambao ni mkubwa kuliko kanisa lake la mahali. Anapenda kuona kwamba kanisa lake ni sehemu ya kundi la makanisa ambayo yanaamini katika mafundisho ya imani inayofanana, lenye kushirikiana na kuwa na ushirika unaofanana wa kuabudu pamoja. Hataki kujisikia kwamba kusanyiko lake la mahali pamoja ndilo peke yake duniani ambalo lina aina yake maalumu ya imani na matendo.

► Mwanafunzi mmoja au wawili wanaweza wakaelezea jinsi wanavyofaidika na kukutana kwao na makanisa mengine yanayofanana na kanisa lao.

Katika somo la Kwanza, tulijifunza kuhusu taarifa zifuatazo:

> Kwa ajili ya kuwa na uthabiti wa mafundisho ya imani, Kanisa la mtaa linapaswa lizingatie mambo matatu:
>
> 1. Kuwa na imani kwamba Biblia ndiyo mamlaka iliyo kamili.
> 2. Mafundisho ya imani yaliyokuwa muhimu katika historia ya Ukristo.
> 3. Kuwa na ushirika na jumuiya ya makanisa yaliyo na teolojia nzuri inayokubalika.

Katika somo hili tutazungumzia kuhusu kipengele cha tatu kilichoko katika orodha hii.

**Tafsiri ya shirika la Kanisa**

Shirika la kanisa ni kundi la makanisa yaliyojiunga pamoja na kuwa na uongozi mkuu mmoja, wanashirikishana baadhi ya mambo ya imani, wanajitoa kwa pamoja kukamilisha baadhi ya malengo, na wanakuwa na aina fulani ya kuabudu pamoja.

## Aina za Shirika Dhaifu na Zenye Nguvu

Shirika linaweza likaitwa "dhaifu" au "lenye nguvu" hutegemeana na nguvu ya mambo yanayoweka ushirika pamoja.

Katika shirika dhaifu, uongozi mkuu unakuwa na mamlaka kidogo sana juu ya kanisa la mahali; orodha ya imani za pamoja inaweza ikawa ni fupi sana na ya msingi; malengo ya pamoja yanaweza yasihitaji ushiriki mkubwa kutoka kwa makusanyiko ya mahali pamoja ya mitaa; na wawakilishi kutoka makanisa hukutana mara kwa mara tu. Katika shirika hilo, mali za kila kanisa inamilikiwa na kanisa la mahali. Na kanisa la mahali linaweza kuchagua kujitoa kwenye shirika hilo wakati wowote. Makanisa yaliyojiunga yanaweza kujitoa kwenye shirika hilo kama yakijisikia kwamba hayana hitaji la kuendelea kuwa katika shirika hilo.

Washiriki wa shirika dhaifu kwa kawaida husisitiza uhuru wa kujitawala wa kanisa la mahali (autonomy). Huwa hawataki shirika kutawala kanisa la mahali, kwa hiyo, kwa uangalifu sana wanapunguza mamlaka ya shirika. Kwa hiyo, kuita shirika "dhaifu" haina maana ya kusema kwamba unashindwa kwenye malengo yake. Washirika wa shirika dhaifu wanataka uongozi mkuu wa shirika uwe mdhaifu. Mamlaka yanagawanywa na kushikiliwa na makanisa ya mahali.

► Je, unafikiria ni nini kizuri kuhusiana na shirika "dhaifu"? Ni mambo gani ambayo siyo mazuri kuhusiana nao?

Katika "shirika lenye nguvu" uongozi mkuu wa shirika hilo wanakuwa na mamlaka kamili juu ya viongozi wa makanisa ya mahali; orodha ya imani za pamoja zinahusisha mambo mengi; makanisa ya mahali yanategemewa kutoa fedha kwa ajili ya malengo ya pamoja; na makanisa ya mahali yanakutana mara kwa mara. Mali za kanisa zinaweza kumilikiwa na shirika. Kama ndivyo, makanisa binafsi hayawezi kuchagua kuachana au kujiondoa kwenye shirika.

Washirika wa "shirika zenye nguvu" wanategemea kuona uongozi mkuu wa shirika ukishughulika na utatuzi wa baadhi ya matatizo yao mbalimbali. Wanasisitiza kujikabidhi na kutumika kabisa kwa ajili ya shirika na kanisa la mahali.

Kuna aina mbalimbali zilizopo za shirika za makanisa. shirika linaweza lisiwe na tabia zote za kulifanya kuwa shirika dhaifu au lenye nguvu, lakini linaweza kuwekwa kwenye kundi la dhaifu au lenye nguvu kutegemeana na tabia ambazo shirika hilo linazo. mashirika yenye nguvu mara nyingi yanaitwa "madhehebu."

► Je, unafikiria ni nini kizuri kuhusiana na "shirika zenye nguvu?" Ni mambo gani ambayo siyo mazuri kuhusiana nao?

► Je, ni mashirika gani ya kanisa ambayo unajua kuhusu habari zake? Je, unaweza kuziainishaje?

### Majukumu ya Dhehebu

Shirika la kanisa lenye nguvu linaitwa dhehebu. Hiyo haimaanishi kwamba shirika hilo linazo tabia zote zinazohusiana na shirika lenye nguvu, bali unaweza kuelezewa kwamba ni lenye nguvu badala ya kuwa mdhaifu.

Dhehebu zuri linakuwepo kwa ajili ya kuhudumia makanisa ya mahali. Dhehebu linasaidia makanisa katika kukamilisha mambo ya pamoja ambayo makanisa mengi ya mahali hayawezi kufanya vizuri yakiwa yenyewe.

> "Kanisa lina mamlaka ya kutoa maagizo kuhusiana na ibada za dini, sherehe, na kuwa na mamlaka juu ya utata wa kiimani, na bado siyo sheria kwa kanisa kuamua kitu chochote ambacho ni kinyume au kinachopingana na Neno la Mungu lililoandikwa…"
>
> *- Vifungu vya dini vya Kanisa la Uingereza*

1. **Linatoa ufahamu wa utambulisho ulio tofauti na aina nyingine za makanisa.** Washiriki wa kanisa la mahali wanafahamu kwamba wako tofauti na makanisa mengine katika eneo lao. Wanahamasishwa kujua kwamba wao ni sehemu ya kundi la makanisa ambayo yanashirikishana mafundisho yao ya imani.

2. **Linaanzisha mafundisho ya imani.** Kanisa la mahali halipaswi kujiona wako huru kubadilisha na kukuza mafundisho yake ya imani bila ya kusikiliza kutoka kwa mtu mwingine tena. Dhehebu linapaswa lishikilie mafundisho ya imani ya kihistoria na yaliyo ya msingi ya Ukristo, lakini pia wanapaswa wawe na mafundisho ya imani ya kina ambayo wanaamini kwamba ni ya Kimaandiko.

3. **Linaweka viwango vya sifa kwa ajili ya wachungaji na washiriki wa kanisa.** Dhehebu linapaswa liweke viwango vya sifa ili kwamba Wachungaji na washiriki wa makanisa waweze kuwa na mfano endelevu wa Ukristo. Viwango vya sifa vinapaswa viwe katika msingi uliotolewa katika 1 Timotheo 3 na Tito 1, lakini vinapaswa viwekwe wazi kutokana na kila mila au utamaduni.

4. **Linatoa mpangilio wa uongozi wa kanisa.** Dhehebu linapaswa litoe kwa kanisa la mahali mpangilio wa kuchagua watu kwenye nafasi mbalimbali ndani ya kanisa na kwa ajili ya kudumisha uwajibikaji

5. **Linatoa msingi wa mafunzo kwa wachungaji.** Makanisa mengi hayana vianzo vya mapato na maandiko ya kufundishia kwa ajili ya kuwafundisha wachungaji wa baadaye. Dhehebu linapaswa liendeleze programu za mafunzo ambazo zitakuwa rahisi kupatikana na ziwe za vitendo.

6. **Linatoa mwongozo wa uwekaji wa wachungaji kwenye makanisa.** Wachungaji wasiokuwa na makanisa na makanisa yasiyokuwa na wachungaji yanaweza kusaidiwa kwa msaada wa viongozi wa dhehebu. Viongozi wazuri wa dhehebu wataheshimu viongozi wa kanisa kwenye maeneo yote ya maamuzi yao.

7. **Linatoa mwongozo wakati kanisa la mahali linapokuwa linapitia kwenye mgogoro.** Kama kanisa la mahali litakuwa na mgawanyiko kwa ajili ya jambo fulani au halina uongozi unaoaminika, viongozi wa dhehebu wanapaswa kutoa msaada.

8. **Linaunganisha na kutoa misaada ya umisheni na juhudi za uanzishwaji wa makanisa mapya.** Kundi la makanisa wanapaswa kushirikishana maono ya kazi ya umisheni. Wanapaswa kuunganisha vianzo vyao vya mapato na nyenzo mbalimbali na kusaidia watu katika kukamilisha malengo ya umisheni.

> "Uinjilishaji kwa ajili ya ulimwengu ni wazi kwamba ndio umisheni wa Ukristo. Lakini ukamilishwaji wa huu umisheni unategemea kanisa, kwa sababu maajenti wa kutumika kwa ajili ya ukamilishaji wake kwa njia nyingine haiwezekani."
>
> \- John Miley,
> *Systematic Theology*

9. **Linafanya ushirika wa kiwango cha juu kuliko ilivyo kwa kanisa la mahali.** Washirika wanashawishiwa na kutiwa moyo wa kushirikishana muda wao na makanisa mengine yaliyo katika dhehebu hilo.

10. **Linaandaa matukio ambayo yatayaweka makanisa yake kuwa kitu kimoja.** Dhehebu linapaswa liandae makongamano na mikutano ambayo itasaidia ushirika wa makanisa na kupanga malengo pamoja.

11. **Linatuma viongozi kwenda kwenye makanisa kutoa ushauri na kuwatia moyo.** Atapaswa atoke kiongozi wa kanisa kutembelea kila kanisa la mahali angalao mara moja kwa mwaka, na ikiwezekana kufanyika mara kwa mara itakuwa vizuri zaidi.

12. **Linatoa ushauri kwa ajili ya kukuza mpango endelevu wa kifedha wa huduma ya mahali.** Shirika linapaswa liweke mkazo kuhusu uthamani na umuhimu wa kanisa la mahali na kuwaongoza jinsi ya kukua katika mambo ya kifedha.

Kama dhehebu litawajibika vizuri na kwa ukamilifu katika malengo haya, inaweza kuwa ni msaada wa thamani sana wa kukamilisha malengo ya kanisa. Itakuwa ni jambo lisilowezekana kwa makanisa mengi ya mahali kuweza kutimiza majukumu yote yaliyotajwa hapa juu peke yao. Viongozi wa madhehebu wanapaswa wakumbuke kwamba dhehebu lipo kwa ajili ya kutumikia makanisa ya mahali.

► Kwa kuwa sasa tumeshaona ni kitu gani ambacho madhehebu yanaweza yakafanya kwa ajili ya makanisa yake, tutafakari swali hili: Je, ni kwa jinsi gani kanisa linaweza kufaidika na shirika dhaifu wakati wakijiepusha na matatizo ambayo kwa kawaida huambatana pamoja nao?

► Je, ni kwa jinsi gani kanisa linaweza kufaidika na shirika lenye nguvu wakati wakijiepusha na matatizo ambayo kwa kawaida huambatana pamoja nao?

### Kuwajibika kwa Kanisa la Mtaa kwenye Dhehebu

Orodha iliyoko hapa haiwezi ikawa ni ya kufanana kwa kila dhehebu, lakini ni maelezo ya ujumla ya kile ambacho dhehebu kama kawaida huhitaji kwa ajili ya makanisa yake.

Kanisa la mahali linajitoa kabisa kuwajibika katika mambo yafuatayo:

1. Kukubaliana na taarifa ya fundisho la imani la dhehebu, kufundisha mafundisho ya imani, na kutoruhusu mafundisho ya imani yaliyo kinyume kufundishwa kwenye kanisa.
2. Kufundisha na kuwataka washirika kuendelea kuishi katika maisha endelevu ya Mkristo.
3. Kushiriki kwenye makongamano na matukio mengine, na kusaidia katika gharama kwa jinsi itakavyowezekana.
4. Kutoa taarifa ya mwaka iliyo sahihi inayohusiana na mahudhurio, watu walipoamua kuokoka, watenda kazi, na mapato.
5. Kudumisha umoja wa mikusanyiko ya makanisa ya mahali pamoja ya ya dhehebu na viongozi wake na kushughulikia migogoro kwa kuzingatia njia za kibiblia.
6. Kutojishirikisha na shirika lingine lolote ambalo litahitaji kuwa na uwajibikaji unaofanana.

*Kama wanafunzi wanatoka katika kanisa ambalo limejumishwa kwenye mahali wa makanisa, chukua dakika chache za kuangalia mambo yanayohitajika kwa ajili ya muungano huo.*

► Je, shirika la kanisa lako lilikuwa limeanzishwa na shirika la kimisheni la kimataifa? Kama ndivyo, elezea uhusiano uliopo kati ya makanisa na hilo shirika la kimisheni.

### Uhusiano kati ya Shirika la Kimisheni na Muungano wa Makanisa yake.

Wakati mwingine makanisa huwa kwenye mahusiano na shirika la umisheni la kimataifa. Shirika linaweza likaanzisha makanisa, au makanisa yaliyopo yakaamua kujiungamanisha na shirika hilo. Makanisa yaliyounganika na shirika la umisheni hutengeneza shirika wa makanisa.

Mwanzoni, wamishonari wa kigeni wangeweza kuishi nchini na kuwa viongozi wa shirika. Baada ya muda, uongozi unakua kutoka kwa wachungaji wenyeji. Umisheni unapaswa uwe na lengo la kutengeneza wachungaji ili wamisionari wa kigeni wasiendelee kuongoza shirika la makanisa yao moja kwa moja.

Wakati viongozi wa kitaifa wa shirika yanapoendelezwa, kunakuwepo na ngazi tatu kwenye shirika: viongozi wa umisheni, viongozi wa shirika wa makanisa hayo, na wachungaji wa makanisa ya mahali. Viongozi wa shirika hufanya kazi moja kwa moja na wachungaji wa makanisa ya mahali. Mara nyingi viongozi wa umisheni hufanya kazi na viongozi wa shirika.

Baadhi ya mashirika ya kimisheni hutoa uongozi wenye nguvu ambao hutengeneza shirika wenye nguvu wa makanisa. Mashirika mengine ya umisheni hutoa msaada kwa mashirika ya makanisa dhaifu na hawadai kuwa na madaraka yeyote juu yao.

Kama mahusiano yaliyopo kati ya haya madaraja matatu ya uongozi hayatafafanuliwa kwa uwazi kunaweza kukatokea mikanganyiko ya kutoelewana. Mara nyingine watu kutoka kwenye makanisa hayo ya mahali huwasiliana na viongozi wa umisheni kuhusiana na vigezo vyao badala ya viongozi wa kitaifa wa dhehebu kwa sababu wanafikiria kwamba shirika la kimisheni limejaa ukarimu katika vianzo vyake vya mapato. Wakati mwingine viongozi wa umisheni hufanya kazi moja kwa moja na makanisa, wakiwavuka viongozi wa dhehebu. Hali hii inaleta mchanganyiko kwa viongozi wa dhehebu kwa sababu inafanya majukumu yao kutokuwa wazi.

Kwenye sehemu iliyotangulia tuliorodhesha majukumu ya dhehebu. Kwenye dhehebu lililoanzishwa na umisheni, majukumu hukamilishwa kwa viongozi wa muungano na viongozi wa umisheni kufanya kazi kwa pamoja. Kwa kipindi cha muda, viongozi wa dhehebu watapaswa kwa polepole kuendelea kuchukua majukumu zaidi. Hali halisi ya dhehebu liliokomaa ni kwamba unaweza kufanya kazi vizuri sana hata kama hautapata msaada kutoka kwenye misheni husika.

### Taarifa Saba kwa Muhtasari

1. Shirika la makanisa/dhehebu husaidia kuwepo na uthabiti wa kanisa la mahali.
2. Shirika linaweza kuwa "dhaifu au "lenye nguvu" kutegemeana na jinsi uongozi mkuu wa shirika/dhehebu unavyokuwa ni muhimu.
3. Washirika wa dhehebu "dhaifu" kwa kawaida husisitiza uhuru wa kujitawala wa makanisa ya mahali.
4. Washirika wa dhehebu "lenye nguvu" wanasisitiza kujikabidhi na kutumika kabisa kwa ajili ya dhehebu na kanisa la mahali.
5. Kanisa haliwezi kuwepo kwenye dhehebu na wakati huo huo likawepo kwenye shirika lingine ambalo linahitaji uwajibikaji kamili wenye nguvu.
6. Dhehebu linakuwepo kwa ajili ya kusaidia makanisa kukamilisha malengo yao kupitia njia ya ushiriki.
7. Shirika la kimisheni la kimataifa linapaswa kuhamishia majukumu yake pole pole kwa viongozi wa dhehebu.

**Kazi za kufanya Somo la 4**

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 4. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.

2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.

3. Mtihani: Kwenye mwanzo wa kipindi kingine cha darasa, unahitajika kuandika kutoka katika kumbukumbu za ufahamu wako majukumu kumi ya dhehebu na angalau mambo matano ambayo kanisa linapaswa kuwajibika kabisa kwa dhehebu lake.

# Somo la 5
# Uanachama wa Kanisa

## Utangulizi

► Je, mtu anaweza akawa Mkristo na akaishi maisha ya Ukristo bila ya kuwa na kanisa?

> “Wale watu wa mwanzo walioamini walilipenda kanisa kwa sababu walimpenda Yesu.”
> - Larry Smith, *I Believe: Fundamentals of the Christian Faith*

Kuna sababu nyingi ambazo watu wanaweza wakawa nazo kwa ajili ya kuja kanisani. Mtu anaweza kuja kanisani kwa ajili ya kujifunza, kuuhisi uwepo wa Mungu, kupata kibali cha kukubalika na urafiki, kutiwa moyo, kubadilishwa, kumwabudu Mungu pamoja na washirika wengine, kudhihirisha kujikabidhi kabisa kwa Mungu na watu wake, kusaidia katika huduma za kanisa, na kutaka kuona kwamba ni kitu gani Mungu atatenda.

Kama mtu atakuwa haingii kwenye kanisa, mambo yaliyoorodheshwa hapa juu hayana umuhimu kwake. Atakuwa ni mtu wa aina gani asiyejali mambo hayo? Kuwepo katika kanisa siyo uthibitisho kwamba mtu ni Mkristo, lakini kama mtu hahudhurii katika kanisa, inawezekana akawa siyo Mkristo

► Je, kwa nini uanachama wa kanisa ni jambo la kujali sana? Je, haitoshi tu mtu kwenda kanisani na akafanyika kuwa Mkristo?

## Uanachama wa Kanisa ni Uwajibikaji kwa ajili ya Mpango wa Mungu

Kwenye somo lililopita, tuliona kwamba huduma ya Paulo ilikuwa ni mahsusi ya kuelezea kuhusu kanisa. Paulo aliweka msisitizo wa kanisa kwa sababu ni njia ya Mungu ya kutekeleza mpango wake wa wokovu kwa dunia nzima.

Mtume Paulo alikuwa ameitwa:

> na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu… ili sasa… kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane… (Waefeso 3:9-10).

“Siri” ni mpango wa Mungu wa kuelezea ukamilikaji wake wote na kuifunua hekima yake katika kanisa. Kanisa na ushirika wa watu ambao wamekubaliana na mpango wa Mungu na ambao wao wenyewe wamejikabidhi kabisa kwenye mpango wa Mungu. Kama mtu atakuwa hajaingia kwenye kanisa, mtu huyo hajajikabidhi kwenye mpango wa Mungu.

► Je, kuna sababu gani walizo nazo watu za kukataa kuwa na msimamo au kujikabidhi katika uanachama wa kanisa?

## Nyumba ya kweli ya Mungu

Mungu huishi ndani ya kila mtu aliyeamini, lakini huishi ndani ya kanisa (kundi la watu waliojikabidhi kabisa) kwa njia ya pekee. Angalia mahali ambapo aya hizi zinasema kwamba Mungu huishi:

> Katika yeye [Yesu Kristo] jengo lote linaungamanishwa vyema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho (Waefeso 2:21-22).

Mungu huishi ndani ya kanisa. Kanisa, ambalo ni kundi la waumini, ni nyumba ambayo Mungu anaishi ndani yake kwa Roho.[3] Makao ya Mungu katika kanisa ni kwa makusudi zaidi ya yale yanayoweza kutimizwa na watu binafsi. Ikiwa mtu anakataa kujitoa kwa kanisa, anakataa kuwa sehemu ya mpango huu wa Mungu.

## Familia ya Mungu

Mtu hupata utambulisho wake wa kiroho anapohukumiwa na dhambi, kisha hupata upendo, neema na kukubalika kwa Mungu. Anapotubu na kuweka imani yake kwa Kristo, anakuwa mtoto wa Mungu. Hiki ndicho kitambulisho muhimu zaidi ambacho mtu anaweza kuwa nacho.

Muumini pia ana utambulisho wa kiroho kama mshiriki wa familia ya Mungu (Waefeso 2:19). Waamini wengine ni ndugu na dada zake wa kiroho. Anahisi udugu na mkristo yeyote wa kweli ambaye anakutana naye.

Kanisa lipo kama familia ya Mungu ulimwenguni na pia kusanyiko la mahali pamoja katika mtaa ambalo linafanya kazi kama familia ya Mungu ya mtaa. Kama kaka au dada anakuwa na hitaji lake, ni familia yake ya kiroho ya mtaa inayomsaidia. Kama na ambavyo mtu aliyeamini anaweza akategemea familia yake ya kiroho iwe tayari kumpa msaada, anapaswa ajikabidhi kabisa kwenye familia hiyo na pia awe tayari kusaidia wengine. Msaada unaotoka katika familia hautaweza kuwepo kama hakungewepo na waumini ambao wamejikabidhi kabisa kwa muda wao na mali zao katika hilo.

Baadhi ya watu huomba msaada lakini hawapatikani katika kuwasaidia watu wengine. Hawaelewi ni nini maana ya kujikabidhi kabisa kwenye familia.

Watu wengine hujitazama au hujitunza wenyewe tu wakitegemea kwamba na watu wengine watafanya vivyo hivyo. Hawaelewi wajibu wao katika kukidhi vigezo ya watu wengine.

► Je, ni kwa jinsi gani unaweza kumwelezea mtu kwamba anapaswa ajikabidhi kabisa kwenye familia ya Mungu?

---

[3] Katika 1 Wakorintho 6:19, mwili wa mwamini binafsi unaitwa hekalu la Roho Mtakatifu; kwa hiyo si vibaya kufikiria watu mmoja-mmoja kuwa makao ya Mungu. Mahali pengine katika waraka huo huo, mwili wa mahali unarejelewa kwa pamoja kama hekalu la Mungu (1 Wakorintho 3:16-17).

## Kosa la Ubinafsi

Mtu anapaswa kwa binafsi yake mwenyewe awe anaamini ukweli wa Mungu na kwa binafsi yake mwenyewe aweze kumtii Mungu. Uhusiano wa mtu na Mungu huanza wakati anatubu na kuweka imani yake katika Kristo. Uhusiano binafsi wa mtu na Mungu haumtegemei mtu yeyote. Kila mtu aliyeamini anaye Roho Mtakatifu wa kumwongoza katika kulielewa Neno la Mungu.

Hata hivyo, Wakristo wengi wamegeuka kuwa watu wa kipekee kabisa katika tabia zao. Mitazamo yao ya kibinafsi inakuwa ndiyo uamuzi wao wa mwisho. Wanaamini tu tafsiri zao binafsi walizo nazo za Maandiko. Wanatafuta kusudi la kibinafsi kwa ajili ya maisha yao ambayo yataheshimu karama zao wenyewe, kuliko kutafuta ukamilifu kwa kutumia karama hizo zilizoko katika mwili wao. Maamuzi yao muhimu yameegemea kwenye maoni yao wenyewe, hisia zao wenyewe, na hayaongozwi na hekima za kanisa.

Watu wengi hawawezi kuelezea kusudi la kanisa. Wanaliona kanisa kama lenye manufaa tu ya kutoa faida kwa watu wachache. Hawajikabhi kabisa kama familia. Hawakubaliani na mamlaka yeyote ya kiroho. Ni wepesi kujitoa kwenye kanisa na kutafuta lingine kama kukatokea kuwepo na tatizo. Tatizo hili liko kila mahali, lakini watu kwenye baadhi ya tamaduni wana tabia ya kujitahidi kuishi maisha binafsi ya kiroho kwa sababu tamaduni zao zinasisitiza uhuru wa mtu binafsi (individualism).

Makanisa mengi wamekubaliana na dhana kwamba watu wako huru kiroho. Mahubiri yao hutoa maelekezo ya jinsi watu watakavyoweza kufanya maamuzi binafsi katika kupata matokeo yaliyo mazuri zaidi. Makanisa mengi yanaongozwa na timu ya watu ambao wanatengeneza programu, na makusanyiko yanakuwa ni makundi ya watazamaji tu. Aina nyingine ya kanisa ni kampuni binafsi ya mchungaji, anajaribu kutoa faida za kutosha kuweka watu na kukusanya msaada wao wa kifedha.

Maelezo ya Agano Jipya kuhusiana na kanisa ni kusanyiko la mahali pamoja la mahali ambalo hushirikishana majukumu. Haiwezekani kwa kanisa kukamilisha majukumu yake bila ya kuwepo na kusanyiko lililojikabidhi kabisa na lenye watu wanaoshirikiana. Takribani nyaraka zote za Agano Jipya hazijaelekezwa kwa watu binafsi, bali kwa makanisa, na zinapaswa zitafsiriwe na zitumike kwa njia hiyo.

## Baadhi ya Malengo ya Kanisa la mahali/Mtaa Yanayoonekana kwenye Agano Jipya

► Kwenye kila kipengele kilichoko katika orodha hii hapa chini, elezea ni kwa jinsi gani kusanyiko la pamoja la kanisa litaweza kushirikishana jukumu hili na kufanya vizuri zaidi kuliko ambavyo ingefanywa na mtu binafsi.

1. Kufanya Uinjilisti (Mathayo 28:18-20).
2. Kuabudu kama kusanyiko (1 Wakorintho 3:16).
3. Kudumisha fundisho la imani (1 Timotheo 3:15, Yuda 3).

4. Kutoa msaada wa kifedha kwa wachungaji (1 Timotheo 5:17-18).
5. Kutuma na kuwapa msaada wamisionari (Matendo 13:2-4, Warumi 15:24).
6. Kuwasaidia washirika wa kanisa walio wahitaji (1 Timotheo 5:3).
7. Kuwaweka katika nidhamu wale wanaoanguka katika dhambi (1 Wakorintho 5:9-13).
8. Kufanya ubatizo na kushirikisha Meza ya Bwana (Mathayo 28:19, 1 Wakorintho 11:23-26).
9. Kuwakamilisha kwenye uanafunzi waumini hadi wafikie kwenye utimilifu (Waefeso 4:12-13).

Mambo mengi yaliyoko hapa hayawezi kufanywa na mtu mmoja anayejinasibu kufanya akiwa mwenyewe. Mambo haya yanategemea ushirikiano wa kikundi cha waumini na muundo wa uongozi.

Mungu humwita kila mtu aliyeamini kuingia kwenye kanisa la mtaa na kulisaidia kanisa hilo kutimiza malengo yake hapa duniani. Endapo mshirika atakuwa hatumiki ndani ya kanisa, atakuwa hatimizi kusudi la Mungu kama mshirika wa mwili wa Kristo

> "Ni wajibu wa kila Mkristo siyo tu kukiri kwa uwazi imani yake iliyo katika Kristo, bali kuingia kwenye ushirika wa kundi la watu walioamini katika jumuiya yake, na kubeba yeye mwenyewe majukumu ya kuwa mwanachama wa kanisa."
>
> - Wiley & Culbertson, *Introduction to Christian Theology*

Mungu anao mpango kwa ajili ya kundi la mtaa la watu walioamini. Anatoa kile kinachohitajika na anahitaji msimamo kutoka kwa mshirika.

### Mfano wa Mwili

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 12:12-27 kwa ajili ya kikundi.

Paulo alisema kwamba washirika wa kanisa wanapaswa wafanye kazi pamoja kama viungo vya mwili wa kawaida. Kiungo hakipaswi kijaribu kujiondoa chenyewe kutoka katika viungo vingine. Kiungo kimoja hakiwezi kukamilisha mambo bila ya kutegemea viungo vingine.

Mkristo anapaswa atambue kwamba vipawa vyake vinapata thamani yake kwenye maisha ya kanisa. Kama vile ambavyo jicho au sikio lisivyokuwa na manufaa hadi pale linapokuwa linafanya kazi kwa ajili ya mwili, vile vile kuna uwezekano wa mtu kutokuona kusudi muhimu kwenye mapenzi ya Mungu hadi pale atakapowajibika kama mshirika wa kanisa mwenye msimamo kabisa.

## Mchakato wa Uanachama

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Matendo 2:46-47 kwa ajili ya kikundi.

“Bwana akalizidisha kanisa kila siku.” Kujiunga na kanisa halikuwa jambo lililokuwa gumu kwenye siku za mwanzo za kanisa. Ushuhuda kuhusiana na kuokoka na imani ndio uliokuwa msingi wa uanachama. Hata bila ya utaratibu wa kawaida wa mchakato wa uanachama au orodha ya masharti ya uanachama, ilikuwa rahisi kumwona ni nani aliyekuwepo ndani ya kanisa.

Mara nyingi kanisa huanza bila ya kuwepo kwa utaratibu wa uanachama. Mwanzoni kanisa linakuwa na timu ya uinjilisti. Kisha, watu wa mtaa ambao wamekubaliana na huduma hujiunga na kuwa wahusika. Kikundi hukutana mara kwa mara kwa ajili ya majadiliano kuhusiana na mambo ya vitendo ya kufanya, mambo ya kiroho, maono kwa ajili ya wakati ujao, na vipengele vya kushirikishana maisha pamoja. Hakuna orodha ya uanachama, lakini kila mtu anatambua kwamba ni watu gani wenye msimamo au waliojikabidhi kabisa.

Kwa kadri kanisa linavyoendelea kukua, maswali huanza kujitokeza. Watu wengi hulitembelea kanisa na kushiriki katika shughuli zake; lakini ni watu gani halisi walio wa kanisa? Kanisa linapaswa liwe ni shahidi, lakini litakuwaje shahidi kama jamii iliyopo haijui ni nani mshirika halisi wa kanisa? Tunafundisha kusanyiko kujikabidhi kabisa katika kuwasaidia watu wengine walioko kwenye kundi hilo, lakini watajuaje ni nani walioko? Kama mtu atakataa kupokea marekebisho ya maisha yake na akaendelea kuishi maisha ya dhambi hadharani, anawezaje kutofautishwa kutoka kwenye kundi la waumini waliojikabidhi kuwa na msimamo kabisa wa kuishi maisha ya uaminifu?

Makanisa mengi ya wakati wa sasa yana vigezo vingi vinavyohusiana na uanachama wa mtu. Wana tamko la mafundisho ya imani, masharti yanayohusiana na maisha ya mshirika, na kipindi cha katika matazamio. Siyo rahisi kwa mtu mpya aliyeokoka kwa haraka kuwa mshirika wa makanisa hayo.

Mtu mpya aliyeokoka anastahili akubalike mara moja kwenye ushirika wa kanisa. Anahitajika awe ni sehemu ya kundi la waumini ambao wamemaanisha na kujikabidhi kabisa kwa ajili ya wengine. Huwa anapoteza marafiki ambao siyo Wakristo anapokuwa ameokoka, na kwa ajili hiyo anahitaji ushirika wa Kikristo.

Mtu mpya aliyeokoka pia anahitaji afundishwe uanafunzi unaotokana na ushirika wa karibu na Wakristo wengine. Atabadilishwa kutokana na thamani ya watu waliopo ambao hushirikishana maisha yao pamoja naye.

Inakuwaje kama mtu aliyeokoka hawezi kujiunga na kanisa kwa sababu ya masharti mazito ya uanachama ambayo hawezi akayaelewa? Kama atakuwa hashirikishwi kwenye uanachama, anajihisi kwamba hakubaliki ndani ya kanisa. Anahitajika apate aina fulani ya uanachama haraka kadri itakavyowezekana. Kanisa la kwanza liliweza kuwahusisha waongofu kama washiriki haraka.

### Uanachama wa Ujumla wa Kanisa/Uanachama wa Ushirika

Kanisa litakuwa linafanya vyema katika kuwafanya watu wapya waliookoka kuwa washirika haraka, hivyo uanachama wa kanisa utawajumuisha pia Wakristo ambao hawajakomaa. Watu wapya wanaookoka hawana ufahamu wote kuhusiana na mafundisho ya imani yaliyo muhimu kwa kanisa. Wanakuwa bado hawajakuza mfumo wa maisha ya Mkristo aliyekomaa. Kwa hiyo, hawapaswi kuwajibika katika kufanya maamuzi kwa ajili ya kanisa. Kwa kuwa uanachama wa kanisa unahusisha pia watu ambao siyo Wakristo waliokomaa, uanachama wa ujumla wa kanisa haupaswi kufanya maamuzi yanayohusiana na mwelekeo wa kanisa.

Ndani ya uanachama wa jumla kunapaswa kuwepo na washirika ambao wanakuwa ni sehemu ya baraza la uongozi. Baraza la uongozi la kanisa linapaswa liundwe na Wakristo waliokomaa ambao wanaelewa mafundisho ya imani na mfumo wa maisha unaofundishwa na kanisa. Hili ni kundi ambalo linafanya maamuzi kwa ajili ya kanisa. Uanachama katika kundi hili unahitajika uwe wa vigezo vya sifa za juu kuliko ulivyo uanachama wa jumla wa kanisa. Kutoka katika kundi hili, washirika wanaweza kutumika kama waalimu na viongozi ndani ya kanisa. Baraza la uongozi linahakikisha kwamba kanisa linabaki kuwa la kweli kwenye mafundisho yake ya imani pamoja na malengo yake.

Uanachama wa jumla unawakubali watu wapya waliookoka walio na msimamo wa kujikabidhi kabisa kwa kanisa. Vigezo vilivyopo kwa ajili ya uanachama wa jumla ndiyo mambo ya msingi ya Ukristo na msimamo wa kujikabidhi kabisa kwenye hilo kanisa. Mtu aliyeokoka anaweza kukubaliwa haraka kuingia kwenye uanachama wa jumla endapo ataonekana kwamba kwa ukweli ameokoka. Mtu aliyeokoka hupokelewa kwenye ushirika na kuwajibika ndani ya kanisa kwa haraka kama anavyohitaji. Baadhi ya makanisa yanauita huu uanachama wa jumla kwamba ni "Ushirika."

► Je, ni kwa nini mtu mpya aliyeokoka anahitajika kuhusika kwa haraka ndani ya kanisa?

► Katika mfumo wa uanachama ulioelezewa katika sehemu hii, je, ushirika ni nini, na ni aina gani ya mtu ambaye ni mwanachama wake?

► Katika mfumo wa uanachama ulioelezewa katika sehemu hii, je, Baraza la Uongozi ni nini, na ni aina gani ya mtu ambaye ni mwanachama wake?

*Ushirika na Baraza la Uongozi* ni mfumo mmoja wa uanachama. Katika sehemu zinazofuatia hapa chini, aina nyingine mbili za mifumo zimejadiliwa.

### Uanachama wa Mkristo Aliyekomaa

Dhana moja ya uanachama inahitaji wanachama wawe wenye weledi au ufahamu mkubwa katika mafundisho ya imani na wawe wamekomaa kikamilifu kiasi cha kwamba wanaweza kukubalika kuwa wapiga kura kwenye maamuzi ya kanisa. Kundi hili huchagua watu watakaochukua nafasi za utumishi, ikiwa ni pamoja na mchungaji. Aidha wanapiga kura

kwenye maamuzi ya utendaji au kuchagua kikundi cha wawakilishi ambacho kitakuwa kikifanya maamuzi hayo.

Kwa kuwa uanachama unathibiti serikali ya kanisa, muumini mpya hawezi kwa haraka akakaribishwa kuingia kwenye uanachama. Kwa kadiri ambavyo kanisa linakuwa kwenye hadhari na umakini, ni kwa jinsi hiyo hiyo kutakuwepo na orodha ndefu ya vigezo vya kuwa uanachama na muda mrefu kati ya mtu kuokoka na uanachama. Kanisa linaweka vigezo vya uanachama ambavyo ni pamoja na mambo yote ambayo Mkristo aliyekomaa anatakiwa awe, sio tu maelezo ya msingi ya mtu aliyeokoka. Mtu aliyeokoka anaweza akawa mshiriki wa maisha ya kanisa kwa miaka mingi bila kuwa na sifa za kufanyika kuwa mwanachama. Baadhi ya watu waliookoka wanaweza kuamua kuondoka kwa sababu hawawezi kuwa wanachama.

**Uanachama wa Kusanyiko la Waumini**

Kwenye baadhi ya makanisa, wale ambao kwa kawaida wanahudhuria ibada wanahesabika kuwa ni wanachama. Mamlaka nyingine zinaweza zikawa ndizo zenye maamuzi ya shughuli za kanisa, lakini yeyote anayehudhuria kwenye kanisa ni mwanachama. Hata hivyo, hata lile kanisa ambalo linadai kwamba halina orodha ya wanachama, kuna mfumo ambao haujaandikwa rasmi ambao unaangalia ni nani aliyeko pamoja nao na ni nani ambaye hayuko pamoja nao.

Kwenye kanisa ambalo lina uanachama wa kusanyiko la waumini, uimara wa kanisa unaweza kuwa kwenye mikono ya mchungaji au viongozi wanaotoka kwenye familia zenye ushawishi au umaarufu.

Endapo kanisa changa lina uanachama wa kusanyiko la waumini kama ndiyo mamlaka ya mwisho, kwa namna yeyote ile haliwezi likatabiri litakavyokuwa kwa miaka michache itakayokuja mbele.

Endapo kanisa la zamani lenye uanachama wa kusanyiko la waumini lina uimara au uthabiti, kuna uwezekano kwamba liliimarishwa na aidha kundi la familia au mchungaji mwenye nguvu aliyetumikia hapo kwa muda mrefu. Itakuwa ni vigumu kwao kuweza kuelezea masharti ambayo mambo yanafanyika, lakini wanawaamini wale walioko kwenye uthibiti au mamlaka. Kanuni zilizoandikwa zinaweza zisiwepo au zinaweza zikapuuzwa. Wakati ambapo mchungaji au viongozi wengine wanabadilishwa, kanisa linaweza kupitia kwenye mabadiliko makubwa.

► Je, kuna faida na hasira gani unazoziona kwenye hii mifumo miwili ya uanachama iliyoelezewa hapo juu?

► Tazama mifano miwili ifuatayo, moja kutoka katika kanisa lililopo Marekani, na mwingine kutoka katika kanisa lililopo Ufilipino. Jadili ni kwa jinsi gani haya maelezo ya aina mbili yanavyolinganishwa na uanachama wa kanisa kwenye makanisa unayoyafahamu.

**Mfano wa Kwanza**

**Ushirika wa Kanisa la Ushindi *(The Victory Chapel Fellowship)***

*Jamii (Watu wote)* hualikwa kushiriki takribani kwenye shughuli zote za Kanisa la Ushindi ikiwa ni pamoja na ibada za kuabudu, mikusanyiko ya jumuiya za nyumbani, kushirikishana mahitaji, maombi, vyakula vinavyoandaliwa na usharika au kusanyiko, na mafundisho ya Biblia. Hata hivyo, Agano Jipya huonyesha kwamba kikundi cha watu wanaofanya kanisa la mtaa hakina budi kiwe kinachotambulika. Lazima kitambulike wazi kwa jamii kwamba ni watu gani wanaoshiriki katika kanisa hilo. Bila ya kikundi hicho kuwa kinatambulika, litakuwa ni jambo lisilowezekana kwamba kanisa lina ushuhuda mbele ya dunia, au kuweza kushirikisha ushirika wa kweli wa Kikristo ulio katika msingi wa umoja wa Ukristo usiokuwa na mipaka ya urafiki, kufanya nidhamu ya kanisa ya kibiblia, na kubeba kwa pamoja majukumu ya huduma kwa ajili ya kanisa. Kwa hiyo, majukumu kwa ajili ya huduma za Kanisa la Ushindi yanategemea kila kitu kutoka kikundi cha kusanyiko au usharika kinachoitwa "Ushirika."

**Vigezo vinavyotekelezwa na wale walioko kwenye Ushirika**

Tunatambua kwamba kuna vigezo vingine maalumu ambavyo ni udhihirisho wa kukua kiroho, lakini vigezo vinavyofuata vinatoa mambo ya msingi ambayo yanaonekana kuwa ni muhimu kwa ajili ya umoja na ushirika wa kweli wa kuabudu wa Kikristo.

**(1) Maisha ya Kiroho**

Dhihirisha ushahidi wa kuokoka, matamanio ya kiroho, na msimamo kabisa wa kuenenda kwa uhusiano wa utiifu pamoja na Mungu.

**(2) Hamasa ya Kibiblia**

Epukana na uasherati, matumizi ya madawa ya kulevya, kuvuta sigara, na vinywaji vyenye kulevya.

**(3) Msimamo wa Kujikabidhi au kujitoa kabisa kwa Kanisa.**

Hudhuria ibada zote za kanisa kwa uaminifu labda uwe umezuiliwa na hali ya kiafya, kuwepo kwenye huduma nyingine, au uwepo kazini ambao hauwezi kuzuilika kwenye siku za Jumapili. Toa zaka katika utoaji wa kanisa.

**(4) Umoja wa fundisho la Imani**

Umoja na uelewa wa kanuni ya imani ya Kanisa la Ushindi ni muhimu. Mchungaji huwajibika kushirikishana majadiliano ya Pamoja na muda wa maelekezo kwa kila mtarajiwa.

**(5) Maadili ya Vitendo**

Dumisha uaminifu katika aina zote za mahusiano na uaminifu katika yote uliyoamua kuwa na msimamo nayo. Dumisha tabia endelevu ya upendo na utiifu kwa wale wengine walioko kwenye ushirika.

**Sera Mbalimbali**

Tunatambua kwamba baadhi ya wanachama wapya hawataendelea kuwepo, lakini tunachagua kutokuwa na kipindi cha majaribio, kwa sababu waumini wapya wanahitaji kujihusisha mara moja katika shughuli za kanisa.

Baraza la uongozi litafanya tathmini ya jina lililopendekezwa kwa ajili ya Ushirika baada ya mtarajiwa kuwa amefanyiwa usahili na mchungaji.

Mtu aliyeokoka ambaye amekubalika kuwa kwenye Ushirika atapangwa kwa ajili ya kubatizwa labda iwe kwamba alishawahi kubatizwa *(ubatizo wa maji mengi)* hapo awali baada ya kuokoka.

Endapo muumini aliyeko kwenye Ushirika ataonekana kuwa amekiuka mahitaji ya vigezo vilivyowekwa, baraza la uongozi linaweza aidha kumwondoa kwenye ushirika au kutoa muda wa kuwa chini ya uangalizi na kuwajibika, na baada ya hapo suala lake litaangaliwa au litafikiriwa tena.

## Mfano wa Pili

**Kanisa la Biblia Methodisti la Ufilipino**

Baada ya kumpokea Yesu kama Mwokozi wangu na Bwana, nikaamini katika kifo chake, kumwagika kwa damu yake na kufufuka kwake ikiwa ni ukamilifu wa wokovu wangu, ninajiunga sasa na mwili wa Kristo wa ulimwengu wote. Lakini kama ambavyo mwili na viungo vingi, vivyo hivyo na mwili wa Kristo. Kupitia maombi ya kweli, ninajisikia kuongozwa na Roho Mtakatifu katika kujiunga na familia ya Kanisa la Biblia Methodisti la Ufilipino – kwenye ushirika wake, imani, na nidhamu ya kiroho kwa kadri Mungu atakavyozidi kuniwezesha. Kwa kufanya hivyo, ninajikabidhi mwenyewe kwa Mungu na kwa wanachama wengine katika kufanya yafuatayo:

**Kwanza, kulinda umoja wa kanisa langu.**

- Kwa kufanya kwa upendo dhidi ya wanachama wengine (1 Petro 1:22)
- Kwa kukataa umbeya na kusengenya (Waefeso 4:29)
- Kwa kuwatii viongozi waliochaguliwa (Waebrania 13:17)
- Kwa kuwa na huruma kwa ndugu ambao wameanguka kutoka katika neema ya Mungu (Wagalatia 6:1-2)

**Pili, kushiriki katika majukumu ya kanisa langu.**

- Kwa kuomba kwa ajili ya kukua kwake (1 Wathesalonike 1:1-2)
- Kwa kuwakaribisha watu ambao hawana kanisa waweze kushiriki (Luka14:23)
- Kwa kuwakaribisha wageni kwa ukarimu (Warumi 15:7)
- Kwa kuwatambulisha watu kwa Yesu Kristo (Matendo 8:33-35)

**Tatu, kuwa katika huduma ya kanisa langu.**

- Kwa kugundua karama za kiroho (1 Petro 4:10)
- Kwa kuwezeshwa kutumika pamoja na wachungaji (Waefeso 4:11-12)
- Kwa kukuza moyo wa utumishi katika kuwahudumia watakatifu, kwa wenye njaa, kwa walio uchi, wagonjwa, wajane na yatima, na waliofungwa – kwa kadri ya uwezo na nafasi itakayopatikana (Mathayo 25:31-46; Wafilipi 2:3-7)

**Nne, Kwa kuunga mkono ushuhuda wa kanisa langu.**

- Kwa kuhudhuria kwa uaminifu (Waebrania 10:25)
- Kwa kupokea kwa unyenyekevu Neno la Mungu kama litakavyokuwa linahubiriwa, na kutembea katika nuru yake (1 Yohana 1:9-10)
- Kwa kuishi maisha ya utakatifu (Waebrania 12:14; Wafilipi 1:27)
- Kwa kukiri makosa (James 5:16)
- Kwa kushiriki Meza ya Bwana (1 Wakorintho 11:23-26)

- Kwa kutoa matoleo mara kwa mara (Mambo ya Walawi 27:30; 1 Wakorintho 16:2; 2 Wakorintho 9:7)

Imetiwa sahihi leo ____ tarehe ya _______________

Sahihi ya Mwanachama _________________________________

Imethibitishwa na: _____________________ Mchungaji wa Kanisa la Mtaa

## Taarifa Saba kwa Muhtasari

1. Mungu huishi ndani ya kikundi cha waumini kwa njia maalumu.
2. Kanisa ni familia ya Mungu, mahali ambapo waumini huweka msimamo na kujikabidhi kabisa kwenye uhusiano wa kifamilia.
3. Uanachama wa kanisa ni njia mojawapo ya kujiweka kwenye msimamo na kujikabidhi kabisa kwenye mpango wa Mungu kwa ajili ya kanisa.
4. Kusanyiko au Usharika ni lazima uweze kushirikishana majukumu ya kanisa kwa pamoja.
5. Uwezo wa mtu binafsi ni muhimu sana unapotumika kwenye maisha ya kanisa.
6. Mtu mpya aliyeokoka anahitajika kuhusika kwa haraka ndani ya kanisa.
7. Ukomavu haupaswi kuwa kigezo cha uanachama wa kanisa.

## Kazi za kufanya Somo la 5

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 5. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.
3. Kazi ya Kuandika: Jaribu kukadiria asilimia (%) ya watu wanaohudhuria kwenye kanisa lako ambao ni wanachama wenye msimamo na wamejikabidhi kabisa. Elezea ni kwa jinsi gani mtu anafanyika kuwa ni mwanachama katika kanisa lako.

# Somo la 6
# Kushirikishana Maisha Pamoja

## Kanisa baada ya Pentekoste

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Matendo 2:42-47 kwa ajili ya darasa. Ni maelezo gani unayoyaona kuhusiana na ushirika wa kanisa baada ya Pentekoste?

Mara tu baada ya Pentekoste, kitabu cha Matendo kinaelezea kuhusu maisha ya kanisa. "Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika." Watu wengi waliuza vitu vyao ili kusaidia maisha ya jamii ya kanisa. Walikuwa wakikutana mara kwa mara katika hekalu kwa ajili ya ushirika wa kumsifu Mungu na pia wakikutana kwa ajili ya ushirika wa nyumba kwa nyumba.

Kwenye kipindi ambacho utendaji wa Roho Mtakatifu ulikuwa wa hali ya juu miongoni mwao, maisha ya jamii ya kanisa nayo yalikuwa katika kiwango cha juu sana. Kwa wale waumini wa mwanzo, kuwa sehemu ya kanisa ilimaanisha ni zaidi ya kushiriki kwenye ibada za Jumapili. Kila siku waumini walishirikishana kwa pamoja kuhusu maisha yao.

> "Kwa pamoja kwenye Maandiko na kanuni za imani ushirika wa Kikristo unawakilishwa kama namna ya neema."
> - Wiley & Culbertson, *Introduction to Christian Theology*

## Maisha katika Familia

Kwenye Agano Jipya, kanisa linaitwa ni familia (Wagalatia 6:10, Waefeso 3:15). Waumini wanaitwa ni watoto wa Mungu (Wagalatia 3:26, 1 Yohana 3:2), na kuwaita kila mmoja kaka na dada (Yakobo 2:15, 1 Wakorintho 5:11).

Tuitafakari familia kama ambavyo kama ambavyo ilikuwa ikieleweka katika maeneo mengi ya dunia hadi wakati wa sasa. Mtandao wa ndugu (au jamaa) ulitengeneza ukoo, ambao ulikuwa sehemu ya kabila. Familia iliyopanuliwa ilitoa ulinzi, ilihusika katika upatikanaji wa haki, ilihusika katika kuwa na maeneo ya ardhi, kazi, ndoa, elimu, pia ilihusika katika kuwasaidia wazee, yatima na wajane. Mambo hayo yalikuwa ni vigumu kuweza kupatikana nje ya muunganiko wa familia.

Katika hali hiyo ya utamaduni, kila mtu ndani ya familia alikuwa ndani ya dini moja inayofanana. Suala la dini halikuwa linachukuliwa kama ni chaguo la mtu binafsi. Watoto walikuwa wanalelewa katika mafundisho yaliyoendana na utamaduni wa dini ya familia.

> "Kwa maana kanisa ni familia ya Mungu, ambapo kwa kuzaliwa na kwa damu sisi ni mali—jumuiya ya urithi na upendo ambayo tunaingia kwa kuzaliwa upya, kuokolewa kwa damu ya Yesu."
> - Larry Smith, *I Believe: Fundamentals of the Christian Faith*

Watu wengi waliookoka na kuwa Wakristo walikataliwa kwenye familia zao. Walipoteza kila kitu ambacho kwa kawaida kilikuwa kinatolewa na familia. Kanisa lilifanyika kuwa ndio familia yao mpya. Hii ndiyo maana waliitana kila mmoja kwamba ni kaka na dada. Watu wa kanisa walimsaidia kila mtu na wakitegemeana kila mmoja

Kama watu wakionana kwenye siku za Jumapili tu, wanaanza kufikiria kwamba kukutana Jumapili tu ndio kanisa. Makanisa ya Agano Jipya yalikutana siku za Jumapili, lakini kanisa lilikuwa hai na likiendelea kufanya kazi kila siku.

► Je, ni kwa jinsi gani mambo yataweza kuwa tofauti kwa ajili ya kanisa ambalo linashirikishana masuala ya maisha kila siku?

Wachungaji wanapaswa wafahamu kwamba kuhudumia kusanyiko kwa muda wote wa wiki ni muhimu sana kama vile ilivyo muhimu kuongoza ibada ya kumwabudu Mungu. Aina zote za karama za kiroho na uwezo binafsi wa watu mbalimbali unahitajika, na siyo karama zitumike kwenye siku za ibada za kanisa tu. Kuna njia ambayo kila mtu anaweza akatumika. Watu katika jamii wataweza kuona inamaanisha nini hasa kuwa sehemu ya familia ya kiroho.

**Kama familia ya watu wenye imani, kanisa wanatumia rasilimali watu na kupata rasilimali za Mungu vya kukidhi mahitaji ya kila aina kwa ajili ya wale walioko kwenye ushirika, wakidhihirisha kwa ulimwengu hekima ya Mungu katika kila kipengele cha maisha na kuwakaribisha watu ambao hawajaokoka ili waokoke na kuingia kwenye familia.**

## Vipengele vya Maisha ya Pamoja

Kama watu wanashirikishana maisha pamoja, kuwa kwao kwa pamoja kutahusisha vipengele vifuatavyo:

1. **Huduma inapangika na kukamilika kwa pamoja.** Katika makanisa mengi, timu ndogo inahusika kwenye kupanga na kuwajibika kwa ajili ya kanisa. Kila mtu katika kanisa anapaswa aweze kushiriki kwenye kuwajibika kwa ajili ya kanisa, ikijumuisha waongofu wapya.

2. **Mahitaji yanatimizwa kwa pamoja.** Kama mtu atakuwa na tatizo, ataweza kuwategemea marafiki zake walioko kwenye kanisa kwa ajili ya kupewa msaada. Hiyo haimaanishi kwamba mtu atakuwa anaruhusiwa kutowajibika, lakini kama anafanya lile lililo kwenye uwezo wake kulifanya, familia ya kanisa inapaswa iwe tayari katika kusaidia.

3. **Majukumu yanakamilishwa kwa pamoja.** Uhusiano mzito unajengwa wakati waumini wanapowajibika kwa pamoja katika kumsaidia mtu mmojawapo katika ushirika. Wanaweza pia wakawajibika kwa pamoja katika kuzisadia familia zao wenyewe.

4. **Muda wa kuburudika unafanyika kwa pamoja.** Watu katika kanisa wanapaswa wapate nyakati za kufurahia kwa pamoja katika kula, kutembelea, na kufanya shughuli nyingine mbalimbali.

5. **Nyakati maalumu za maisha husherehekewa kwa pamoja.** Siyo tamaduni au mila zote zinazokuwa na matukio maalumu yanayofanana. Nyakati zingine maalumu ambazo watu husherehekea ni kama kuzaliwa, kuhitimu shule, kubatizwa, kumbukumbu za siku za kuzaliwa, kufunga ndoa, kupata watoto, maziko, na shughuli nyingine za nyakati maalumu. Watu katika dini nyingine kwa kawaida wanakuwa na siku mahsusi kwa ajili ya kusherehekea nyakati hizi. Kanisa linapaswa liwe na njia ya kushirikishana nyakati hizi maalumu za maisha kwa pamoja.

### Kutoa zaka wakati wa Agano la Kale.

Wakati wa Agano la Kale, zaka hazikuwa tu kwa ajili ya kusaidia hekalu na wale waliokuwa wakiendesha ibada. Zaka zilikuwa zinatumika pia kwa ajili ya kusaidia mahitaji ya wajane, yatima na wageni wahamiaji (Kumbukumbu la Torati 26:12). Zilikuwa pia ni kwa ajili ya mikusanyiko maalumu (Kumbukumbu la Torati 12:17-18). Matumizi ya zaka yanatuonyesha sisi kwamba vipengele vyote vya maisha kwa pamoja ni vya muhimu kwa ajili ya kanisa.

### Ushirika na Uchumi

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Yakobo 2:15-16 kwa ajili ya kikundi. Je, aya hizi zinadokeza nini kuhusiana na ushirika wa Kikristo?

Wakati mwingine watu huishi kana kwamba mahitaji ya kifedha hayana uhusiano na ushirika wa waumini. Lakini Maandiko yanatueleza kwamba kuwa sehemu ya familia ya watu wenye imani ni kumaanisha kwamba tunapaswa tuwajibikie mahitaji.

Ushirika unamaanisha ni kushirikishana kuhusu maisha, ambapo huhusisha zaidi ya uzoefu wa kiroho. Neno la Kiyunani *Koinonia,* linalotumika kwenye Agano Jipya, mara nyingi linatafsiriwa kama "ushirika" na neno hili linatumika kwa ajili ya aina yeyote ya kushirikishana. Wakati mwingine linatumika katika kushirikishana mapato ya kifedha (2 Wakorintho 9:13, 2 Wakorintho 8:4; Warumi 15:26). Jamii ya Kikristo katika Yerusalemu kwenye karne ya kwanza, hakuna mtu aliyekosa kile alichokuwa anakihitaji (Matendo 4:34-35), kwa sababu watu walishirikishana vile vitu walivyokuwa navyo.

Kulipotokea kuwepo na ubaguzi kwenye utoaji wa msaada wa kifedha wa kanisa huduma hiyo ilizuiliwa. Tatizo hilo liliporekebishwa, injili iliendelea kuongeza watu wapya waliookoka (Matendo 6:1, 7).

Mnamo mwaka wa 125 B.K. Mkristo aliyejulikana kwa jina la Aristide aliandika:

> Walitembea katika unyenyekevu wote na upendo, na hakuna uongo uliopatikana mingoni mwao, na walipendana kila mmoja na mwenzake. Hawakuwanyanyasa wajane na wala hawakuwahuzunisha yatima. Yeye aliyekuwa nacho, humgawia bila masharti yule ambaye alikuwa hanacho. Kama wakimwona mgeni, humleta

> malangoni mwao na kufurahia pamoja naye kana kwamba alikuwa ndugu yao: kwa kuwa wao wenyewe waliitana ndugu, siyo katika mwili, bali katika roho na Mungu; lakini mmojawao akitwaliwa kutoka katika ulimwengu huu (akifariki), na yeyote akienda kumwona, ndipo hutoa gharama za mazishi kwa kadri ya uwezo wake; na endapo wakisikia kwamba yeyote miongoni mwao amewekwa jela au kupewa mateso kwa ajili ya Masihi wao, wote kwa pamoja walitoa walivyokuwa navyo kwa ajili ya mahitaji yake; na ikiwezekana wao kumwokoa, wanafanya hivyo. Na kama miongoni mwao yuko mtu ambaye ni maskini na mhitaji, na hawakuwa na vitu vya kutosheleza mahitaji, walifunga kwa maombi kwa muda wa siku mbili hadi tatu ili kwamba waweze kutoa mahitaji pamoja na vyakula muhimu.

Julian mwasi, Mfalme wa Roma (361-363 B.K.) aliyelitesa kanisa, alitoa taarifa yake kuhusu Wakristo: "Wagalilaya makafiri hawawalishi maskini wao tu, bali na wetu pia."[4]

Kanisa litatimiza nusu ya majukumu yake kama litahubiri kuhusu toba tu, endapo halimkaribishi mtu huyo aliyetubu kwenye familia ya watu wa imani ambako atajifunza jinsi ya kuendeleza maisha yake mapya. Kwa mfano, kama kanisa linamwambia mwanamke kuwa hawatampa pesa kwa kuwa ni kahaba, kanisa linapaswa limweleze ni kwa jinsi gani atafute msaada kutoka katika hiyo familia ya watu wa imani.

Kwenye maeneo mengine ya dunia, tunaona makusanyiko ya kanisa ambayo yanadhihirisha aina hii ya jumuiya ya Kikristo. Ushirika huu wa jumla siyo tu kwamba unatokana na kuwajali wanachama wake kwenye mambo ya kifedha, lakini pia unatokana na uwezeshwaji mkubwa wenye nguvu unaofanywa kwa ajili ya huduma.

> Makanisa haya ya maskini (katika Bolivia) yana kitu tunachoweza kukiita utumishi kwa ajili ya kuendelea kuishi. Makanisa yenye umaarufu yaliyoanzishwa miongoni mwa watu maskini hayawezi kuwa tegemezi kutoka kwenye utamaduni, kutoka kwenye msaada wa dola, kutoka kwenye mali zilizowekwa wakfu za watu matajiri, au kutoka kwenye kundi la wahudumu waliobobea kitaalamu. Wanapaswa wawepo kwenye ushirika ambao wanachama wake huunganisha nguvu zao katika kuifanya jumuiya iweze kuwa hai, iweze kukua, iweze kueneza imani, na iweze kudumu. Utumishi unaohusiana na ujumla wa maisha unazoeleka kama ni uhamasishaji wa ujumla wa umishenari. Kitu kinachoonekana kuwa vigumu sana kukipata kutoka kwenye makanisa yenye maendeleo na yaliyo imara ni uhamasishaji wa watu wa kawaida – ushiriki wa ujumla katika kujali ustawi wa jumuiya ya Kikristo. Miongoni mwa makanisa ya watu maskini, uhamasishaji huu ni mfumo wa kawaida wa maisha ya jumuiya. Kunakuwa hakuna njia nyingine ya maisha na uendeshaji wa huduma ni kitu kinachowezekana.[5]

---

[4] Wakristo waliitwa "makafiri" au "wanaomkana Mungu" kwa sababu waliamini katika Mungu mmoja tu, na kwamba alikuwa ni Mungu asiyeonekana kwa macho, kuliko kuamini wingi wa msururu wa miungu ya sanamu inavyoonekana.

[5] Samuel Escobar, katika *The Urban Face of Mission: Ministering the Gospel in a Diverse and Changing World*. Kimfanyiwa uhariri na Manuel Ortiz na Susan S. Baker. (Phillipsburg: P & R Publishing, 2002), 105.

Tunaweza tukafikiria kwamba kanisa ni lazima liwe na fedha nyingi sana kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ajili ya wanachama wake. Lakini aina hii ya jumuiya inadhihirishwa katika makanisa ya watu maskini katika nchi ya Bolivia.

Watu wa kila jamii wanashirikishana maisha ya kifedha kupitia uchumi wa jamii. Tunanunua vitu tunavyovihitaji na tunafanya kazi ili kujipatia fedha.

Aina nyingine ya uchumi inafanya kazi kwenye familia. Kazi ambayo kila mwanachama anafanya kwa ajili ya familia haipimwi kwa viwango vya dola. Kila mtu anategemewa atoe msaada kwa namna yeyote ile kadri atakavyoweza, bila ya kuwekewa masharti magumu. Msaada unatolewa katika maudhui ya kifamilia. Haitegemewi kwamba kila mwanachama aweze kufanya mambo yanayofanana na mwingine au afanye kazi yenye thamani inayofanana, lakini atapaswa afanye kile kinachoweza kufanyika. Kama mwanachama wa familia hayuko tayari kufanya kwa hiari kile ambacho anaweza kukifanya, atafuatiliwa kuhusiana na hilo na anaweza asipatiwe msaada anaohitaji kutoka kwa wanachama wengine.

> "Onyesha kwamba unataka kuwa Mkristo kwa kutenda mema, hasa kwa wale wa jamaa ya imani... Waajiri wao badala ya wengine. Nunua kutoka yao sivyo kutoka mtu mwingine. Kusaidiana katika biashara. Hasa kwa sababu ulimwengu utapenda walio wake, na wao tu."
>
> - John Wesley
> "Rules for the Society of the People Called Methodists"

Uchumi wa kanisa unapaswa uwe zaidi ni uchumi wa kifamilia kuliko uchumi wa jamii. Ili uweze kufanya kazi, mahusiano katika kusanyiko la kanisa ni lazima yawe ya zaiidi ya sana urafiki wa kawaida. Maswali mengi yataulizwa wakati mtu atakapokuwa anaomba msaada baada ya kutokuwa na uwajibikaji kwenye rasilimali zake mwenyewe au baada ya kuwa hashirikiani na wenzake kwa hiari katika kusaidia watu wengine.

Kusanyiko la kanisa linajifunza jinsi ya kukuza uhusiano wake miongoni mwa watu wake. Ni lazima waweze kuelezea kanisa kuhusu watu ambao kamwe huwa hawako tayari kusaidia watu wengine lakini wao wanaomba wapewe msaada. Ni lazima wawafundishe watu ambao hawawezi kushirikiana na wenzao. Ni lazima wakabiliane na wale ambao wanajiona wako huru kufuata matakwa yao wenyewe kwa kufuata mambo ya maadili yao wenyewe na hawako tayari kupokea marekebisho ya kichungaji.

► Je, kuna mifano gani ya njia ambazo wanachama katika kanisa wanaweza kusaidiana wao wenyewe? (Kazi za bustani, kutunza watoto wadogo, kuajiriwa, nyakati za matatizo)

## Maelekezo ya Vitendo

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Timotheo 5:3-16 kwa ajili ya kikundi.

Kifungu hiki kinatoa maelekezo ya vitendo vya jinsi kanisa linavyopaswa kutoa msaada kwa wanachama wake walio wahitaji. Aya ya 16 inasema kwamba watu wanapaswa wawasaidie watu wao wenyewe ili kanisa nalo liweze kusaidia wale ambao hawana watu wa kuwasaidia. Mtume anachukulia kwamba msaada wa kifedha kwa wanachama wake ni jukumu la kanisa.

Ni wazi kwamba, kama kila mwanachama atakuwa analitegemea kanisa kifedha, kanisa halitaweza kumsaidia kila mtu. Kifungu hiki kinatoa maelekezo ya vitendo ili kwamba kanisa liweze kusaidia wale watu ambao kwa hakika wanahitaji msaada huo.

Kifungu hiki kinazungumzia mahsusi kuhusiana na wajane, lakini kanuni zinaweza zikatumika pia kwa watu wengine. Tunatambua kwamba kanisa lina wajibu kwa ajili ya watu wengine: Yakobo 2:15-16 anaonyesha kwamba tunapaswa tuwajibikie katika hitaji la kaka au dada; Yakobo 1:27 anataja kuhusu wajane na yatima.

Kanuni tatu kuhusu msaada wa kifedha wa kanisa kwa wanachama wake:

1. **Familia ina jukumu la kwanza la kuwajibika.** Watu katika familia wanalo jukumu la kusaidia jamaa zao wenyewe walio na mahitaji ya kusaidiwa ili kanisa lisibebe wajibu wa kuwasaidia (1 Timotheo 5:4, 16). Kama mtu hawezi kuisaidia familia yake mwenyewe, huyo mtu siyo mwamini (5:8). Kama mchungaji ataona kwamba katika kanisa kuna uhitaji, atapaswa kutafuta ni kwa jinsi gani jamaa zake wanaweza kufanya katika kutoa msaada.

2. **Mwanachama mwaminifu anastahili apewe msaada.** Mjane anastahili kupewa msaada kama atakuwa ameishi maisha ya uaminifu ya Kikristo na alikuwa akisaidia watu wengine (5:10). Kanuni hii inaweza kutumika kwa watu wengine mbali na wajane, endapo watakuwa ni wahitaji na hawana uwezo wa kujisaidia wenyewe.

3. **Mwanachama atapaswa afanye jambo linalowezekana kufanywa na yeye mwenyewe na kwa watu wengine.** Mkristo anapaswa afanye jambo linalowezekana kufanyika kwa ajili ya kuwa baraka kwa watu wengine (5:10). Kama atakuwa hana kazi ya kuajiriwa, anaweza akatafuta njia nyingine ambazo anaweza kusaidia nazo watu wengine. Mtu ambaye kwa hiari yake mwenyewe hataki kufanya kazi, hapaswi kabisa kusaidiwa na kanisa (2 Wathesalonike 3:10).

► Mwanafunzi anapaswa asome 2 Wathesalonike 3:6-12 kwa ajili ya kikundi.

Kifungu hiki kinatueleza zaidi kuhusu maisha ya kanisa la mwanzo. Kwa hapa Paulo anashughulikia tatizo la watu ambao walikuwa wanalitegemea kanisa kwa ajili ya kupewa misaada ili kwamba wao wasifanye kazi. Walikuwa Wanatumia muda wao kwa ajili ya kutembelea tu watu na kueneza majungu.

Hali hii inatuelezea nini kuhusiana na kanisa la mwanzo? walikuwa wanachukua jukumu la kuwajali watu wao. Kanisa lilikuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba hakuna mtu yeyote ndani ya kanisa mwenye njaa. Walikuwa kama wanafamilia.

Kwa kuwa walikuwa kama wanafamilia, ilikuwa ni rahisi kwa mtu kuwa mvivu na kuwa tegemezi kwa watu wengine. Paulo aliwaambia kwamba wanapaswa wamtake kila mtu afanye lile linalopaswa kufanyika. Kama mtu hataki kwa hiari yake mwenyewe kufanya linalowezekana kufanyika, hataruhusiwa kula chakula ambacho kimetolewa na watu wengine.

Ni jambo zuri sana wakati kanisa linapokuwa ni kama familia inayotoa mahitaji ya aina zote. Ili hilo liweze kutendeka, kanisa ni lazima liwe na kanuni za kufuata. Kanisa ni lazima liwe na mahitaji kwa ajili ya wale walio tegemezi kwa ajili ya kupewa msaada na kanisa. Bila ya mahitaji, kanisa katika muda mfupi litaelemewa na watu wavivu na halitakuwa na uwezo wa kuendelea kutimiza mahitaji.

Wachungaji na mashemasi ni lazima walielekeze kanisa lifanye kazi kama familia. Ni lazima wawajibikie katika mahitaji kwa upendo. Hata hivyo, upendo una maana kwamba watakuwa tayari kuzungumza ukweli. Kama mtu hataki kuwajibika, mtu mwingine ni lazima awe tayari kuzungumza naye kuhusu jambo hilo. Kama mtu hatoi msaada kwa watu wengine na kufanya lolote analoweza kufanya kwa ajili ya kujisaidia yeye mwenyewe, kanisa halipaswi liendelee kutoa msaada kwake.

Ni haki kuuliza maswali wakati mtu anapojitokeza kuomba msaada. Je, yeye yuko tayari kuwasaidia watu wengine? Je, anafanya kazi wakati anapokuwa anaweza? Je, anatumia fedha zake kwa busara? Je, anachukua jukumu la kuijali familia yake?

Watu wengi wanakuja kwenye kanisa kuomba misaada. Kanisa ni lazima liwe na njia ya kuwajali watu kwa mara ya kwanza wanapokuja, hata kabla mtu huyo hajaonyesha kuwajibika. Kisha, ni lazima kuwepo na njia ya kukuza uhusiano. Mtu huyo atapaswa afahamu afanye nini ili kuwa sehemu ya ushirika wa kanisa.

**Taarifa Saba kwa Muhtasari**

1. Kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya kanisa huwaleta wanachama kwenye uhusiano wa karibu kwa ajili ya kushirikishana maisha pamoja.
2. Kanisa ni familia inayoshirikisha maisha ya kila siku na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya kukidhi kila hitaji.
3. Kanisa humkaribisha mwenye dhambi aliyetubu kwenye familia ya watu wenye imani ambapo hujifunza jinsi ya kuendeleza maisha yake mapya.
4. Kanisa linapokuwa linafanya wajibu wake kila siku, kunakuwepo na nafasi ya huduma kwa kila muumini.
5. Muda wa kanisa unapotumika kwa pamoja unahusisha huduma, mahitaji mbalimbali, kazi za kufanya, kuburudika, na nyakati za sherehe.
6. Ushirika wa Kikristo unahusisha pamoja na mambo mengine kushirikishana katika rasilimali muhimu.
7. Kanisa halipaswi kuwasaidia watu ambao hawataki kufanya lolote wanaloweza kufanya kwa ajili ya kujisaidia wao wenyewe na watu wengine.

**Kazi za kufanya Somo la 6**

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 6. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.
3. Kazi ya Kuandika: Je, kuna njia gani mbalimbali ambazo watu wa kanisa lako kwa pamoja wanashirikishana maisha zaidi ya ibada ya kuabudu?

# Somo la 7
# Kanisa katika Dunia

## Kanisa katika Jamii

► Je, ni kwa jinsi gani kanisa lihusike ndani ya jamii?

Yeremia aliandika kwa Wayahudi akiwa utumwani akiwaambia kuhusu uhusiano wao utakavyokuwa kati yao na jamii ya kipagani waliokuwemo. Wayahudi hawa walikuwepo utumwani pasipo matakwa yao; dini ya jamii iliyokuwepo ilikuwa ya kipagani; serikali iliyokuwepo ilikuwa ya ugandamizaji iliyoharibu taifa lao; na, walikuwa wakingojea siku ambayo wangeondoka. Labda walifikiri hawangejihusisha na matatizo yeyote ya jamii ile.

Sikiliza ujumbe ambao Mungu alimpa Nabii kwa ajili ya watu hawa:

> Kautakieni amani *(shalom)* mji ule, ambao nimewafanya mchukuliwe mateka, mkauombee kwa Bwana; kwa maana katika amani yake mji huo ninyi mtapata amani (Yeremia 29:7).

*Shalom*, neno hili kwa kawaida likiwa linatafsiriwa kwamba ni amani, halirejelei tu amani peke yake, bali pia baraka zinazoambatana na amani. Linarejea baraka zinazotoka kwa Mungu. Hawa watu waliokuwa wakimwabudu Mungu katika nchi ya wapagani wanaenda kupata baraka wanapokuwa wanajaribu kuzileta baraka hizo kwa watu wa jamii ya makafiri!

> "Kanisa la Kikristo ni jumuiya ambamo Roho Mtakatifu hupitia kwa ajili ya kuongoza ukombozi na ugawaji wa karama, njia ambayo Mungu huitumia kufanyia kazi yake ya upatanisho katika Kristo aliyeko kwa wanadamu. Kanisa limeitwa kutoka katika dunia ili kusherehekea ujio binafsi wa Mungu, na limetakiwa lirejee duniani kwa ajili ya kutangaza ufalme wa Mungu ulio kiini cha ujio binafsi wa Mungu na tegemeo la kurejea tena alikotoka."
>
> \- Thomas Oden,
> *Life in the Spirit*

Matatizo ya dunia yanatokana na chanzo chake cha ndani cha tatizo la dhambi. Watu binafsi na mataifa yenye nguvu yaliyojipanga vizuri hawaheshimu Neno la Mungu. Kanisa ndilo pekee lenye sifa ya kuweza kuzungumzia matatizo ya dunia kwa sababu kanisa lina uwezo wa Kufafanua Neno la Mungu na kudhihirisha hekima ya Mungu. Kanisa halipaswi tu kuzungumzia na kuwa kinyume cha dhambi zilizopo katika jamii, bali pia kufafanua na kudhihirisha ni kwa jinsi gani jamii inapaswa ifananie.

## Kanisa na Majirani Wanaolizunguka

► Je, ni alama gani zinazoonyesha mafanikio kwa ajili ya kanisa?

Kutokana na kuwepo kwa dhana ya mafanikio ya kidunia, mtu anaweza akafikiri kwamba kanisa lina mafanikio kama lina mahudhurio ya watu wengi, bajeti kubwa, na jengo kubwa sana.

Walio Wakristo kamili wanajua kwamba mambo hayo hayana maana yeyote mbele za macho ya Mungu, bali tu mara nyingi tunavutiwa na mambo hayo. Kwa kawaida tunafikiria kwamba mchungaji anakuwa amefanikiwa kama atakuwa na kanisa kama hilo.

Kipimo muhimu cha kupima mafanikio ni idadi ya watu wanaookoka kwa uhakika kwa sababu ya huduma ya kanisa. Kukua kiroho kwa waumini pia ni jambo muhimu sana, lakini lililo na ugumu wa kupima. Udhihirisho wa kweli wa mafanikio ya kanisa ni mabadiliko yanayoonekana kuletwa na kanisa kwa majirani waliolizunguka.

► Je, unafikiria nini kuhusu taarifa hii?

> Mafanikio ya kanisa la mtaa yanapaswa yashikamane moja kwa moja kwenye kiwango kwamba linaleta mabadiliko ya ujumla na ya haraka kwa ujirani unaolizunguka. Hiki ni kigezo muhimu, Kigezo kingine chochote cha mafanikio kinafuata baada ya msingi huu.[6]

Injili huleta matokeo makubwa nje ya watu ambao tayari wameshaokoka. Kila mtu aliyeokoka na kuanza kuishi maisha yanayoendana na kanuni za Ukristo huwa ni kivutio kwa watu wengine. Yesu alisema kwamba wafuasi wake ni chumvi na mwanga wa ulimwengu.

Kanuni za Ukristo ndizo zilizo msingi wa uhuru na haki, na ndizo zilizo kigezo kikuu cha kuweza kuleta mabadiliko kwenye jumuiya. Kama kanisa linawashawishi watu kufuata kanuni za Ukristo, jumuiya itakuwa tayari kushawishika kuanzishwa kwa uhuru na haki.

Hali hii pia inahusika kwenye jumuiya ya mtaa. Kama watu walio majirani watakuwa wameokoka, kwa vyovyote kutakuwepo na mabadiliko kwenye ujirani wote.

► Je, kuna mabadiliko gani yatakayotokea kwenye majirani wako kama watu wengi wangeweza kushawishika kufuata kanuni za Ukristo?

Itakuwa na maana gani kwa majirani wanaokuzunguka kushawishiwa na huduma ya kanisa lako? Kutakuwepo na upungufu wa uhalifu, kuwanyanyasa watoto na kuwapuuza, tabia zisizo za kimaadili, machafuko, ubaguzi wa rangi, biashara haramu, biashara za uyanyasaji, na mambo ya kishenzi *(uharabu)*. Wapangaji watakuwa waaminifu zaidi. Wapangishaji watatoa nyumba zilizo na usalama zaidi. Watu wengi watakuwa na uwezo wa kumiliki maskani yao wenyewe. Wafanyabiashara watakuwa tayari kutengeneza nafasi za kuwaendeleza watu wao waliowaajiri. Watu walioajiriwa watakuwa na tabia nzuri zaidi kwa ajili ya kazi.

---

[6] John Perkins, akinukuliwa na Daniel Hill katika "Church in Emerging Culture," in *A Heart for the Community*. Kimfanyiwa uhariri na John Fuder na Noel Castellanos. (Chicago: Moody Publishers, 2009), 203.

Matokeo ya kiroho kwa ajili ya kanisa ndiyo kipaumbele cha kwanza, lakini kama matokeo hayo yatakuwa ni halisi, yatadhihirishwa kwenye mabadiliko yatakayoonekana kutoka kwa majirani waliolizunguka.

### Huduma kwa Watu Maskini

► Je, Yesu alisema kwamba amri kuu ya pili ni ipi?

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Luka 10:25-29 kwa ajili ya darasa.

Mwanasheria alimwuliza Yesu jinsi ya kuupata uzima wa milele. Yesu akamwuliza, "Imeandikwa nini katika torati?" Katika kujibu, mwanasheria alichanganya sheria kuu mbili. Alisema kwamba unapaswa kumpenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na jirani yako kama nafsi yako (Luka 10:27). Yesu alimjibu kwamba jibu lake lilikuwa sahihi, kisha akamwambia, "Fanya hivi nawe utaishi". Mtu aliye na upendo wa aina hiyo anao uzima wa milele.

Kisha mwanasheria akauliza, "jirani yangu ni nani?" Hakuwa anafikiria kwamba alitakiwa ampende kila mtu. Alikuwa anataka apate upenyo mwembamba wa aina fulani ya watu ambao ni lazima awapende, ili aweze kujisikia kwamba alikuwa anatimiza matakwa yote ya sheria. Yesu alijibu swali hili kwa kutumia hadithi.

► Je, ni hadithi gani Yesu aliyotumia kama mfano wa kumpenda jirani yako?

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Luka 10:30-37 kwa ajili ya darasa.

Yesu alielezea hadithi ya Msamaria Mwema kama mfano wa kile kinachomaanisha kumpenda jirani yako kama unavyojipenda wewe mwenyewe. Upendo unaleta hamasa au motisha kwetu sisi kwa ajili ya kuwajibika kwa mtu aliye mhitaji.

Yesu alielezea kazi yake maalumu katika Luka 4:18-19:

> Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.

Taarifa hii inajibu swali linaloulizwa kwamba, *Kwa nini Yesu alikuja?* Yesu alisema kwamba hili ndilo alilotiwa mafuta ili alifanye. Lilikuwa ni kusudi lililokuwa limetabiriwa kwa ajili yake katika Agano la Kale.

Kazi ya Yesu maalumu inatoa mwelekeo kwa kanisa, lililo "mwili wa Kristo" ulimwenguni. Jambo la kwanza Yesu alilolisema lilikuwa ni kuwahubiri maskini habari njema. Kanisa litakuwa halikamilishi kazi yake maalumu kama litakuwa linazembea au kuwatenga watu maskini. Yesu alisema kwamba maskini ni watu waliobarikiwa kwa ajili ya ufalme wa mbinguni (Luka 6:20). Mtume Yakobo alisema kwamba Mungu aliwachagua maskini wa dunia wawe matajiri wa imani (Yakobo 2:5). Mungu amechagua kudhihirisha uwezo wake kwa kuwatumia maskini na wanyonge wa dunia hii (1 Wakorintho 1:27-29). Kanisa lina

sababu nyingi za kufanya jitihada maalumu kwa ajili ya kufanya uinjilisti kwa watu maskini. Sababu mojawapo ni kwamba injili huenea kwa haraka zaidi miongoni mwa watu walio maskini.

Maelezo kuhusiana na huduma ya Yesu yanaonyesha kwamba alikuwa anategemea pia kubadilisha hali zilizopo za ulimwengu.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Mika 6:6-8 kwa ajili ya darasa. Nabii alikuwa anauliza swali gani?

Nabii Mika alilitafakari swali ambalo Mungu kwa uhakika anataka kutoka kwa watu wake wanaomwabudu. Baadhi ya watu waliuliza kama mafahali ya wanyama yangeweza kutosha kwa ajili ya dhabihu. Mika akaeleza kwamba siyo suala la kutafuta dhabihu ambayo ni kubwa mno kwa ajili ya kuwa na thamani mbele za Mungu. Mungu ameshatoa mahitaji yake. Tuna wajibu wa kutenda haki na kusaidia watu wengine katika kupata haki.

Huruma hairejei tu kwenye aina ya matumizi ya mamlaka. "Huruma hurejea kwenye unafuu wa mahitaji. Yesu alisema kwamba yule Msamaria Mwema alikuwa ni mfano wa upendo ambao Mungu anaagiza kwa sababu "alionyesha upendo." Wakati mwingine makanisa yanadhania kwamba yanapaswa yawe katika mtazamo wa mahitaji ya kiroho tu. Wanadhania kwamba hawana wajibu katika masuala ya umaskini. Hata hivyo, Biblia inataja maskini mara 400. Matatizo ya maskini yanahusika na Mungu. Kama ilivyokuwa kwa Msamaria Mwema, Makanisa yanapaswa yaonyeshe upendo kwa wale watu wanaoonekana kwamba wanahitajika kupewa msaada.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Ezekieli 16:49-50 kwa ajili ya darasa. Aya hizi zinataja dhambi gani ya Sodoma?

Jiji la Sodoma linakumbukwa kwa ajili ya dhambi ya matendo ya uasherati; lakini uovu wa jiji hilo haukuwa matendo haya peke yake. Watu wa Sodoma walitumia mafanikio yao katika kujipatia starehe wao wenyewe na hawakutafuta njia ya kuwawezesha maskini ili waweze kubadilisha hali zao za maisha.

### Dhana ya Parishi au parokia/usharika

Wakati kanisa linapokuwa na wajibu kwa ajili ya aina fulani ya majirani wanaowazunguka, eneo hilo la kanisa linaitwa Parokia au usharika. Kihistoria, mashirika makubwa ya makanisa walitegemea kila kanisa la mtaa litumike kwa ajili ya eneo maalumu la kijiografia. Hii ni tabia ya Kanisa Katoliki katika maeneo mengi duniani, Kanisa la Kilutheri la Ujerumani, na Kanisa la Uingereza nchini Uingereza. Madhehebu mengi ya Kiprotestanti hayana parishi au Parokia/usharika kwa njia sawa.

Jaribu kufikiria itatokea nini kwa kanisa kujifikiria lenyewe kama ni kanisa kwa ajili ya jamii. Kila mtu katika parishi au usharika huo atakuwa amejua mchungaji ni nani na kwamba alikuwa anapatikana kwa ajili ya maombi, kufariji na kutia moyo, kushauri, aidha wakiwa wanahudhuria kwenye kanisa lake au la. Anapokuwa anafanya ziara miongoni mwa jamii,

lengo lake la msingi halitakuwa kushawishi watu wahudhurie kwenye kanisa. Badala yake, atakuwa anapeleka huduma ya kanisa kwao.

Kanisa linatakiwa lipeleke huduma ambazo zinakubaliana na mahitaji ya majirani wanaowazunguka, kama vile, ushauri wa kifamilia, kutoa nasaha kwa vijana, na mafunzo ya kazi yanayohusiana na mienendo ya tabia. Haya siyo kwamba hayahusiani na kusudi la kanisa. Ni maeneo ambayo Biblia hujibu masuala yote nyeti, na kanisa linapaswa lishirikishe hekima ya Neno la Mungu kwenye maeneo ya matendo. Ni rahisi kunyooshea kidole mambo ya uovu yaliyoko ndani ya jumuiya, lakini kanisa linapaswa litoe ufafanuzi wa jinsi jumuiya inavyotakiwa iwe.

► Je, ni mahitaji gani yaliyopo kwenye jamii inayokuzunguka ambayo yanaweza yakabadilishwa na Neno la Mungu?

> "Kama mwili wa Yesu, kanisa ni kikundi cha ushirika wa kuabudu ambacho kipo katika kutimiza mapenzi ya Mungu na kuwakilisha matarajio ya Ufalme wake."
>
> - Larry Smith,
> *I Believe: Fundamentals of the Christian Faith*

Manabii wa Agano la Kale waliona kwamba ardhi na watu waliopo ni mali ya Mungu, na kumtaka kila mtu alishike Agano la Mungu. Walihubiri kuhusu baraka zilizokuja kwenye jumuiya wakati zikifuata mpango wa Mungu na kuhusu laana ambazo zilikuja kutokana na kukosa utiifu.

Mchungaji anapaswa aione jumuiya yake kama ni parishi au usharika wake ulio chini ya Mungu. Mungu ndiye Mmiliki na Mtawala anayetoa baraka kama wataishi kwenye mpango wake. Mchungaji anatakiwa aendelee kuwataka watu wa jumuiya waishi ndani ya maelekezo ya Mungu. Atapaswa aelezee inamaanisha nini kuishi na baraka za Mungu na kuwatia moyo kuja kwenye uhusiano na Mungu.

Dhana ya parishi au usharika haimaanishi kwamba kila mtu kwenye majirani wanaokuzunguka ni mwanachama wa kanisa. Kanisa linahusisha tu wale ambao wamemaanisha na kujikabidhi kuishi maisha yenye uhusiano na Mungu, lakini jumuiya hushawishiwa na kanisa.

Dhana ya parishi au usharika haimaanishi kwamba majirani wanaokuzunguka wanathibiti kanisa na kuweka vigezo vyake. Kanisa limesimikwa na Mungu, linafuata Neno Lake, na kwamba linawakilisha ufalme wa Mungu kwa majirani wanaolizunguka.

Kwa kuwa kanisa limetakiwa kuwa chumvi na nuru inayoangaza, kanisa limetakiwa kuleta mabadiliko kwa majirani wanaolizunguka.

### Kipaumbele cha Injili

Huduma nyingi zinatoa programu ambazo zinakidhi mahitaji kwa majirani wanaowazunguka. Wanahudumia mahitaji ya jumuiya na kufikiri kwamba kuwahudumia watu kwa njia za vitendo kutawafanya wawe marafiki na kusababisha wawe makini kwa ajili ya kupokea injili. Malengo yao ni kutengeneza nafasi za kushirikisha injili. Wanataka waonyeshe kwamba ni watu wanaojali.

Mpangilio wao ni kama ifuatavyo: Programu, kisha Mahusiano, kisha Injili. Hata hivyo, kuna njia nyingi zinazosababisha programu hizo kwenda vibaya. Msaada labda hautaunda uhusiano wowote isipokuwa uhusiano wa mtoaji na mpokeaji tu.

Wakati mwingine injili inaonekana kutengwa kutoka katika vitu vingine vinavyotolewa, na watu wanaweza kupata msaada bila ya kuwa na hamasa kwa injili. Watu wanaokuwa watendakazi katika huduma wanaweza kuwa na harakati kubwa sana za kutoa msaada na siyo kushirikisha injili. Wapokeaji wa misaada wanaweza wakapokea vitu vingi sana kisha wakaondoka tena kwenda kutafuta msaada mahali pengine.

Mpangilio huo unabidi ubadilishwe. Kanisa linapaswa liweke msisitizo wa injili kwanza kama kipaumbele chake cha kwanza cha kukutana na kila mtu.

► Injili ni nini?

Wakati kanisa linawasilisha injili kwa ulimwengu, ni lazima waweze kuwa waaminifu kuhusisha pamoja na maelezo ya maisha mapya ndani ya kanisa. Wokovu siyo maamuzi binafsi ambayo yanamwacha mtu peke yake katika hali ya maisha mapya yasiyoeleweka ni kitu gani. Watenda dhambi kwa kawaida hawatakubaliana na injili hadi hapo watakapokuwa wamevutiwa kwenye jumuiya ya watu wa imani ambao wanawasilisha injili.

Kwenye huduma ya Yesu na mitume, tunaona kwamba injili ni "habari njema" za ufalme wa Mungu. Ni ujumbe ambao mwenye dhambi anaweza kupokea msamaha na kuja kwenye uhusiano na Mungu. Anakombolewa kutoka kwenye nguvu ya dhambi na kufanywa kiumbe kipya. Anaingia kwenye familia ya watu wenye imani, mahali ambapo kaka na dada zake wa kiroho watamtia moyo na kumsaidia katika mahitaji yake.

Kanisa linapaswa lione kusudio lake la msingi la kuwasilisha injili. Kila mtu anatakiwa afahamu kwamba kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho za watu ni kitu ambacho kiko kwa ajili ya kanisa. Kisha, kanisa linawavutia watu ambao wako kwenye utayari wa injili. Huduma ya injili inatengeneza uhusiano.

Kisha baada ya hapo kanisa linasaidia watu walioko kwenye uhusiano na kanisa. Inawezekana ikawa siyo watu wote ambao watakuwa tayari wameokoka, lakini wakavutiwa na huduma ya injili ya kanisa.

Kwa hiyo, huduma ambayo imebadilishwa ni Injili, kisha Uhusiano na kisha Msaada (na siyo programu). Kanisa halipaswi kuwa kama shirika linalotoa huduma za kusaidia. Badala yake, kanisa ni kikundi cha watu ambacho kinasaidia watu walioko kwenye uhusiano pamoja na wao. Endapo wataanzisha programu mbalimbali, watu watajitokeza kwa ajili ya programu hizo bila ya uhusiano.

## Taarifa Saba kwa Muhtasari

1. Kanisa lenye matokeo yanayotarajiwa husababisha mabadiliko kwa majirani wanaowazunguka.
2. Ni lazima tuonyeshe upendo wetu kwa majirani zetu kwa kuwajibika katika mahitaji yao.
3. Kanisa linapaswa liwahudumie watu walio maskini ili kukamilisha umisheni wake.
4. Kanisa linapaswa liwahudumie watu walioko kwenye eneo lao la kijiografia.
5. Kanisa linapaswa lielezee na lidhihirishe ni kwa jinsi gani jumuiya inapaswa iwe.
6. Huduma ya injili ni kipaumbele cha kwanza cha kanisa.
7. Kanisa linapaswa liwe na msaada kwa watu kwenye muktadha wa uhusiano.

## Kazi za kufanya Somo la 7

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 7. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.
3. Masailiano: Zungumza na watu kadhaa wasio hudhuria kanisani. Watake wakuelezee ushawishi wa kanisa kwa majirani wanaolizunguka. Andika muhtasari wa mahojiano hayo.

# Somo la 8
# Msaada wa Kanisa la Mahali

## Maagizo ya Yesu

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Luka 10:1-9 kwa ajili ya kikundi. Je, kuna kitu gani kisichokuwa cha kawaida kuhusiana na maelekezo ya Yesu aliyowapa wanafunzi wake wakati alipowatuma kwenda kufanya huduma?

Wanafunzi walitumwa kuwa wa kwanza kuhubiri injili katika maeneo mengi ya vijiji. Yesu alikuwa na uwezo wote na nyenzo zote na alikuwa na uwezo wa kuwapa kitu chochote. Angeweza kuwapa fedha za kuwatosha katika kununua chochote ambacho wangehitaji katika kukidhi mahitaji ya watu wengine. Angeweza kuwapa nguvu za kujigawia mkate na Samaki wao wenyewe na kwa ajili ya watu waliokuwa wanawahubiria. Wangeweza kugawa chakula kwenye kila Kijiji walichokuwa wanakitembelea.

Badala yake, aliwatuma bila fedha. Aliwaambia wategemee kupata misaada yao kutoka kwa watu waliokuweko katika vijiji walivyotembelea. Mitume walikwenda kama Yesu alivyowaagiza, na walipatiwa mahitaji yao (Luka 22:35).

► Je, kwa nini Yesu aliwatuma kwa njia hii?

Huduma yao iliwavutia watu sahihi. Kwa kuwa walihubiri injili kwanza, waliwavutia watu waliokuwa wanahitaji injili. Kwa kuwa walikuwa na mahitaji, waliwavutia watu waliotaka kusaidia. Walikuwa na watu wazuri sana kwa ajili ya mwanzo wa kanisa.

Je, ingekuwaje kama wangeenda kwenye vijiji wakiwa na kila kitu ambacho walikuwa wanakihitaji pamoja na vitu vya kuwapa watu? Wangewavutia watu ambao siyo sahihi. Wangeweza kukusanya kundi la watu ambao wangekuja kwa ajili tu ya kupata kitu chochote. Baada ya hapo, huduma ingekuwa endelevu tu kwa kuendelea kuwapa vitu. Hawangeweza kupata wa kuwasaidia bila kuwalipa kwanza. Hawangeweza kuwa na kikundi cha watu ambao wangekuwa ni chanzo kizuri cha wao kuweza kuanzisha kanisa.

Mfumo ambao Yesu alikuwa amewapa uliweza kuanzisha kikundi ambacho kingefanyika ni kanisa. Lilikuwa ni kundi la watu walisisimka na ujumbe wa injili na kutamani kusaidia. Ni muhimu sana kwamba makanisa yaweze kuanza katika njia iliyo sahihi.

## Sababu Zinazofanya kanisa liweze Kupata msaada wa Mahali Pale Pale

► Je, ni kwanini kanisa lipate msaada wa mahali pale pale? Kabla ya kuangalia orodha ya sababu zinazofuata hapa chini, ni sababu gani nyingine unazoweza kuzifikiria?

1. **Yesu alituonyesha kwamba huduma ya mahali inapaswa ianze kwa njia iliyo sahihi.** Aliwatuma wanafunzi wake kutoka nje bila ya kuwa na fedha ili kwamba huduma yao iweze kuwa kivutio kwa watu waliokuwa wanavutiwa na injili na ambao walikuwa wanataka kutoa msaada.

2. **Mungu alitoa maelekezo ya kutoa kwa ajili ya makanisa ya Agano Jipya.** Makanisa yalitakiwa kutuma misaada ya uwezeshaji kwa ajili ya kanisa la kwanza katika Yerusalemu (1 Wakorintho 16:1-3; 2 Wakorintho 8:1-7, 2 Wakorintho 9:1-6). Yalitakiwa kuwatunza wajane na watu wengine waliokuwa wahitaji katika kanisa (1 Timotheo 5:16; Yakobo 1:27, Yakobo 2:15-16). Yalitakiwa kutoa msaada kwa watu walioko kwenye huduma za kudumu (Wagalatia 6:6).

3. **Mungu huliwezesha kila kanisa kuwa mwili wa Kristo pale mahali lilipo (**1 Wakorintho 12:27**).** Hii inamaanisha kwamba kanisa lililokuwa linaweza kufanya maamuzi na kuendeleza maono kwa ajili ya huduma zake lenyewe. Hali hyo haiwezi kutokea kama kanisa ni tegemezi kwa viongozi wake wa nje kwa ajili ya msaada na mwelekeo wa kanisa. Msaada wa kifedha kutoka mahali pale lilipo ni muhimu sana kwa ajili ya kukua kwa kanisa.

4. **Mungu hubariki mapato ya kifedha ya watu wanaotoa zaka.** Laana iko juu ya mapato ya kifedha ya watu ambao hawatoi zaka (Malaki 3:8-10).

5. **Kuwa tegemezi kwa misaada kutoka nje kunaliweka kanisa la mahali/mtaa katika hatari.** Uchumi wa Kitaifa na wa Kimataifa hazina uhakika. Endapo wafadhili wa nje wataacha kutoa misaada yao, makanisa yaliyo tegemezi kwao yatataabika.

6. **Wachungaji wanapaswa wahudumiwe na watu wao wanaowahudumia (**Wagalatia 6:6**).** Kusanyiko la kanisa la mtaa linatambua kama mchungaji wao ni mwaminifu. Wanajua kama anautumia muda wake mwingi kwenye huduma. Hapaswi kupewa misaada ya muda mrefu na watu walio mbali na kanisa.

► Je, kuna matatizo gani yanayojitokeza kutokana na kuwa tegemezi kwa misaada ya mbali?

## Sera za Kifedha za Umisheni kulingana na Utawala wa Ndani wa Kanisa la mahali

Umisheni wa Kimataifa au dhehebu unapaswa kufuata baadhi ya kanuni ambazo kwa njia nyingine zinasaidia makanisa. Shirika linapaswa liwe makini katika kusaidia kwa njia ambayo itayafanya makanisa yawe imara zaidi, kuliko kuyafanya yawe tegemezi zaidi. Hapa kuna mifano ambayo umisheni au dhehebu wanaweza wakaikuza.

1. **Kusisitiza kuhusu kutoa zaka kama msingi wa mapato ya kifedha wa Mkristo.** Kama kusanyiko la kanisa litakuwa halitoi zaka, Mungu hataweza kubariki mapato ya kifedha ya kanisa. Kama tayari hawafanyi kile ambacho walitakiwa wakifanye, itakuwa wana uelewa potofu kuhusiana na huduma ya mapato ya kifedha. Msaada wa nje unafanya mambo kuwa mabaya zaidi badala ya kuwa mazuri zaidi.

2. **Fanya miradi ambayo itatoa kitu cha kudumu kuliko msaada kuwa mapato ya kila siku,** Shirika linapaswa litumie fedha kwa ajili ya miradi ambayo itaweza kusaidia kanisa liwe na nguvu zaidi kifedha, kuliko kutoa mishahara ambayo inafanya kanisa liwe tegemezi kwa misaada kutoka nje. Mahali ambapo mishahara ya kila mwezi kutoka katika shirika tayari inakuwa ipo, shirika linapaswa lifanye mpito wa kulisaidia kanisa liweze kujitegemea lenyewe.

3. **Usianzishe huduma ambazo kamwe haziwezi kupata msaada wa mahali pale pale ulipo.** Mashirika hayapaswi kuanzisha mambo ambayo yatakuwa tegemezi kutoka misaada ya nje kwa muda wote itakapokuwa inafanya kazi. Lengo ni kuanzisha huduma au shughuli za biashara ambazo zinaweza zikawa ni za kanisa la mahali na ziendeshwe kutokea mahali pale pale. Kwa mfano, uwepo wa shule unapaswa uwe ni huduma ya kanisa la mahali.

   Juhudi zozote za huduma ambazo kamwe hazina uwezekano wa kufadhiliwa na watu wa mahali pale pale zinatakiwa ziwe ni kitu cha muda ambacho kinalenga kukamilisha kusudi fulani kwa haraka bila ya kutengeneza utegemezi (Mifano: Ufanyaji wa makongamano na uendeshaji wa semina mbalimbali).

4. **Kuujengea uwezo uongozi wa kanisa la mahali kuliko kulipita kando.** Wakati watu wa nje au viongozi wa ngazi za juu wanapotoa misaada moja kwa moja kwa watu wenye mahitaji bila ya kupitia kwa viongozi wa kanisa la mahali wale walioko kwenye huduma za kanisa la mahali wanaonekana kwamba hawana ufanisi wowote. Kuliko kutoa misaada moja kwa moja kwa watu wenye kuhitaji misaada katika kanisa la mahali, shirika linapaswa liwawezeshe viongozi wake katika kukidhi mahitaji hayo.

► Je, kuna mifano gani iliyopo ya aina potofu ya misaada ya umisheni? Je, kuna mifano gani iliyo sahihi ya aina ya misaada ya umisheni?

## Kuepuka huduma ya misaada

Kanisa halipaswi kuweka kando vipaumbele vyake kwa ajili ya "huduma ya msaada." Kuna watu na mashirika ambayo yanataka kutoa rasilimali zao kwa ajili ya kuondoa umaskini lakini hawana mawasiliano ya moja kwa moja na watu ambao ni wahitaji. "Mashirika ya misaada" ni mashirika ambayo hukusanya rasilimali kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya kuwapa watu wenye uhitaji wa kupewa misaada. Wakati mwingine wakuu wa misaada hiyo hupata mishahara kutokana na rasilimali walizo nazo. Wakati mwingine kunakuwepo na udanganyifu, wafadhili pamoja na walio na uhitaji wa kupewa misaada wanatapeliwa. Hata wakati ambapo misaada inaenda kwa watu sahihi, watu wanaotoa huduma ya msaada

wanakuwa na mwenendo wa kutaka kumfurahisha zaidi mfadhili kuliko kujaribu kuelewa mahitaji halisi ya watu.

Huduma ya msaada kwa kawaida hulipita kando kanisa la mahali. Inatolewa katika njia ambayo inapuuzia uhusiano wa kanisa na watu wanaopokea msaada. Kutoa kuna matokeo mazuri wakati inapofanyika kupitia kwa kanisa, kwa viongozi ambao wanajua hali halisi za watu, na kwa njia ambayo inaonyesha umuhimu wa kanisa.

Endapo shirika litakuwa linatimiza mahitaji ya watu maskini (kama chakula) bila ya kubadilisha hali zao, inamfanya yule maskini kuwa tegemezi zaidi. Kama watakuwa wanazo rasilimali za kutosha, wanaweza wakaanzisha jumuiya za watu ambao ni tegemezi. Wakifanya hivyo kuendelea kufanya hivi kwa kipindi kirefu, watakuwa wanainua vizazi vipya vyenye watu ambao ni tegemezi.

Umisheni haupaswi kuwepo kwenye sehemu ya huduma ya msaada na ukasahau vipaumbele vya kanisa. Kwa kufanya hivyo hatimaye kwa pamoja kutaliumiza kanisa na watu wenye mahitaji.

► Je, ni mifano gani ambayo ulishawahi kuiona ya huduma ya msaada na matokeo yake?

## Mpango wa Mungu katika Kuwawezesha Wachungaji

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Kumbukumbu la Torati 18:1-5 kwa ajili ya kikundi. Je, kifungu hiki kinatuelezea nini kuhusiana na msaada wa kifedha kwa ajili ya huduma?

Kuwasaidia kifedha watu walioko kwenye huduma ya wakati wote ilikuwa mpango wa Mungu tangu nyakati za Agano la Kale. Makuhani walipaswa kuungwa mkono kwa kazi yao hekaluni. Hawakupokea urithi wa ardhi, kwa sababu hawakutakiwa kuwa na shughuli za kilimo.

Uwezeshwaji wa kifedha kwa ajili ya watu walioko kwenye huduma ya wakati wote ulikuwa ni mpango wa Mungu tangu wakati wa Agano la Kale. Makuhani au makasisi walikuwa wawezeshwe kwa ajili ya kazi zao katika hekalu. Hawakupewa kumiliki sehemu yeyote ya kipande cha ardhi, kwa sababu hawakutakiwa kujishughulisha sana katika mambo ya kilimo.

Wakati mwingine Israeli iliposhuka katika kiwango chao cha uaminifu wa kuabudu, uwezeshwaji kwa ajili ya makuhani au makasisi pia ulishuka. Ilikuwa ni ishara ya kukosa uaminifu wakati watendakazi katika hekalu wanapoliacha hekalu na kuondoka kwenda kutafuta njia nyingine za kujisaidia wenyewe (Nehemiah 13:10).

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 9:1-14 kwa ajili ya kikundi. Je, kifungu hiki kinatuelezea nini kuhusiana na msaada wa kifedha kwa ajili ya huduma?

Paulo alisema kwamba mpango wa Mungu ni kwa ajili wahubiri wa injili kuwezeshwa na huduma zao, kama ilivyo katika mfumo wa Agano la Kale (1 Wakorintho 9:13-14). Paulo alitumia vielelezo kadhaa kuhusiana na kanuni hii. Mkulima anawezeshwa na mazao

anayolima. Mchungaji wa wanyama anawezeshwa kutokana na ongezeko la mifugo yake. Askari haendi vitani kwa gharama zake mwenyewe.

Mtume anasema kwamba huduma inahitaji uangalizi kamili wa mchungaji. Hali iliyo nzuri ni kwa yeye kuweza kuachana na shughuli nyingine za ajira (aya ya 6). Mtume anasema kwamba huduma pia ni lazima iweze kumwezesha mke wa mchungaji, ikimaanisha pia ni pamoja na watoto (aya ya 5).

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Timotheo 5:17-18 kwa ajili ya kikundi. Je, kifungu hiki kinatuelezea nini kuhusiana na msaada wa kifedha kwa ajili ya huduma?

Wazee watawalao vema wanatakiwa wahesabiwe kustahili heshima maradufu. Aya ya 18 inaonyesha kwamba heshima hiyo ni uwezeshwaji wa kifedha.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Wagalatia 6:6 kwa ajili ya kikundi.

Mtu anayepokea mafao kutoka katika huduma anatakiwa atoe msaada katika kuwezesha huduma.

## Mwanzo wa kawaida wa Kuanza Kanisa

Tangu wakati wa karne ya kwanza ya kanisa, makanisa mengi yamekuwa yakianza kama vikundi vidogo vilivyokusanyika nyumbani kwa watu. Majengo ya makanisa hayakuwahi kuwepo kwa miaka mia mbili ya kwanza, lakini bado Ukristo ulienea kwa haraka sana. Katika majiji makubwa, maelfu ya watu walikutanika kwenye ibada za makanisa, lakini bado walikuwa wanakutana tena kwa vikundi majumbani kwa watu.

Paulo alipokuwa akisafiri na kufanya uinjilisti, kipaumbele chake kilikuwa ni kuanzisha kanisa katika kila eneo alilokuwa akipita. Njia hiyo pamoja na mambo mengine ilihusisha kuteua wachungaji (Matendo 14:23; Tito 1:5). Mchungaji katika kila eneo alikuwa ni mtu ambaye tayari alikuwa anaishi katika eneo hilo na alikuwa sehemu ya ushirika husika.

> "Tusisifu wale wapangaji wasio na makazi ambao huzurura huku na kule bila kuungana na kanisa lolote, kwa sababu popote pale hawaoni maadili yao yakitimia, daima kuna kitu kinachokosekana."
>
> – Philip Melanchthon, *Loci*

Mchungaji kwa kawaida huanzisha huduma yake bila ya kuwa na msaada wa kifedha. Anakuwa anamsaidia mmishenari au anaanza kuhubiri injili bila ya uwepo wa mmishenari kwa sababu ana matamanio ya kutoa msaada. Ataanza kuonyesha karama na uwezo kwa ajili ya huduma. Atafanya hayo siyo kwa ajili ya kulipwa, bali kwa sababu ya ari ya kiroho.

Kikundi cha watu walioamini kinapokuwa kimeundwa, majukumu ya mchungaji huongezeka na kutumia muda mwingi zaidi. Kikundi kinapaswa kiwe msaada wa kumwezesha mchungaji ili aweze kutumia muda wake mwingi vizuri kwenye huduma. Mwanzoni uwezeshaji unaweza usiwe katika hali ya ukamilifu, lakini unaweza ukawa unaongezeka polepole.

► Je, utasemaje kwa mtu ambaye anasema kwamba anataka kuwa mchungaji lakini anangojea msaada wa kifedha?

### Mambo yenye upekee

Paulo alielezea kwamba Mpango wa Mungu ni kwa ajili ya wachungaji kupata uwezeshwaji. Hata hivyo, huduma yake mwenyewe wa wakati mwingine ilikuwa ya kipekee. Kwenye maeneo kadhaa alifanya kazi kwa ajili ya kujisaidia yeye mwenyewe (1 Wathesalonike 2:9; 2 Wathesalonike 3:8).

Kanisa Jipya haliwezi kuwa na uwezo wa kumtegemeza mchungaji kwa ukamilifu wote. Wakati mmishenari anapoondoka na kwenda kwenye eneo jipya kwa ajili ya kuhubiri injili, inawezekana kusiwepo na msaada wa kumtosha. Kwa hiyo, mhubiri anapaswa awe ni mtu ambaye anahubiri kwa sababu ana matamanio ya kufuata wito wa Mungu. Atafanya huduma kwa sababu iko kwenye moyo wake, hata kama halipwi chochote.

Kama mchungaji hayuko tayari kwa hiari yake kufanya shughuli zitakazosaidia yeye mwenyewe na kuhubiri bila ya malipo wakati inapobidi, hana upendo kwa Mungu ambao ingepaswa awe nao. Watu wengine watafanya kwa sababu ya fedha na hawatafanya kwa ajili ya Mungu. Tunapaswa kwa hiari yetu wenyewe kufanya kila kitu kwa ajili ya Mungu. Kama mchungaji atafikiri kwamba yeye ni muhimu sana katika kufanya kazi au shughuli za kujisaidia mwenyewe, anapaswa akumbuke mfano wa Paulo. Kamwe haijawahi kutokea kuwepo na mmishenari maarufu kuliko Paulo, lakini alikuwa na hiari ya kufanya chochote kile kilichokuwa muhimu kwa ajili ya kukamilisha huduma.

Paulo alisema kwamba alihubiri injili kwa sababu ya wito wa Mungu. Alihubiri kwa sababu hakuna namna nyingine ambayo angeweza kumfurahisha Mungu vinginevyo. Mhubiri analo jukumu maalumu, na atahukumiwa na Mungu kama hatatii (1 Wakorintho 9:16-17).

► Je, ni kitu gani kinatakiwa kiwe ni motisha kwa mchungaji kwa ajili ya huduma yake?

Mtume Petro alisema kwamba mzee wa kanisa ni mchungaji ambaye anapaswa kulichunga kundi la Mungu, na awe mwenye kutaka sana kulisimamia na kulichunga. Lengo lake halipaswi liwe katika kutaka fedha (1 Petro 5:1-2).

Dema alikuwa mtu aliyekuwa akimsaidia Mtume Paulo, lakini baadaye aliachana naye kwa sababu ya kupenda mambo ya ulimwengu huu (2 Timotheo 4:10). Jaribu kufikiria heshima aliyokuwa ameipata Dema kwa kufanya kazi na Paulo kwenye kizazi cha kwanza cha kanisa, lakini bado aliachana na huduma kwa sababu ya kutaka mali. Baadhi ya wachungaji wanapenda mambo ya dunia kuliko wanavyompenda Mungu. Baadhi yao huachana na huduma, lakini wengine hudiriki kuitumia huduma kama njia ya kujipatia mambo ya dunia hii.

Tabia ya waalimu wa mafundisho ya imani potofu ni kwamba wanafanya hivyo kwa ajili ya kujipatia mapato ya fedha (Tito 1:11; 2 Petro 2:3).

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 2 Wakorintho 12:17-18 kwa ajili ya kikundi. Je, tunajifunza nini kuhusiana na Paulo na Tito kutoka katika kifungu hiki?

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Wafilipi 2:19-22 kwa ajili ya kikundi. Je, tunajifunza nini kuhusiana na Timotheo kutoka katika kifungu hiki?

Paulo aliweka mfano wa kutumika kwa sababu ya upendo wake kwa Mungu. Timotheo na Tito walifuata mfano wake (Wafilipi 2:19-22; 2 Wakorintho 12:17-18).

## Uwajibikaji Kifedha

Ni jambo la muhimu sana kuwa na uwajibikaji kwenye mambo ya kifedha katika kanisa la mahali au mtaa. Mtume Paulo aliweka mfano kwa ajili yetu. Alipokuwa akikusanya fedha kutoka katika kanisa moja na kupeleka katika kanisa lingine, aliweka watu wa kushuhudia na akahakikisha kwamba hakuna jambo lolote lililokuwa linafanyika kwa siri (2 Wakorintho 8:20-21).

Watu wa dunia hawawaamini watu wanaoshughulika na utunzaji wa fedha. Wanahisi kwamba watu wengi wanadokoa kutoka katika fedha wanazozitunza. Wanaamini kwamba wachungaji wengi wanatumika tu kwa ajili ya kujipatia mapato ya kifedha. Ni jambo la muhimu sana kwa kanisa la mahali kuwa na mfumo wa uwajibikaji wa kifedha ambao unathibitisha kwamba mchungaji wao anaweza akaaminika.

► Je ni mambo gani ya kufanya ambayo yatalisaidia kanisa kuonyesha kwamba mapato ya sadaka yanatumika kwa uaminifu?

Kwa ajili ya uwajibikaji kifedha, mapato ya sadaka yanapaswa yakusanywe na yahesabiwe na baadhi ya watu kwa pamoja, na siyo mtu mmoja tu. Mtu mwingine tofauti na si mchungaji atapaswa awe akiweka kumbukumbu za jinsi ambavyo fedha zinatumika.

Baadhi ya wachungaji hufundisha kwamba matoleo yote ya zaka ni mali yao. Biblia haijafundisha kwamba zaka yote inapaswa liende kwa mchungaji. Zaka hutumika kwa ajili ya makusudi mbalimbali (Kumbukumbu la Torati 26:12).

Mchungaji atapaswa kusaidia katika kusimamia matumizi ya zaka na sadaka mbalimbali kwa ajili ya kutunza huduma ya kanisa. Kusanyiko la kanisa litakuwa tayari kutoa zaidi kama litaona kwamba kuna uaminifu kwenye matumizi ya sadaka mbalimbali wanazotoa.

## Taarifa Saba kwa Muhtasari

1. Huduma kwenye eneo jipya inapaswa kusisitiza injili na kuwavutia watu walio sahihi.
2. Kanisa lililokomaa siyo tegemezi kwa misaada ya nje au kwa uongozi.
3. Mashirika yanapaswa yasaidie makanisa katika njia ambayo haitadhoofisha msaada kutoka mahali pale pale.
4. Mashirika yanayotoa ufadhili mara nyingi yanakwamisha huduma za kanisa na kusababisha kanisa kuwa tegemezi.
5. Kanisa linapaswa kumtegemeza mchungaji wao ili aweze kutoa muda wake mwingi kwa ajili ya huduma ya kanisa.
6. Kanisa linapaswa liwe na mfumo wa uwajibikaji ambao utathibitisha uaminifu wao.
7. Mchungaji anapaswa kuhamasishwa na upendo wake kwa Mungu na kutaka sana kutumika.

## Kazi za kufanya Somo la 8

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 8. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.
3. Mtihani: Kwenye mwanzo wa kipindi kingine cha darasa, unahitajika kuandika kutoka katika kumbukumbu za ufahamu wako bila kukariri angalau sababu tano kutoka katika sababu sita zinazofanya kanisa liweze kupata msaada wa mahali pale pale na sera nne za kifedha za umisheni.

# Somo la 9
# Zaka

## Utangulizi

Somo linalohusu zaka ni lenye kuelekea kuleta mabishano kwenye maeneo mengine. Watu wengine wanafikiri kwamba wazo la utoaji wa zaka halikubaliani au halipatani na wokovu kwa njia ya imani. Wanasema inaelekea kana kwamba ni malipo kwa ajili ya wokovu. Watu wengine hawataki kujisikia wana jukumu la kutoa msaada kwa kanisa. Wanatoa tu kile wanachojisikia kutoa ili mradi ametoa. Katika somo hili tutaangalia kwenye misingi ya Biblia na makusudi ya vitendo ya zaka.

► Je, ni mambo gani umesikia kutoka kwa watu wakisema sababu zilizo kinyume na utoaji wa zaka?

## Bwana wa Vitu Vyote

Mkristo anaelewa kwamba Mungu ndiye Mmiliki wa kila kitu katika ulimwengu huu. Mungu anatumiliki kama Muumbaji wetu. Alitufinyanga sisi, akatupa uwezo wa aina mbalimbali, na akaumba rasilimali zote tunazotumia. Kila kitu kiliumbwa na yeye, anaendelea kuwepo kwa uwezo wake, na yupo kwa ajili ya utukufu wake (Wakolosai 1:16-17).

Mungu pia anatumiliki kwa njia ya ukombozi. Alilipa gharama kwa ajili ya ukombozi wetu. Alitukomboa sisi kutoka katika hukumu tuliyokuwa tumestahili kwa sababu ya dhambi. Tunawiwa maisha yetu kwake kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yetu (2 Wakorintho 5:14-15).

Mungu pia anatumiliki sisi kwa njia ya wokovu. Kama wenye dhambi tulikuwa chini ya nguvu za Shetani na dhambi. Wokovu unatuondoa sisi kutoka kwenye kongwa la uovu (Matendo 26:18).

Kwa kuwa sisi ni mali ya Mungu, pia kila kitu tulicho nacho ni mali ya Mungu.

► Toa mfano ni kwa jinsi gani unasimamia mali na vitu vyote ulivyopewa kwa ajili ya Mungu.

## Maelekezo Maalumu ya Mungu.

Wakati mwingine Mungu huonyesha umiliki wake wa kila kitu kwa kutoa maelekezo maalumu kwa ajili ya ile sehemu ya kile tulicho nacho. Tunapokuwa tumetii maelekezo ya Mungu katika sehemu hiyo, tunaonyesha kwamba kwa hiari yetu tuko tayari kumtii yeye katika kila jambo.

Kwa mfano, wakati Mungu alipomweka Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni, aliwakataza wasile tunda kutoka katika mti fulani. Maagizo maalumu yaliyokuwa yametolewa yalihitaji udhihirisho wa utiifu.

Mahitaji maalumu ya Mungu yanatupa sisi nafasi ya kudhihirisha utiifu. Kama mtu hayuko tayari kuwa mtiifu kwa maelekezo maalumu ya Mungu kuhusiana na sehemu fulani za maisha yake, inaonyesha kwamba siyo mtiifu kwa maelekezo ya jumla ya Mungu kwa yale mengine yote yaliyoko.

Mwanamke mmoja alilalamika kwa mchungaji wake kwamba hakuwa ameelewa ni kwa nini Mungu alikuwa hambariki. Mchungaji alimwuliza kama alikuwa anamtii Mungu. Yule mama akasema, "Ndiyo, najitahidi kufanya yale ambayo ni sahihi. Sijui jambo lolote ninalofanya tofauti." Mchungaji akamkumbusha kwamba alikuwa hahudhurii ibada. Akasema, "Unaweza usijue Mungu anataka ufanye nini katika baadhi ya siku, lakini ukajua ni nini anachotaka ufanye kwenye siku ya Jumapili. Kama hufanyi kile unachojua kwamba ni sahihi katika siku hiyo, inawezekana humtii Mungu kwenye siku nyingine."

Kuna mifano mingi ya kibiblia ya nyakati ambazo Mungu alitoa maelekezo maalumu kuhusiana na kipengele cha maisha ya mtu. Mungu hutoa zawadi kwa ajili ya kuwa mtiifu na hutoa adhabu kwa kutokuwa mtiifu. Zawadi na adhabu hazikuathiri tu sehemu ya maisha ambayo ilikuwa chini ya mahitaji. Wanayoyachagua na kuamua yalileta madhara kwenye kila sehemu ya maisha yao.

## Mifano ya Maelekezo Maalumu

### (1) Mti uliokuwa umekatazwa katika Bustani ya Edeni

Mungu alikuwa amewaagiza Adamu na Hawa wasile tunda la mti fulani. Walibarikiwa na kuishi katika uwepo wa Mungu, mpaka pale walipoacha kutii. Wakati walipokiuka katazo la kutokula kutoka katika mti mmoja, Walipoteza uhuru wa kuwepo tena ndani ya Edeni, wakavunja uhusiano wao na Mungu, na wakaleta laana kwa wanadamu wote (Mwanzo 3:17-19).

### (2) Siku ya Sabato

Mungu alikuwa ametoa makatazo kadhaa kuhusiana na Siku ya Sabato. Mtu ambaye hakuweza kutii maelekezo ya Mungu kuhusiana na siku hiyo alikuwa pia siyo mtiifu kwa siku nyingine zilizokuwepo. Kukosa utiifu kulileta laana kutoka kwa Mungu kwenye kila sehemu ya maisha (Isaya 58:13).

### (3) Yeriko

Yeriko ulikuwa ni mji wa kwanza uliokuwa umeharibiwa na Israeli wakati wa kuingia kwenye Nchi ya Ahadi. Mungu aliwaambia kwamba kila kitu kitakachokuwa kimechukuliwa kutoka katika mji wa Yeriko kitengwe kwa ajili ya Mungu. Miji mingine haikuwa na hitaji hili, lakini Mungu alitoa maagizo maalumu kwa ajili ya Yeriko. Kutokutii kulisababisha kushindwa katika vita, kifo cha watu thelathini na sita na kifo cha familia moja (Yoshua 7:5).

**(4) Sauli na Amaleki**

Mungu alimwambia mfalme Sauli wa Israeli kulipiga na kuliharibu taifa la Amaleki na kuwauwa watu na wanyama wote waliokuweko. Sauli aliwaacha wengine wakiwa hai. Alijinadi kwamba alikuwa amemtii Mungu, ingawaje hakuwa ameitii amri iliyokuwa maalumu. Mungu alimkataa Sauli kuendelea kuwa mfalme (1 Samweli 15:3, 9, 20-23).

**(5) Sabato za Ardhi**

Ardhi ilikuwa inatakiwa ipumzishwe katika kila mwaka wa saba. Watu walikataa kumtii Mungu na hawakuzingatia kuitimiza Sabato kwa ajili ya ardhi. Kama mkulima hakuweza kumtii Mungu kwenye mwaka wa saba, inawezekana hakuwa anamtii Mungu kwenye miaka mingine. Wakati watu walipokataa kutii, Mungu aliruhusu waipoteze ardhi yao kabisa. Sabato za ardhi zilitekelezwa kwa miaka sabini ya kukaa utumwani (2 Mambo ya Nyakati 36:21).

**(6) Mazao ya Kwanza**

Waisraeli walipaswa wampe Mungu mazao ya kwanza ya ardhi. Kama wangetii, Mungu alibariki mavuno ya mashamba yao (Mithali 3:9-10). Baraka hiyo haikuwa tu kwa ajili ya ile sehemu waliyotoa, bali kwa ajili ya mazao yote. Kama hawakuweza kutimiza hili hitaji, ardhi haikubarikiwa. Kama mtu hatatoa sehemu ya kile ambacho Mungu anakitaka, hata kwenye sehemu nyingine pia hamtii Mungu.

**(7) Zaka**

Mungu anaamuru kila sehemu ya kumi itolewe. Kama mtu hatatoa, anaonyesha kwamba fedha yake hajaikabidhi kwa Mungu. Aidha pia hatumii asilimia tisini zilizoko kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Mungu atabariki vyote alivyo navyo kwa mtu anayetoa zaka (Malaki 3:10). Kama mtu hatatoa kwa ajili ya kuwezesha huduma, vitu vyote alivyo navyo vitakuwa vimelaaniwa (Hagai 1:6).

Mmiliki wa duka aliondoka akasafiri. Kabla ya kuondoka, alimwambia mfanyakazi wake, "Angalia hili duka na uhakikishe unalifanyia usafi na kusafisha sakafu yake." wakati aliporudi, sakafu ilikuwa haijafanyiwa usafi. Mfanyakazi akasema, "Nililiangalia duka kwa ajili yako." Mwenye duka akasema, "Kwa kuwa hukufanya lile maalumu nililokuwa nimekuagaiza, ninajua kwamba katika kazi zako zote ulijifurahisha mwenyewe tu badala ya kunifurahisha mimi."

► Je, ni kwa jinsi gani mtu anaweza kuonyesha kwamba anamtii Mungu?

## Makusudi ya Asili ya Utoaji wa Zaka

► Je, zaka ilikuwa inatumika kwa ajili ya nini?

Huduma ya kikuhani ya wakati wa Agano la Kale ilikuwa inawezeshwa kwa njia ya utoaji wa zaka (Hesabu 18:20-21). Walawi ambao walikuwa ni kabila lililokuwa na makuhani, hawakupewa urithi wa ardhi (Kumbukumbu la Torati 18:1-4). Walikuwa wanawezeshwa kifedha kwa ajili ya huduma zao ndani ya hekalu. Mpango wa Mungu kwa ajili ya Walawi ulikuwa ni waweze kujielekeza tu kwenye huduma na siyo kujihusisha na mambo ya biashara.

Zaka lilitumika katika kuwezesha ibada ya hekalu na wale wote ambao walikuwa wanahusika kwa ajili ya ibada hiyo. Zaka lilitumika pia kwa ajili ya sikukuu za jamii zilizohusika na ibada, ambazo maskini walikaribishwa (Kumbukumbu la Torati 12:17-18, Kumbukumbu la Torati 14:22-29). Zaka lilitumika katika kusaidia watu waliokuwa maskini, wajane, yatima na wageni wote waliofika malangoni kwao (Kumbukumbu la Torati 26:12).

► Je, ni tofauti gani unazoziona kwenye matumizi ya zaka kwa wakati wa sasa?

Baada ya kujua kwamba wametoa zaka zao kwa uaminifu, watu wa Israeli walikuwa wanaweza kuomba kwa ajili ya baraka za Mungu. (Kumbukumbu la Torati 26:12-15). Kukataa au kuacha kutoa zaka ni kumwibia Mungu, lakini kutoa zaka kwa ajili ya "Ghala la Yesu" kutaleta baraka zisizoweza kuondosheka (Malaki 3:8-10).

► Je, utawezaje kusema kwa mtu ambaye anajinadi kwamba yeye ni maskini sana na hawezi kutoa zaka?

## Umuhimu wa Utoaji wa Zaka kwa Wakati wa Sasa

Baadhi ya watu Wanasema kwamba utoaji wa zaka ulikuwa ni mfumo tu kwa ajili ya wakati wa Agano la Kale.

► Je, kuna sababu zozote za kuamini kwamba mfumo wa utoaji wa zaka haukuwa hitaji la muda mfupi la Agano la Kale?

### (1) Ibrahimu

Ibrahimu alitoa zaka kwa Melkizedeki muda sana hata kabla ya Kutolewa kwa sheria ya Musa kwa ajili ya Israeli. Hii inaonyesha kwamba ilikuwa ni kanuni ya ujumla kabla ya Musa. Utoaji wa zaka haukuanza na sheria ya Agano la Kale, bali ilikuwa ni kanuni iliyokuwepo tangu mwanzo (Mwanzo 14:20; Waebrania 7:4).

### (2) Yakobo

Yakobo aliahidi kumtolea Mungu zaka (Mwanzo 28:20-22), ingawaje sheria ya Musa ilikuwa bado haijatolewa. Yakobo alijua kwamba tayari ilikuwa ni kanuni iliyokuwepo kwa ajili ya kumtolea Mungu.

**(3) Yesu**

Yesu aliithibitisha kuhusu utoaji wa zaka na hakusema kwamba ilikuwa ni kwa ajili ya wakati uliopita tu (Mathayo 23:23).

**(4) Paulo**

Paulo aliwaambia waumini wa kanisa wawe wanatoa "kwenye kila siku ya kwanza ya juma" kwa kadri ya kufanikiwa kwao (1 Wakorintho 16:2). Kwa hiyo, walikuwa wanatakiwa kutoa kiwango kilichokuwa kinalingana na jinsi walivyokuwa wakipokea au wakipata. Mwongozo wa Agano la Kale wa asilimia kumi (10%) unaonyesha kile ambacho Mungu aliona kwamba kilikuwa ni kiwango sawa cha uwiano kinachotakiwa kitolewe. Hakuna sababu ya kufikiria kwamba mawazo ya Mungu yamebadilika.

> "Na sasa wakati mwingine tunasikia mtu akisema kwa mshangao, 'Mtu yule anatoa zaka!' Ni kwa jinsi gani jambo hili ni fedheha, niliuliza, kwamba kile ambacho miongoni mwa Wayahudi hakikuwa ni jambo la mshangao au la umashuhuri sasa limekuja kuwa ni jambo la mshangao miongoni mwa Wakristo? Kama ingelikuwa ni jambo la hatari kushindwa kutoa zaka kwa wakati ule, basi, kwa uhakika ni hatari zaidi kwa sasa."
>
> \- John Chrysostom
> *Mahubiri kuhusu Waefeso*
> (Yaliandikwa kabla ya 400 B.K.)

**(5) Wakati wa sasa.**

Mungu bado anao mpango kwa ajili ya wale wanaotumika kwenye huduma kwa muda wao wote waweze kuwezeshwa kifedha na huduma zao. "Wale wanaohubiri injili wanapaswa waishi kutokana na injili." Mungu hajawahi kupanga wachungaji wafanye kazi na wajiwezeshe wenyewe na wasiwe na muda wa kuwajibika kwa ukamilifu kwenye huduma zao. Katika 1 Wakorintho 9:11-14 tunaambiwa kwamba mtu anayepanda vitu vya rohoni anapaswa kuvuna kifedha kutoka kwa wale anaowahudumia. Katika 2 Wakorintho 12:13 tunaonyeshwa kwamba makanisa kwa kawaida yalimwezesha Paulo kifedha wakati alipokuwa akiyahudumia.

## Sera za Kanisa

Utoaji wa zaka unapaswa utokane na wale walio waumini kamili wa kanisa. Kanisa halipaswi kufundisha kuhusu utoaji wa zaka kwa watu ambao hawajaokoka.

> "Zaka inapaswa lilipwe bila ya kujali nafasi aliyo nayo mtu."
>
> \- Augustine

Mtu anayehudhuria kanisani kwa mara ya kwanza kamwe hapaswi kujisikia kwamba yeye anawajibika kutoa fedha kwa ajili ya kanisa.

Kanisa halipaswi lijaribu kukusanya zaka kutoka kwa watu ambao wamelitembelea kanisa na bado hawajajikabidhi kuwa wanachama kamili wa kanisa.

Kanisa linapaswa lihakikishe kuwa watu hawafikiri kwamba utoaji wa zaka ni sehemu ya wokovu. Hakuna mtu yeyote anayepaswa kufikiri kwamba zaka litamsaidia mtu kupata wokovu.

Kanisa linapaswa litoe huduma kwa kusanyiko na kwenye jumuiya waliyomo bila ya kudai malipo.

Waumini wote wa kanisa wanapaswa kujua ni kwa jinsi gani fedha za kanisa zinatumika. Kanisa linatakiwa lifuate hatua zilizo makini za utunzaji wa fedha ili kwamba kila mtu aweze kufahamu ni kitu gani kinachofanyika kwa uaminifu.

Zaka siyo mali ya mchungaji peke yake. Zaka inapaswa iwezeshe huduma za kanisa. Hata hivyo, kumwezesha mchungaji kunatakiwa kuwe ni kipaumbele cha kanisa.

**Taarifa Saba kwa Muhtasari**

1. Mungu ndiye mmiliki wetu pamoja na vitu vyote tulivyo navyo.
2. Zaka ni uwajibikaji kamili kwa kanisa na Mungu kwa pamoja.
3. Mtu ambaye hayuko tayari kutoa zaka kwa ujumla hamtii Mungu kwa fedha zake.
4. Zaka siyo malipo ya wokovu.
5. Zaka ni mpango wa Mungu wa kuwezesha huduma ya kanisa.
6. Mungu hubariki utoaji wa zaka na utoaji wa dhabihu.
7. Zaka ni uwajibikaji wetu wa kumaanisha katika kumtegemea Mungu na utoaji wake.

**Kazi za kufanya Somo la 9**

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 9. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.
3. Masailiano: Wahoji baadhi ya waumini wa kanisa lako kama huwa wanatoa zaka, na ni kwa nini wanatoa au hawatoi. Andika muhtasari unaohusiana na mahojiano hayo.

# Somo la 10
# Ubatizo

## Mwanzo wa Desturi ya Ubatizaji

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Mathayo 3:1-12 kwa ajili ya kikundi.

Kwenye Agano Jipya, tunatambulishwa dhana ya ubatizo kupitia huduma ya Yohana Mbatizaji. Hata hivyo, Yohana hakuanzisha ubatizo. Mafarisayo waliwabatiza Mataifa walioamini na kuingia katika Uyahudi. Mafarisayo Hawakuwabatiza Wayahudi, kwa sababu walichukulia kwamba Wayahudi tayari walikuwa ni watu wa Mungu. Yohana alitekeleza kwa jinsi ya tofauti kabisa desturi hii kwa sababu yeye aliwabatiza Wayahudi.

► Je, Yohana alimkataa nani kwenye ubatizo? Kwa nini? Hali hiyo inatufahamisha nini kuhusiana na hitaji la ubatizo?

Baadhi ya Mafarisayo walijitokeza ili wabatizwe na Yohana, lakini Yohana aliwakataza kwa sababu walikuwa hawajatubu.

Mafarisayo walidhania kwamba wao hawakuwa na hitaji la kutubu na kupata msamaha kwa sababu walikuwa Wayahudi. Yohana aliwataka waelewe kwamba watu halisi wa Mungu ni wale wanaompenda na kumtumikia yeye. Watu wanaojinadi kuwa wao ni watu wa Mungu kwa sababu ya kuzaliwa kama Wayahudi ni kama miti ya matunda ambayo haizalishi matunda. Mungu aliwakataza.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Yohana 3:22-23 na Yohana 4:1-2 kwa ajili ya kikundi.

Ni dhahiri kwamba Yesu alisisitiza kuhusu ubatizo katika huduma yake. Yesu mwenyewe hakubatiza, lakini aliikabidhi jukumu hilo kwa wanafunzi wake. Walibatiza watu wengi kuliko hata ilivyokuwa kwa Yohana.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Mathayo 28:18-20 kwa ajili ya kikundi.

Mwishoni mwa huduma ya Yesu hapa duniani aliwaagiza wanafunzi wake waende mahali popote duniani wakawafanye watu kuwa wanafunzi. Aliwaagiza wabatize.

Tunajua kwamba agizo hili halikuwa tu kwa ajili ya mitume, kwa sababu huduma ya umisheni itachukua karne nyingi kumalizika. Yesu alitoa ahadi kwamba atakuwa pamoja nao "hadi mwisho," hii ikionyesha kwamba hili agizo na ahadi hii ni kwa ajili ya kanisa katika vizazi vyote.

Tunaona kutoka katika nyaraka za Agano Jipya kwamba kanisa la karne ya kwanza lilitii agizo hili neno kwa neno (Matendo 2:38, Matendo 8:38).

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 1:12-17 kwa ajili ya kikundi. Kwa nini Paulo alifurahia kwamba yeye mwenyewe hakubatiza watu wengi katika Korintho?

Ubatizo uliwakilisha kuingia kwenye kanisa. Kanisa la Korintho lilikuwa limegawanyika na waumini wake wanachama walikuwa wanafuata viongozi mbalimbali. Paulo anawakumbusha kwamba ubatizo hauna maana kwamba watu wanafanyika kuwa ni wafuasi wa mtu fulani; bali inamaanisha kwamba wanafanyika kuwa ni wafuasi wa Kristo. Alikuwa amefurahia kwamba yeye mwenyewe hakuwa amebatiza watu wengi miongoni mwao, ili kwamba hakuna mtu yeyote atakayefikiria kwamba alikuwa anawataka wawe wafuasi wake binafsi. Kipaumbele cha Paulo kilikuwa ni kuhubiri injili.

► Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusiana na zoezi la kawaida la ubatizo kwenye kanisa la mwanzo?

Kifungu hiki kinatuambia kwamba kanisa la mwanzo lilibatiza waumini kila mahali. Walikuwa wanafuata agizo la Yesu. Ubatizo haukuwa tu kwa ajili ya watu katika Israeli. Haikuwa ni desturi ya muda mfupi tu. Ilifanyika kila mahali ambapo injili ilikwenda.

Tangu mwanzo, kanisa limekuwa likifanya huduma ya ubatizo kama ushuhuda katika jamii au kwa jamii hadharani kwamba mwenye dhambi ametubu na ameingia kwenye ushirika wa watu walioamini.

> "Ubatizo wa Kikristo ni sakramenti inayoandamana na ibada za kidini kuashiria kukubalika kwa faida zinazotokana na kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo, na ahadi iliyo na kusudio kamili la utiifu katika utakatifu na haki."
>
> - Wiley & Culbertson, *Introduction to Christian Theology*

Kwa watu wengi, ubatizo siyo katika wakati ambapo wanafanyika kuwa Wakristo. Mwenye dhambi anayetubu anakuwa ameokoka na wakati huo yeye mwenyewe akiwa ameiweka imani yake kwa Kristo. Baada ya kuwa ameokoka, anapaswa aheshimu na kutii agizo la kubatizwa kama udhihirisho wa maisha yake mapya ya utiifu kwa Yesu kama Bwana na Mwokozi. Kuna watu ambao ni tofauti, kwa sababu ilikuwa wakati wa ubatizo ni kwamba waliiweka imani yao katika Kristo na uzoefu wa kuokoka. Lakini, kwa kawaida, ubatizo ni ushuhuda kwamba wokovu tayari umeshatokea.

► Je, utamwambia nini mtu anayesema kwamba alifanyika Mkristo wakati alipobatizwa?

### Kosa la Kuepuka: Kufikiri kwamba Ubatizo ni sehemu ya Wokovu

Baadhi ya watu wanatafsiri aya kadhaa za Maandiko kumaanisha kwamba ubatizo ni sehemu ya wokovu. Wanaamini kwamba mtu huwa hajaokoka kabisa hadi atakapokuwa ameokoka. Anania alimwambia Sauli, "Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako" (Matendo 22:16). Hata hivyo, dhambi zetu huwa zinaoshwa kwa damu ya Kristo (1 Yohana 1:7). Utakasaji wa kutumia maji unaweza tu kuwakilisha uhalisia wa kiroho. Anania alikuwa anamwambia Sauli kwamba anapaswa afanye udhihirisho wa kimwili wa hatua ya imani. Ubatizo ulikuwa ni ushuhuda kwamba dhambi zake zimeondolewa kabisa.

Katika Waebrania 10:22, tunaambiwa kwamba waumini wanapaswa wamkaribie Mungu "hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi." Inawezekana maji yanarejelewa kuwa ni ubatizo. Hiyo siyo uhakika kabisa. Hata hivyo, hata kama inarejelea kuwa ni ubatizo, aya haijasema kwamba ubatizo unatuokoa. Inasema tu kwamba tunapaswa tutii agizo la Mungu la kubatizwa.

Katika Yohana 3:5 Yesu alimwambia Nikodemo kwamba mtu anapaswa "azaliwe kwa maji na kwa roho." Taarifa hii inafuatia taarifa yake kwamba mtu anapaswa azaliwe tena kwa mara nyingine, jambo ambalo lilimchanganya Nikodemo. Nikodemo alikuwa akifikiria kuzaliwa kunakofanyika kimwili. Yesu alikuwa akisema kwamba mtu ni lazima azaliwe siyo tu kimwili, bali pia kiroho, ili kuweza kuingia kwenye ufalme wa mbinguni. "Kuzaliwa kwa maji" ndiko kuzaliwa kimwili.

## Ubatizo ni katika Kumtii Kristo

Ubatizo siyo kazi ambayo mtu anaifanya ili kukidhi sifa ya wokovu au kupata wokovu. Baadhi ya watu hufundisha kwamba kwa kuwa ubatizo siyo kazi ambayo inaleta wokovu, hatupaswi tuutekeleze. Wana wasiwasi kwamba watu watafanya waweke imani yao kwenye ubatizo badala ya kutegemea neema iliyotolewa katika upatanisho. Hata hivyo, agizo lolote linalotokana na Kristo tunapaswa kulitii, na hatupaswi kufikiri kwamba utiifu wetu katika maagizo ya Mungu ndio unaotuletea wokovu wetu.

## Ubatizo kama Njia ya Neema

Ubatizo unaweza ukaitwa ni njia ya kupokea neema. Hiyo haimaanishi kwamba unatuokoa sisi, au kwamba kitendo hicho moja kwa moja kinatupa neema. Kama mtu akibatizwa bila ya kuwa na imani, ubatizo huo hauna thamani yeyote. Ubatizo ni njia ya neema kwa sababu ni kitendo ambacho Mungu alikitengeneza kwa ajili yetu. Tunapokifanya kitendo hiki kwa utiifu na kwa imani, Roho wa Mungu hufanya kazi ndani ya mioyo yetu katika kutuweka kwenye maisha ya Kikristo.

► Je, ni kwa nini tubatizwe?

## Ishara ya Kitheolojia

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 6:3-11 kwa ajili ya kikundi. Je, ubatizo unaashiria nini kwa mujibu wa kifungu hiki cha Maandiko?

Biblia inatuambia kwamba ubatizo ni ishara ya kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu. Wakati mtu aliyeamini anapobatizwa anashuhudia kwamba anajiungamanisha na upatanisho uliotolewa na Kristo. Mtume aliweza hata kutumia tamko kwamba sisi sote "tuliobatizwa katika Kristo."

Katika wokovu, tunapokea faida za kifo cha Yesu; lakini, katika ufahamu wa kipekee, tunashiriki pia katika mauti yake. Yesu alikufa kwa sababu ya dhambi zetu, na siyo kwa sababu ya dhambi zake, bali dhambi za dunia. Vivyo hivyo, katika wokovu tunakufa kwa dhambi, kwa sababu tunatubu na kugeuka mbali na dhambi.

Somo lililoko katika Warumi 6 ni ushindi juu ya dhambi. Halirejelei tu kwenye msamaha. Ni wazi kwamba mtu aliyeamini anapaswa kuwa huru kutokana na utawala wa dhambi (12-14) na siyo kuendelea katika dhambi (1).

Kwenye wokovu tunashirikishana katika kufufuka kwa Yesu. Kama vile alivyotoka kutoka kwa wafu, na sisi tunaanza maisha mapya tunapokufa kwa dhambi. Tunaanza maisha ya ushindi na uhuru kutoka katika dhambi.

### Suala la kuhusiana na Aina ya Ubatizo

Swali linalohusu aina ya ubatizo ni hili: je, mtu aliyeamini abatizwe kwa kuzamishwa ndani ya maji, kwa kumiminiwa maji au kwa kunyunyiziwa maji?

Wengi wa Wakristo wengi katika dunia hii ambao wanafanya ubatizo wa watu walioamini wanafanya ubatizo kwa kuzamisha ndani ya maji.

Kuna sababu kadhaa ambazo Wakristo wengi huamini kwamba ubatizo kwa kuzamisha ndio njia iliyo sahihi.

1. Neno *batiza* (*baptize au baptizo)* linatokana na neno la Kiyunani linalomaanisha kuzamisha au kutumbukiza ndani ya maji
2. Ubatizo unaashiria kifo cha Yesu, kuzikwa na kufufuka kwake, ambako kunaashiriwa na tendo la kuzamishwa au kutumbukizwa ndani ya maji (Warumi 6:3-5).
3. Ndani ya Biblia, watu walikwenda kwenye maeneo yenye maji wakaingia ndani yake kwa ajili ya kubatizwa (Marko 1:10, Matendo 8:38).
4. Kanisa la mwanzo lilifanya ubatizo kwa njia ya kuzamisha ndani ya maji isipokuwa tu pale ambapo ilikuwa haiwezekani kwa sababu ya afya mbaya ya mtu au ukosefu wa maji. *Didache*, ulikuwa ni muhtasari wa mafundisho ya mitume ulioandikwa karibu mwaka wa 70 B.K., ukisema kwamba mtu aliyeamini anaweza kubatizwa kwa maji ya kumiminiwa endapo maji mengi yatakuwa hayapatikani.

> "Neema tunayoihitaji haiko katika maji, bali iko katika kazi ya Roho Mtakatifu ambayo matumizi yake katika ubatizo yanaashiria; si katika mkate na divai, bali katika upatanisho ambao matumizi yake ya kisakramenti yanamaanisha."
>
> \- John Miley,
> *Systematic Theology*

Kwa ajili ya sababu hizi, Wakristo wengi wanaamini kwamba aina ya ubatizo wa kuzamishwa ndani ya maji ndio wa kibiblia na wa kihistoria.

Baadhi ya Wakristo wanaamini kwamba aina nyingine ya ubatizaji ni wa kimaandiko. Agano la Kale linaelezea sherehe mbalimbali za unyunyizwaji wa maji kuashiria kwamba ni uwakilishwaji wa utakaso. Pia Agano Jipya linarejelea kwenye unyunyizwaji wa damu. Kwa kuwa unyunyizwaji wa damu inaweza ikawa ni ishara ya upatanisho, ubatizo kwa kunyunyiza pia ungeweza kuashiria upatanisho (Kwa ajili ya kurejelea kuhusu kunyunyiziwa

ona Kutoka 24:8; Waebrania 9:19-20, Waebrania 10:22, Waebrania 12:22-24; Hesabu 8:6-7; Isaya 52:15; Ezekieli 36:25; na 1 Petro 1:2.)

Kwa kuwa kamwe Biblia haitoi taarifa ya uhakika ya njia gani ya ubatizo inavyotakiwa itumike, tunapaswa tuwe wavumilivu kwa Wakristo ambao wana mtazamo na au maoni tofauti kuhusiana na jambo hili.

**Suala la Ubatizo wa Watoto Wadogo**

Kanisa ni jumuiya ya wanaoishi kwa imani kwenye agano na Mungu. Wakati mwenye dhambi anapotubu na kujiunga na jumuiya ya imani, ubatizo unakuwa ni ushuhuda wa nje wa kuokoka kwake.

Lakini inakuwaje kwa mtoto mdogo aliyezaliwa na wazazi wa Kikristo walioko katika kanisa? Mtoto ni sehemu ya jumuiya ya imani. Mtoto mdogo anakubalika na Mungu hadi pale atakapokuwa amekua ya kutosha katika kuweza kuchukua maamuzi yake mwenyewe ya kuokoka.

Baadhi ya makanisa yanaamini kwamba mtoto mdogo anapaswa kubatizwa kama ishara kwamba yuko kwenye jumuia ya imani. Kama mtoto atakapokuwa na umri wa utu uzima na akakubaliana na mafundisho ya imani ya kanisa, makanisa haya hufanya sherehe wanazoziita "ubarikio." Baadhi ya makanisa hawachukulii maanani kwamba kuokoka ni muhimu kwa sababu mtoto alizaliwa katika mazingira ya kanisa na kukubali kile alichokuwa anafundishwa (Mifano halisi ni Wakatoliki, Walutheri, na Kanisa la Uingereza.) Makanisa mengine yanayobatiza watoto wadogo yanaamini kwamba kuokoka ni muhimu (Kwa mfano, Wamethodisti wa mwanzo waliokuwa wakiongozwa na John Wesley waliamini kwamba kuokoka ni muhimu hata kwa mtu ambaye alibatizwa wakati akiwa mtoto.)

Baadhi wanaamini kwamba kutahiriwa kulitimiza kusudi linalofanana katika Agano la Kale. Mtoto alikuwa anatahiriwa ili kuonyesha ishara kwamba alikuwa kwenye agano. Alikuwa hangojei hadi awe mzee kamili ili kuelewa agano lilikuwa linamaanisha kitu gani.

Inaelekea Kanisa la mwanzo lilikuwa linafanya ubatizo wa watoto wadogo. Hippolista aliandika kuhusu mila ya kitume katika mwaka wa 212 B.K. na akasema kwamba watoto wanapaswa wabatizwe; na, kama ni watoto sana wasioweza kuzungumza wenyewe, wazazi wao wanaweza wakawasemea. Origen aliandika katika mwaka wa 248 B.K. kwamba mitume walikuwa wakifanya ubatizo wa watoto wadogo. Augustine aliandika katika mwaka 400 B.K. kwamba ubatizo wa mtoto mdogo alikuwa ukifanyika katika kanisa lote tangu wakati wa mitume na kwamba kamwe alikuwa hajawahi kusikia mtu yeyote akipinga au kukataa ubatizo wa watoto wadogo.

Kwenye kitabu cha Matendo, wakati mwingine mitume walibatiza familia nzima (Matendo 11:14, Matendo 16:15, 33). Tunaweza tukasadiki kwamba pia walibatiza watoto wadogo.

**Vipingamizi vya Ubatizo wa Watoto Wadogo**

1. Kwenye Agano Jipya, watu walioamini walikuwa wakibatizwa baada ya kupata ushuhuda wa imani. Walikuwa ni watu ambao walikuwa wametubu na wakaiamini injili. Hakuna maelekezo ya kubatizwa watoto wadogo.

2. Ubatizo wa watoto wadogo hauwezi kutimiza kusudi la asili la utoaji ushuhuda kwamba mwamini alikufa dhambini na anaishi kwa ajili ya Mungu.

3. Matokeo ya kihistoria ya ubatizo wa watoto katika maeneo mengi yamekuwa ni kutengeneza mikusanyiko ya watu ambao hawajaokoka na wanaofikiri kwamba wao ni Wakristo kamili.

Badala ya kubatiza watoto wadogo, baadhi ya makanisa yana sherehe kwa ajili ya watoto wadogo wanazoziita “Kuweka Wakfu.” Kwenye sherehe hiyo, wazazi huwaweka wakfu watoto kwa Mungu na kuahidi kuwakuza kwenye mafunzo ya Ukristo. Kwenye makanisa hayo, ubatizo haufanyiki hadi pale mtoto atakapokuwa amekuwa mkubwa wa kutosha kuelewa kuhusu kutubu na imani.

Wanapohubiriwa watu ambao walibatizwa wakiwa watoto, haina umuhimu wa kutia fedheha ubatizo wao. Badala yake, hubiri kwamba mtu hawezi kuwa ameokoka pasipokuwepo na kutubu dhambi na imani inayookoa. Kama mtu anaishi katika dhambi, ubatizo wake hautakuwa ni sababu ya kufikiri kwamba yeye ni Mkristo.

## Suala la Muda

► Je, ni kwa muda gani kanisa litasubiri ili kumbatiza mtu mpya aliyeamini?

Kwenye Agano Jipya, watu wapya waliokuwa wameamini walikuwa wanabatizwa haraka bila ya kupoteza muda. Ubatizo haukuwakilisha kiwango cha ukomavu au ufahamu wa mtu.

Baadhi ya makanisa wanawataka watu wapya walioamini kuwa katika kipindi cha muda cha mafundisho na ukuaji wa Kikristo kabla ya kufikia hatua ya kubatizwa. Wanataka kuhakikisha kwamba watu wapya walioamini wanakuwa mifano bora ya Wakristo. Wanataka kuwaona wakiishi maisha ya Kikristo kwanza kwa muda fulani kwa kuwa wengine wataweza kuanguka kutoka katika wokovu baada ya kuwa wamekwisha kubatizwa.

Ubatizo ni ushuhuda kwamba mtu aliyebatizwa ameokoka. Siyo taarifa ya kukua kiroho au ufahamu. Kwa hiyo, ubatizo unatakiwa ufanyike mara tu mtu mpya anapokuwa ameamini au ameokoka. Kungojea kunamaanisha kwamba hatuna uhakika kama mtu husika kweli ameokoka. Inaonyesha kuna mashaka kwenye ushuhuda wake, jambo ambalo linaweza kumsababisha awe mdhoofu katika imani yake mwenyewe.

Ubatizo pia ni njia ya neema, kwa sababu jinsi mtu anapokuwa mtiifu katika imani na kulifanya tendo hili liwe udhihirisho kwa watu wote, Mungu humwezesha kuanza kwa neema. Kama tutamfanya mtu mpya aliyeamini awe mtu wa kusubiri wakati wa kuja

kubatizwa wakati mwingine, tunamweka mbali na kuupata huu msaada katika wakati ambapo alikuwa anauhitaji sana kuliko kitu kingine.

Kama inaelekea kwamba mtu haonyeshi kuwa na uelewa wa injili na haonyeshi mabadiliko kwa njia ya neema, hapaswi kubatizwa. Kama atakuwa anazo hizo sifa, anatakiwa abatizwe haraka kama njia ya kuimarisha imani yake.

### Suala la Ubatizo Uliocheleweshwa

Wakati mwingine watu wanaojinadi kwamba wao ni Wakristo hutaka kuchelewesha ubatizo wao. Husema kwamba wameiamini injili na kutubu, lakini bado hawajahitaji kubatizwa. Wakati mwingine huchelewesha hata kwa miaka. Wakati mwingine watu wanasubiri hadi wanakufa.

Kama mtu anakuwa hayuko tayari kubatizwa kwa hiari, mara nyingi kunatokea kuwepo na jambo lililounganishwa na ubatizo ambalo hayuko tayari kulifanya. Inawezekana hapendi kufunganishwa kabisa na kanisa. Inawezekana kuna dhambi ambayo kiuhalisia hajaiacha bado. Inawezekana hapendelei kufanya ushuhuda wa wazi kwa watu kwamba yeye ni Mkristo.

Kama kweli atakuwa ameokoka, mtu huwa ni Mkristo kabla ya kubatizwa. Hahitaji ubatizo ili uweze kumfanya awe Mkristo. Hata hivyo, kama yeye binafsi hana hiari ya kutubu dhambi kabisa na kumshuhudia Kristo, bado yeye anakuwa siyo Mkristo.

► Je, utasemaje kwa mtu anayesema kwamba yeye ni Mkristo lakini hapendi kubatizwa?

### Suala la Jina

► Je, mchungaji anapaswa aseme nini wakati anapokuwa anambatiza mtu mpya aiyeamini?

Wakati Yesu alipowapa mitume Agizo Kuu, aliwaambia wabatize "kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu" (Mathayo 28:19).

Kubatizwa "kwa jina la" Utatu Mtakatifu wa Mungu ilikuwa na maana ya kubatizwa chini ya mamlaka yao. Yesu alitumia neno *jina* sawa sawa na wakati aliposema hakuja kwa jina lake mwenyewe (Yohana 5:43).

Baadhi ya makanisa yanaamini kwamba mchungaji anayefanya tendo la ubatizo anapaswa aseme, "Ninakubatiza wewe kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu." Makanisa mengine yanaamini kwamba njia iliyo sahihi zaidi ya ubatizaji chini ya mamlaka ya Nafsi tatu za Utatu Mtakatifu ni kusema, "Nakubatiza wewe kwa Jina la Yesu."

Kwenye Agano Jipya, tunapata huko mifano kadhaa yenye maelekezo ya kubatiza, na maneno yanatofautiana na maneno ya Yesu aliyoyatumia wakati alipowapa mitume wake Agizo Kuu. Kwenye siku ya Pentekoste, Petro aliwaambia watu wapya waliokuwa wameamini, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo" (Matendo 2:38). Paulo aliwabatiza watu wapya walioamini katika Efeso kwa jina la Yesu (Matendo 19:5). Petro aliwaambia watu wapya walioamini kwenye nyumba ya Kornelio, "wabatizwe kwa jina

la Bwana Yesu" (Matendo 10:48). Paulo alionyesha kwamba waumini wapya katika Korintho walibatizwa kwa Jina la Yesu (1 Wakorintho 1:12-13).

Kwenye kitabu cha Matendo, ubatizaji kwa Jina la Yesu ulionyesha utofauti uliokuwepo kutokana na ubatizo wa Yohana (ambao pia umetajwa mara saba kwenye kitabu cha matendo) na aina za ubatizo wa dini nyingine.

Inaonekana kwamba njia iliyotumiwa na kanisa kukamilisha agizo la Yesu ilikuwa ni kuweka msisitizo wa jina la Yesu kwenye ubatizo. Kuna uwezekano kwamba mchungaji aliyekuwa akifanya tendo la ubatizo kwenye kanisa la karne ya kwanza alikuwa akisema, "Nakubatiza wewe kwa jina la Yesu." Kwenye miaka ya mwanzo ya kanisa, imani katika Yesu ilikuwa ndio suala lililokuwa kubwa. Kama mtu aliweza kuamini katika Yesu, alifanyika kuwa Mkristo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa historia ya kanisa la mwanzo sana, kanisa lilitilia mkazo Utatu Mtakatifu wakati wa ubatizo. Ndani ya kizazi cha kwanza cha kanisa, kulikuwa na watu waliosema kwamba walimwamini Yesu, lakini hawakuwa wanaamini mambo ya kweli kuhusiana na Mungu. Andiko la *Didache* linasema kwamba watu wapya walioamini wanapaswa kuzamishwa mara tatu ndani ya maji kukiwa na kanuni za imani kwa kila nafsi ya Utatu Mtakatifu. Waandishi wengine, kwenye mwaka wa 248 B.K au kabla ya hapo, waliandika kwamba utaratibu wa kawaida wa kanisa ilikuwa ni kutaja Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wakati wa ubatizo (Hippolita, Origen, Tertullian, na wengine).

Tatizo la wakati wa sasa ni kwamba baadhi ya vikundi vya dini au madhehebu vinakataa uwepo wa Utatu Mtakatifu wa Mungu. Wanasema kwamba wanaamini katika Yesu, lakini hawaamini kwamba Yesu ni nafsi inayotofautiana na Baba na Roho Mtakatifu. Wanabatiza kwa jina la Yesu kwa sababu wanaamini kwamba jina hilo Yesu ndilo jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Wanaamini kwamba nafsi zote tatu ziko ndani ya mtu mmoja. Mfano mmojawapo wa kundi linaloamini hivi ni kanisa la *United Pentecostal Church.*

Kwa wakati wa sasa makanisa mengi yanayoamini katika Utatu Mtakatifu yanabatiza wakitumia maneno, "Nakubatiza wewe kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu." Wanathibitisha imani yao iliyo katika Yesu na kuamini katika Utatu Mtakatifu wa Mungu.

## Namna ya Kufanya Ubatizo

**Kusanyiko:** Watu wapya walioamini ambao ndio wanaotegemewa kubatizwa watapaswa kusimama kwa pamoja ili kuonyeshwa kwa watu ambao wamehudhuria kuja kushuhudia. Wakati kundi likiendelea kukusanyika pamoja, mtu mmoja anaweza kuwaongoza katika kuimba kwa dakika chache.

**Andiko:** Mtu mmoja anaweza kusoma kutoka katika Mathayo 28:18-20.

**Tamko:** Mchungaji atatakiwa azungumze na kundi lililohudhuria na kusema, "Hawa walioko hapa kwa ajili ya kubatizwa wamethibitika kwamba wametubu na kuiweka imani yao kwa Kristo. Kwa kuwa ubatizo unawakilisha kifo na ufufuo wa Yesu, waumini hawa wanathibitika kwa njia ya ubatizo kwamba wamekufa kwa dhambi na sasa wanaishi kwa ajili ya Mungu. Wameanza maisha mapya ya utiifu kwa Mungu."

**Maombi:** Kisha mchungaji ataliongoza kwenye maombi kwa ajili ya watu wapya walioamini ambao watapata ubatizo. Maombi yake yatahusisha pamoja na matamko kama haya: "Bwana, tunasema asante kwa ajili ya neema yako ambayo imewaleta watu hawa kwenye wokovu na maisha ya kiroho. Tunasema asante kwa sababu umewatoa katika nguvu ya dhambi. Tunaomba kwa ajili ya Roho Mtakatifu awajaze na kuwapa ushindi kila siku. Wafanye wawe mashahidi kwenye jumuiya zao na wawe baraka kwa kanisa."

**Ubatizo:** Watu wapya walioamini ambao wamekuja kwa ajili ya kubatizwa wataingia mmoja mmoja ndani ya maji kumwendea mchungaji alipo. Kabla ya kumbatiza kila mmoja, mchungaji atapaswa kusema, "Nakubatiza wewe… kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu."

**Wimbo wa pamoja:** Baada ya ubatizo kufanyika, kusanyiko linaweza kuimba wimbo wa pamoja. Mtu mmoja anaweza akaongoza tena kwenye kufanya maombi mafupi.

## Taarifa Saba kwa Muhtasari

1. Wanafunzi wa Yesu walibatiza wakati wa huduma yake.
2. Kanisa la mwanzo lilibatiza watu kila mahali injili ilipokwenda.
3. Ubatizo unaashiria kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu.
4. Ubatizo ni ushuhuda wa wokovu na maisha mapya ndani ya Kristo.
5. Mtu mpya aliyeamini anapaswa kubatizwa mara moja baada ya kuokoka.
6. Mtu hapaswi kudhania kwamba yeye ni Mkristo kwa sababu tu alikuwa amebatizwa.
7. Kanisa linapaswa kuthibitisha imani ya Utatu Mtakatifu katika ubatizo.

**Kazi za kufanya Somo la 10**

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 10. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.
3. Masailiano: Fanya mazungumzo na waumini watatu tofauti na uwaulize ubatizo wao ulimaanisha nini kwao. Andika muhtasari mfupi kuhusiana na mazungumzo hayo.

# Somo la 11
# Meza ya Bwana

## Elekezo kwa kiongozi wa darasa

*Kiongozi wa darasa au wanafunzi waliochaguliwa watapaswa waelezee historia ya ukombozi wa Israeli kutoka utumwani Misri. Ruhusu wanafunzi mbalimbali wachangie mada hii. Kitabu cha Kutoka 11-12 kinaelezea kuhusu Pasaka ya kwanza.*

## Asili ya Zoezi la Meza ya Bwana

Pasaka ilikuwa ni sikukuu ya Wayahudi iliyokuwa ikisherehekewa katika nyakati za usiku wakati taifa la Israeli lilipotoka Misri. Sherehe haikuwa tu kwa ajili ya kukombolewa kutoka Misri; ilikuwa ni sherehe iliyohusu rehema ya Mungu juu yao wakati alipowapiga Wamisri kwa vifo lakini akaziruka nyumba za wana wa Israeli bila vifo (Kutoka 12:27). Kwa hiyo, tukio hili lilikuwa ni ishara ya rehema za Mungu dhidi ya watu wake.

Baada ya kukombolewa kutoka Misri, Waisraeli walikuwa na sikukuu ya Pasaka kila mwaka. Mungu aliwapa vitu vya kusherehekea kwa ajili ya siku hiyo ikiwa ni pamoja na chakula maalumu na matumizi ya damu ya kusherehekea.

Tukio hilo lilikuwa kama aina ya wokovu. Hiyo haina maana kwamba watu waliokombolewa katika siku hiyo walisamehewa dhambi zao zote na kuwa katika uhusiano sahihi na Mungu. Hata hivyo, walikombolewa kutoka utumwani, walipokea neema kutoka kwa Mungu, na damu ilikuwa sehemu ya hitaji la Mungu. Mambo haya yote yaliyofanyika yanafanya tukio hili kuwa kama kielelezo cha wokovu ulioletwa na Kristo. Waisraeli walio wengi walisherehekea sikukuu hii bila ya kutambua maana yake kamili.

Kwenye Pasaka ya mwisho ambayo Yesu alishirikishana na wanafunzi wake, alielezea maana yake. Alianzisha sherehe ya kufanya kwa ajili ya kanisa wakati aliposema "Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu" (Luka 22:15-20). Makanisa huiita sherehe hii "Chakula cha Bwana," au "Meza ya Bwana," au "Ekaristi," au "Ushirika Mtakatifu."

Paulo aliandika kwamba mila hii itafanywa mara kwa mara na kanisa hadi hapo Yesu atakaporudi (1 Wakorintho 11:24-26). Kanisa lilikuwa na nyakati maalumu za sikukuu na ushirika ambazo hazipaswi zichanganywe na Meza ya Bwana. Kwa mfano, wakati Biblia inaposema kwamba waumini wa mwanzo walikuwa "wakimega mkate nyumba kwa nyumba," tunapaswa tukumbuke kwamba maneno haya kuumega mkate yanarejelea tu kwenye kula (Matendo 2:46). Walikuwa wanafanya ushirika wa kula pamoja katika nyumba mbalimbali. Kanisa pia lilikuwa na "karamu za upendo" ambazo hazikuwa sawa na Meza ya Bwana (Yuda 1:12).

## Maana ya Meza ya Bwana

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Yohana 6:47-58 kwa ajili ya kikundi.

Yesu aliushangaza umati aliposema kwamba alikuwa ni mkate kutoka mbinguni na kwamba walitakiwa waule mwili wake na wainywe damu yake.

► Je, Yesu alikuwa anamaanisha nini kwa kauli hizo?

Yesu alisema alikuwa anajitoa mwenyewe kwa ajili uhai wa ulimwengu (Yohana 6:51). Alikuwa anazungumzia kuhusu dhabihu yake mwenyewe ya kujitoa kwa ajili ya utakaso. Alilinganisha dhabihu yake kwa kutumia chakula na kinywaji. Kama vile ambavyo mtu huhitaji chakula kwa ajili ya maisha ya kimwili, ni lazima akubali dhabihu ya Kristo kwa ajili ya maisha ya milele.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Luka 22:15-20 kwa ajili ya kikundi.

Kwenye chakula cha mwisho cha Pasaka pamoja na wanafunzi wake, Yesu alisema kwamba mkate ulikuwa ndio mwili wake na divai ndiyo damu yake. Atautoa uhai wake kwa ajili ya wokovu wao.

## Mkate na Divai



► Je, kwa nini Yesu alitumia mkate na divai kwa ajili ya Meza ya Bwana?

Kunaweza kuwepo na sababu nyingi ambazo zinaonyesha ni kwa nini Yesu alitumia mkate na divai kwa ajili ya Meza ya Bwana.[7] Mkate ulikuwa ndio chakula kikuu cha msingi, kama ilivyokuwa kwenye maeneo mengine ya dunia. Mkate hauwakilishi tu chakula kwa ujumla, lakini pia unawakilisha uhai kwa sababu chakula ni muhimu kwa ajili ya uhai. Divai ilikuwa ndicho kinywaji kinachotumika kwa wakati ule, ukiacha maji. Divai pia inawakilisha sherehe au maadhimisho.

Baadhi ya makanisa ya sasa yanatumia divai kwa ajili ya Meza ya Bwana hata kama hawanywi divai kwa nyakati nyingine zote. Makanisa mengine yanatumia juisi ya zabibu au mvinyo ambao haujachachuka kwa sababu hawataki kuhamasisha unywaji wa aina yeyote ya pombe. Juisi ya zabibu ilijulikana kama mvinyo kwenye Agano Jipya ikiwa aidha bado ni mbichi *(haijachachuka)* au ikiwa kwenye hatua yeyote ya kugeuka kuwa pombe *(kuchachuka).*

Baadhi ya makanisa yamebadilika kabisa kutumia vitu vingine vya kula na kunywa kwa ajili ya Meza ya Bwana. Tunapaswa tuwe waangalifu sana kuhusiana na matumizi ya kitu kingine

[7] Image: “The Lord's Supper” taken by Allison Estabrook on Oct. 14, 2022, retrieved from https://nidhamu.flickr.com/photos/sgc-library/52476662295/, licensed under CC BY 4.0.

kwa ajili ya Meza ya Bwana. Wamomoni wanatumia mkate na maji, lakini hawaamini katika fundisho la imani la Kikristo kuhusiana na upatanisho.

Katika maeneo mengine ya dunia inawezekana mkate na divai visiweze kuwa vinapatikana kama kawaida; vitu vingine vinaweza kuwa vya msingi kama chakula na kinywaji. Katika hali kama hiyo, kanisa kwa njia ya maombi linaweza kufikiria njia nyingine za kutumika.

## Siyo Mwili au Damu ya Kawaida

Kanisa Katoliki na Kanisa la Othodoksi ya Mashariki yanaamini kwamba mkate na divai ndivyo mwili na damu halisi ya Yesu. Kuna makanisa mengine yanayoamini kwamba mwili wake na damu yake ni kweli kabisa viko kwenye mkate na divai. Makanisa mengi ya Kiprotestanti yanaamini kwamba mkate na divai vinawakilisha mwili na damu ya Yesu bila ya uwepo wake katika hali yake ya mwili halisi.

Wakati Yesu alipowahudumia wanafunzi wake kwenye Pasaka, alisema, "Hii ndiyo damu yangu…huu ndiyo mwili wangu." Yesu bado alikuwa amesimama pale, katika hali ya kimwili pamoja nao. Mwili na damu yake vilikuwa bado havijatolewa kama dhabihu. Inaonekana wazi aliimaanisha kwamba mkate na divai vilikua ni ishara ya mwili na damu, na siyo mwili na damu katika hali yake ya uhalisia. Mkate na divai vinavyotumika katika Meza ya Bwana vinapaswa vichukuliwe na kufikiriwa hivyo.

Wokovu uko katika dhabihu ya mara moja tu ya Yesu. Kifo chake hakitokei kwa kurudiarudia. Kwa kuwa Meza ya Bwana ni kitendo cha ibada na imani katika tukio moja tu la kifo cha Yesu, hakuna ulazima kwa mkate na damu vifanyike tena kwamba ni mwili na damu halisi ya Yesu.

Kwa kuwa Wakatoliki wanaamini kwamba kanisa lina mamlaka ya kutoa mwili na damu halisi ya Yesu, waumini wengi miongoni mwao wanaamini kwamba kanisa lina mamlaka juu ya kufanya ni nani anaweza kuokoka. Wanafikiri kwamba mtu hawezi kuokoka kama kasisi atamkatalia kumpa Meza ya Bwana. Mamilioni wanafikiri kwamba mtu huwa ameokoka kwa kutumia Meza ya Bwana.

Mtazamo sahihi wa Meza ya Bwana ni kwamba ni kitendo cha ibada kinachoashiria kifo cha Kristo kwa ajili yetu, wakati ambapo Mungu anaachilia neema yake kama majibu kwa imani ya mtu anayeshiriki. Ni kwa ajili ya watu waliookoka, na ambao wokovu wao hautegemei kupatikana kwa Meza ya Bwana.

► Je, kwa nini hatupaswi kufikiri kwamba Yesu alimaanisha kwamba mkate na divai vilikuwa ni mwili na damu yake halisi?

► Je, ni kwa nini siyo lazima kwa ajili ya wokovu kwamba Meza ya Bwana iwe ni mwili na damu halisi ya Kristo?

## Njia ya Neema

> "Njia za neema ni njia za kiungu zilizochaguliwa ambazo kwa kupitia hizo ushawishi wa Roho Mtakatifu unaungamanishwa na roho za wanadamu."
>
> - Wiley & Culbertson, *Introduction to Christian Theology*

Meza ya Bwana mara nyingi huitwa njia ya neema. Mungu ameiandaa Meza ya Bwana kama njia ya neema wakati inapopokelewa kwa imani kwenye upatanisho wa Kristo. Mkristo anapaswa kumtii Mungu kwa kufuata maagizo yaliyoko kwenye maandiko. Mkristo hapaswi kupuuzia njia hii ya neema.

Endapo mtu atatumia Meza ya Bwana bila ya imani katika Kristo, haiwezi yenyewe ikaleta neema kwake ya moja kwa moja.

Endapo mtu ataitumia bila ya kuheshimu kwa ajili ya kile kinachomaanishwa, anajiletea hukumu juu yake yeye mwenyewe (1 Wakorintho 11:27-29).

Kutubu na imani ni mambo muhimu katika wokovu. Meza ya Bwana siyo jambo lililo muhimu kwa ajili ya wokovu. Meza ya Bwana ni kitendo cha utii na kudhihirisha imani. Mkristo hataacha kuendelea kuwa Mkristo kama hatakuwa na uwezo wa kupata Meza ya Bwana.

► Je, ni jambo la lazima kwa Mkristo kutumia au kushiriki Meza ya Bwana? Toa ufafanuzi wa Jibu lako.

## Njia Sahihi za Utumiaji wa Meza ya Bwana

Mtume Paulo alitoa masahihisho kwa Wakorintho kutokana na utumiaji mbaya wa Meza ya Bwana uliokuwa ukifanyika. Maelekezo yake pia yako kwa ajili yetu sisi.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 11:20-34 kwa ajili ya kikundi. Je, ni mambo gani ambayo Wakorintho walikuwa wanafanya vibaya?

Walikuwa wanaleta chakula na kukifanya ni chakula cha Meza ya Bwana. Kila mtu alikula chakula chake mwenyewe kuliko kushirikishana na wenzake. Hakuna mtu aliyekuwa akimsubiri mwenzake ili waweze kuanza kula kwa pamoja na kwa wakati mmoja. Watu wengine walikuwa wakila kupita kiasi, na wengine bado wakiwa na njaa. Wengine walikuwa wakinywa sana hata kulewa.

► Je, ni maelekezo gani maalumu waliyopewa na Paulo?

Aliwataka wasifanye Meza ya Bwana kama ni chakula. Makanisa yalikuwa na vyakula vya sherehe au ushirika, lakini hivyo havikuwa ni Meza ya Bwana. Aliwataka wasubiriane kila mmoja na mwenzake ili waweze kuanza kwa pamoja.

Paulo alifanya mapitiyo ya njia ambazo Yesu aliweka mila ya kufuata kwa ajili ya kanisa. Yesu alitoa mkate, kisha mvinyo, na akiwa anaelezea maana yake. Ni muhimu sana kwa mshiriki kuvipokea kwa heshima, akikumbuka Meza ya Bwana inamaanisha nini.

Paulo alisema kwamba kila mtu na ajihoji mwenyewe ili kuhakikisha kwamba hashiriki katika Meza ya Bwana "isivyofaa." Baadhi ya watu wanatafsiri kwamba hiyo inamaanisha mtu hapaswi kushiriki katika Meza ya Bwana hadi awe amejihakikisha kwamba maisha yake yanampendeza Mungu katika kila jambo. Hayo sivyo aya inavyofundisha. Mtume alikuwa anazungumzia kuhusu njia ya kushiriki Meza ya Bwana. Mtu anakuwa amehukumiwa endapo atakuwa ameipokea kwa njia isiyo ya kawaida na kutojali.

Ni vyema kwa kusanyiko kuomba pamoja wakati wa kushiriki Meza ya Bwana. Watu tofauti wanaweza wakaandaliwa kuongoza maombi kwenye wakati tofauti wa ibada. Kikundi kinaweza kuimba kwa pamoja wakati wowote wakihitajika. Ibada inatakiwa ifanyike katika hali ya ukimya na yenye mpangilio uliokamilika. Haipaswi iwe ni wakati wa sauti kubwa au kujifurahisha wenyewe. Ni wakati wa kutafakari juu ya dhabihu ya Yesu iliyotolewa kwa ajili ya ukombozi wetu.

## Watu sahihi wanaostahili kushiriki katika Meza ya Bwana

► Je, ni nani aruhusiwe kushiriki katika Meza ya Bwana?

Yesu alifundisha jambo la kufanya kwa wanafunzi wake na akawaambia wafanye kwa pamoja, kwahiyo tunajua kwamba Meza ya Bwana ni kwa ajili ya Wakristo. Meza ya Bwana haipaswi Kutolewa kwa mtu ambaye ni mfuasi wa dini nyingine. Mtu anayeabudu miungu mingine anaabudu mashetani. Hawezi pia akamwabudu Kristo (1 Wakorintho 10:20-21).

Kama mtu anaishi katika dhambi ya wazi na bado hajatubu, hapaswi kushirikishwa katika Meza ya Bwana. Kushirikishwa katika Meza ya Bwana ni kuthibitisha kwamba tumejitambulisha pamoja katika kifo cha Kristo. Mtu ambaye anaendelea kwa hiari yake kuwa mtenda dhambi hana ushuhuda huo.

Mtu anayeishi kwenye dhambi ya wazi ya kujitakia kama vile uasherati, ibada ya sanamu, au ulevi siyo Mkristo (1 Wakorintho 6:9-10). Biblia inatuambia kwamba hatuwezi kuwa kwenye ushirika mmoja na mtu anayetenda dhambi hizi na bado anajinadi kwamba yeye ni Mkristo (1 Wakorintho 5:11). Kwa hiyo halitakuwa jambo sahihi kumshirikisha katika Meza ya Bwana.

Kama mwanachama ametenda dhambi na amekataa marekebisho ya kanisa, achukuliwe kama mtu ambaye hajaokoka (Mathayo 18:17), na kwa ajili hiyo hatapaswa kushirikishwa Meza ya Bwana.

Meza ya Bwana inaonyesha umoja maalumu ambao unawahusu Wakristo. Neno *Meza ya Bwana* linakuwa na maana hiyo. Mtume alisema kwamba katika tendo la Meza ya Bwana tunadhihirisha kwamba tuko mwili mmoja (1 Wakorintho 10:16-17). Kwa hiyo, kama itajulikana kwamba mtu ni mzembe, asiyejali kuhusu kuwa mtenda dhambi, hawezi kushirikishwa katika umoja huo.

Mchungaji anapaswa kushirikisha Meza ya Bwana kwa Wakristo, lakini hawajibiki kuchunguza kila jambo lililo katika maisha yao. Kama mtu atajishuhudia kwamba yeye ni Mkristo na haishi katika dhambi ya wazi, mchungaji anaweza akaukubali ushuhuda wake.

Mtu yeyote ambaye kweli ameokoka anakuwa amepokea upatanisho ambao umewakilishwa na Meza ya Bwana, aidha awe au asiwe ni mwanachama wa kanisa fulani la mtaa. Kwa hiyo, uanachama wa kanisa la mtaa haupaswi uwe ni kigezo kwa ajili ya kushiriki Meza ya Bwana.

Mtu aliyeokoka kwa ukweli ana sifa zote za kushiriki katika Meza ya Bwana na ubatizo. Hapaswi aendelee kusubiri hadi baada ya ubatizo ndipo ashiriki katika Meza ya Bwana, ikiwa yuko tayari kubatizwa.

Kama kusanyiko ni mchanganyiko wa Wakristo na watu ambao hawajaokoka, ikiwa ni pamoja na watu ambao wanaishi katika matendo ya dhambi, Meza ya Bwana haipaswi ishirikishwe kwa kusanyiko lote kwa ujumla. Meza ya Bwana inaweza ikapangiwa wakati wake mwingine kwa ajili ya wale walio na sifa za kushiriki.

► Je, kuna sababu gani ambazo mtenda dhambi za wazi hapaswi kushirikishwa katika Meza ya Bwana?

## Mzunguko wa Meza ya Bwana

► Je, Meza ya Bwana iwe inatolewa kwa mara ngapi? Kwa nini?

Baadhi ya makanisa hushirikisha Meza ya Bwana kila wiki. Makanisa mengine hushirikisha mara moja kwa mwaka. Mengine hufanya mara chache sana, bila ya ratiba.

Biblia haijatuambia ni mara nyingi kiasi gani tushirikishe Meza ya Bwana.

Baadhi ya watu kabla ya kuokoka walitumainia desturi za kidini kwa ajili ya wokovu. Wakati walipookoka na kuachana na aina hiyo ya desturi, wanaweza wasijisikie tena vizuri na aina yeyote ya desturi za kidini. Wanaweza wakafikiri kwamba Meza ya Bwana haipaswi ishirikishwe mara nyingi.

Baadhi ya watu kwa makosa huiweka imani yao kwenye desturi za dini. Wanataka wawe na Meza ya Bwana mara nyingi kwa sababu inawasaidia kufikiri kwamba wameokoka.

Ni jambo muhimu sana kwa mchungaji kuelezea maana ya Meza ya Bwana. Anapaswa awasaidie watu wake kuelewa jinsi ya kuitumia kama baraka kwao katika uhusiano wao na Mungu bila ya kuiamini kwa njia iliyo potofu.

## Mamlaka Kamili kwa ajili ya Usimamizi wa Meza ya Bwana

► Je, ni nani mwenye haki ya kushirikisha Meza ya Bwana?

Biblia inatuambia kwamba kila mtu aliyeamini ni kuhani (Ufunuo 1:6, 1 Petro 2:5, 9). Hii ina maana kwamba tunaweza tukamwabudu Mungu moja kwa moja pamoja na kuwasaidia watu wengine waweze kumwabudu yeye. Hakuna mpatanishi yeyote duniani ambaye ni

lazima kwa ajili ya kutuleta kwa mungu, kwa sababu Yesu ndiye Kuhani wetu Mkuu, na ametupa fursa ya kuingia (1 Timotheo 2:5, Waebrania 4:14-16). Kwa yeye, sisi tunapaswa bila kikomo tuendelee kutoa dhabihu zetu za sifa (Waebrania 13:15).

Kwa kuwa kila mtu aliyeamini ni kuhani, tunaweza tukawa na sababu kwamba mtu yeyote aliyeamini anaweza kushirikisha Meza ya Bwana kwa waumini wengine, hasa wakati ambapo mchungaji hayupo. Hata hivyo, kuna sababu ambazo Meza ya Bwana inapaswa kwa kawaida ishirikishwe kwa maelekezo ya mchungaji.

Biblia haijatoa tamko la moja kwa moja kwamba Meza ya Bwana inapaswa ishirikishwe tu na mchungaji. Hata hivyo, Paulo alitoa maelekezo maalumu kwa ajili ya kushirikisha Meza ya Bwana kwa njia ya utaratibu na yenye heshima. Maelekezo hayo yalikuwa ni kwa ajili ya kikundi, na kiongozi alikuwa anawajibika kukiongoza kikundi. Katika hali ya kawaida washiriki wa kanisa watamtegemea mchungaji wao kwamba atahakikisha Meza ya Bwana itashirikishwa vizuri, na mchungaji atapaswa alichukue hilo jukumu.

► Angalia tena maonyo yaliyotolewa katika 1 Wakorintho 11:27-34.

Paulo alisema kwamba maelekezo yalikuwa ni muhimu kwa sababu ya heshima kwa ajili ya mwili na damu ya Kristo. Kama mtu alikuwa asiyejali, atakuwa mwenye hatia. Hukumu ya Magonjwa na vifo tayari imekuja juu ya walio wengi. Paulo alisema kwamba kama wangekuwa makini kujitathmini wenyewe, watakuwa wameepushwa na hukumu ya Mungu. Paulo alisema kwamba baadaye angekuwa na maelekezo ya ziada kwa ajili yao.

Ni jambo la muhimu kushiriki katika Meza ya Bwana kwa njia nzuri, siyo tu kwa ajili ya kukwepa madhara yanayotokana na matumizi mabaya, bali kupata faida ambazo Mungu ameziweka kwa ajili yetu.

Ni jambo la mantiki kufikiri kwamba mtume alitegemea viongozi wa kanisa waweze kuhakikisha kwamba maelekezo haya yanatekelezwa. Wanachama wa kanisa watapenda kuona wachungaji wao wakiwasaidia katika kushirikishwa Meza ya Bwana kwa njia nzuri kwa sababu ya umuhimu wake.

Mchungaji pia analo jukumu maalumu la kuangalia kwamba Meza ya Bwana haishirikishwi kwa mtu ambaye ni wa dini nyingine au dhambi ya wazi.

Kwa hiyo, Meza ya Bwana kwa kawaida inapaswa ishirikishwe na mchungaji au mtu mwingine chini ya maelekezo ya mchungaji. Mchungaji anaweza kuwaelekeza watu wengine wamsaidie yeye katika ibada ya kushirikisha Meza ya Bwana na anaweza kuidhinisha mtu kutumikia karamu ya Bwana akiwa hayupo.

## Utaratibu kwa ajili ya kushirikisha Meza ya Bwana

**Kukusanyika:** Kutatakiwa kuwepo na utaratibu wa kukusanyika kwa watu ambao watashiriki katika Meza ya Bwana. Kama itapaswa ifanyike kwenye ibada ya kuabudu ya watu wote wa kanisa, viongozi wanaohusika ni lazima waweze kujua ni kwa jinsi gani watawahudumia watu wale tu walio sahihi kushirikishwa.

**Maandiko:** Kabla Meza ya Bwana haijaanza kushirikishwa, Maandiko yanapaswa yasomwe. Taarifa chache zinaweza Kutolewa kuhusiana na Maandiko hayo, lakini ziwe fupi. Mifano ya vifungu vya maandiko ambavyo vinaweza vikatumika ni pamoja na Mathayo 26:26-30, Markoo 15:22-28, Luka 22:14-20, Yohana 10:11-18, Yohana 19:1-6, Yohana 19:16-19, Yohana 20:26-29, 1 Wakorintho 11:23-26, Waebrania 10:11-17, Waebrania 9:24-28, Waebrania 4:12-16, Ufunuo 1:12-18, Isaya 53:1-5, au Isaya 53:6-12.

**Maombi:** Mtu mmoja ataongoza katika maombi. Maombi hayo yanapaswa yahusishe pamoja na taarifa kama hizi: "Bwana, tunasema asante kwa ajili ya ukombozi uliotupatia kupitia dhabihu ya Yesu. Tunasema asante kwa neema ya bure uliyotupatia sisi. Tunapoenda kushiriki Meza ya Bwana kwa pamoja tunashuhudia kwamba tunakutegemea wewe pekee katika maisha yetu ya kiroho. Tunadhihirisha umoja wetu tulio nao kwa pamoja kama waumini. Tunaomba kwa ajili ya neema yako itakayotuwezesha tuishi maisha ya kukupendeza wewe kila siku."

**Kugawa mkate:** Mkate unaweza ukagawanywa na mchungaji au watu aliowachagua. Anaweza akasema, "Mkate huu unawakilisha mwili wa Kristo, uliotolewa kwa ajili ya wokovu wetu." Kila mtu atapaswa anyamaze kimya na kuonyesha heshima wakati wote wa Meza ya Bwana. Kwenye makanisa mengine, mchungaji huwataka watu wanaoshiriki kushikilia mkate hadi kila mmoja anapokuwa amepata, kisha watakula kwa pamoja. Kwenye makanisa mengine, mila iliyopo ni kila mtu kula mkate wake akishaupokea.

**Maombi:** Mchungaji au mtu mwingine yeyote aliyechaguliwa anaweza akaongoza maombi mafupi ya kumshukuru Mungu kwa ajili ya neema yake.

**Kugawa Divai:** Mchungaji anaweza akasema, "Divai hii inawakilisha damu ya Yesu, iliyotolewa kwa ajili yetu." Baadhi ya makanisa hugawa divai ikiwa kwenye vikombe maalumu kwa kila mtu. Wengine hupitisha kikombe kimoja tu. Kwenye makanisa mengine, kila mtu hutumbukiza kipande chake cha mkate ndani ya kikombe kilicho na divai. Jambo muhimu hapa ni kwamba ushirikishwaji hufanyika katika mpangilio mzuri na kwa heshima.

**Maombi:** Mchungaji au mtu mwingine yeyote aliyechaguliwa anaweza akaongoza maombi mafupi ya kumshukuru Mungu.

**Wimbo:** Kikundi kinaweza kuimba wimbo wa pamoja.

## Taarifa Saba kwa Muhtasari

1. Meza ya Bwana hutokana na sherehe za Wayahudi za Pasaka.
2. Pasaka iliashiria upatanisho uliotolewa na Kristo.
3. Mkate na divai ni ishara ya mwili na damu ya Yesu.
4. Meza ya Bwana haitoi wokovu wa moja kwa moja kwa mtu anayeishiriki.
5. Meza ya Bwana inaweza ikaleta neema kama mtu ataipokea kwa imani katika upatanisho wa Kristo.
6. Meza ya Bwana haipaswi kushirikishwa kwa watu wenye kutenda dhambi za wazi au wafuasi wa dini nyingine.
7. Mchungaji analo jukumu la kuhakikisha kwamba ushirikishwaji wa Meza ya Bwana unafanyika vizuri.

## Kazi za kufanya Somo la 11

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 11. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.
3. Masailiano: Fanya mahojiano na waumini watatu kuhusu Meza ya Bwana kwamba inamaanisha nini kwao. Andika muhtasari mfupi kuhusiana na mahojiano hayo.

# Somo la 12
# Nidhamu ya Kanisa

## Utangulizi

Katika Somo la 3, tulijifunza tafsiri hii kuhusiana na kanisa la Mahali au mtaa:

> Kanisa la mahali ni kikundi cha waumini ambacho kinafanya kazi kama familia ya kiroho na jamii ya imani; wakitoa injili na ushirika wa kanisa kwa kila mtu anayetubu; wakitekeleza tendo la ubatizo na ushirika wa meza ya Bwana, wakishirikiana katika kumwabudu Mungu, ushirika, uinjilisti, uanafunzi, na kukamilisha kazi ya mwili wa Kristo kwa karama za Roho Mtakatifu; waliojitoa kabisa kwa ajili ya Neno la Mungu; wakiwa na umoja ulio katika msingi wa mafundisho ya imani ya kibiblia, wakiwa na uzoefu wa neema, na maisha ya Roho Mtakatifu.

Sasa tutafakari tafsiri ya nidhamu ya kanisa.

**Tafsiri ya Nidhamu ya kanisa**

nidhamu ya kanisa ni umoja wa kanisa, wenye lengo la kuwajibisha dhambi inayotendwa na mwanachama kukiwa na makusudi manne ya kulinda um/oja wa kanisa, kusimamia ukweli, kulilinda kusanyiko kutokana na ushawishi mbaya, na kumrejesha tena mwanachama aliyeanguka dhambini kwenye wokovu na ushirika.

► Angalia tafsiri ya kanisa na tafsiri ya nidhamu ya kanisa. Kwa kuzingatia kanisa ni nini, elezea ni kwa nini nidhamu ya kanisa ni muhimu.

## Umuhimu wa Nidhamu ya Kanisa

Kunatokea nini wakati mwanachama wa kanisa anaporejea kwenye dhambi, lakini bado anashiriki kuja kwenye kanisa? Itakuwaje kama mwanachama kwa uhakika haamini misingi ya mafundisho ya imani ya kanisa na anafundisha imani potofu? Inakuwaje kama mwanachama amemtendea mtu mwingine mambo yasiyostahili na hayuko tayari kukiri makosa yake?

Baadhi ya makanisa yalikemewa na Yesu kwa sababu yalishindwa kufanya nidhamu ya kanisa. Kanisa la Pergamo lilikuwa na waalimu wenye kufundisha mafundisho ya imani potofu ambayo ilipaswa kuondolewa, lakini haijaondolewa.(Ufunuo 2:14-16). Kanisa la Thiatira lilikuwa na mwanamke ambaye Yesu alimwita Yezebeli, ambaye aliwaongoza watu kufanya uasherati na kuabudu sanamu; kwa hiyo, Bwana akalikemea kanisa (Ufunuo 2:20).

Biblia inatueleza kwamba haiwezekani kuwepo na ushirika kati ya nuru na giza, au kati ya watu wanaomtumikia Kristo na watu wanaotumikia miungu mingine (2 Wakorintho 6:14-15).

Hapa tutaangalia sababu nne zinazofanya nidhamu ya kanisa iwe muhimu sana. Tukiendelea na somo hili, tutaangalia msaada wa kimaandiko kwa ajili ya hizi sababu, lakini tunaziandika hapa kwa muhtasari ili kuzifanya ziwe nyepesi kujifunza.

1. **Nidhamu ya kanisa ni muhimu kwa sababu kanisa ni lazima liwe na umoja.** Umoja wa kanisa una msingi wake katika mafundisho ya imani ya Biblia na maisha ya Roho. Tafsiri ya kanisa inaonyesha ni kwa jinsi gani wanachama wa kanisa wanapaswa wawe katika ushirika wa kiroho. Ushirika wa kiroho una msingi wake katika uhusiano wao na Mungu na uzoefu wa neema. Kama mtu atakuwa amepoteza uhai wake wa kiroho, hawezi tena akawa na ushirika wa Kikristo. Kama mwanachama atakataa kukubaliana na ukweli, akatubu dhambi, au akakubaliana na makosa, anakuwa hana tena umoja na kanisa.

2. **Nidhamu ya kanisa ni muhimu kwa sababu kanisa ni lazima lisimamie ukweli.** Kuendelea kumruhusu mwanachama wa kanisa aendelee kutenda dhambi ni kushindwa kusimamia ukweli. Kanisa haliwezi kusimama kwa ajili ya ukweli mbele ya ulimwengu kama wanachama wake wanaishi katika kukiuka ukweli.

3. **Nidhamu ya kanisa ni muhimu kwa ajili ya kuzuia watu wa kanisa kutokana na ushawishi mbaya.** Kama mwanachama wa kanisa bado anaendelea katika dhambi ya wazi na bado anaendelea kupewa heshima kama Mkristo, wanachama wengine watashawishika kufanya vivyo hivyo.

4. **Nidhamu ya kanisa ni muhimu katika kumrejesha tena mwanachama aliyeanguka dhambini.** Kama mwanachama wa kanisa anaishi katika dhambi na hakabiliwi kwa matendo yake, kuna uwezekano mdogo sana wa kuweza kutubu. Kama atakabiliwa vilivyo anaweza akakasirika, lakini baadaye atakuwa na uwezekano mkubwa wa kuweza kutubu.

> "Serikali ya kanisa la Kristo kwa mapana yake ni tofauti na serikali za kidunia. Inaundwa kwa unyenyekevu na upendo wa kindugu: inatokana na Kristo, kiongozi mkuu wa kanisa, na siku zote huongozwa kwa hekima zake na katika Roho."
>
> \- Adam Clarke, *Christian Theology*

Adhabu siyo sababu ya nidhamu ya kanisa. Adhabu siyo jukumu la kanisa kwa mwanachama wake. Mungu peke yake ana uwezo wa kuadhibu kwa ajili ya dhambi. Kitendo cha kanisa kinapaswa kiwe ni kwa ajili ya kusudi la kurekebisha, na siyo adhabu.

► Je, ni kitu gani kitakachotokea kama kanisa litashindwa kuchukua hatua za nidhamu kwa mwanachama anayetenda dhambi wazi wazi?

### Maelekezo kutoka kwa Yesu kuhusu Nidhamu ya kanisa

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Mathayo 18:15-20 kwa ajili ya kikundi.

Yesu alikuwa ametoa maelekezo kwa ajili ya kushughulika na migogoro kati ya waumini wawili. Kama muumini anafikiri kwamba kuna mtu aliyemtendea jambo lililo baya, anapaswa azungumze na huyo mtu kibinafsi. Matatizo mengi yanatatuliwa katika hatua hii. Wakati mwingi kumekuwepo na kutoelewana. Kama waumini wawili ni waaminifu na wanyenyekevu, wanaweza wakatatua tatizo lililoko kati yao.

Uhusiano miongoni mwa waumini ni jambo la thamani sana. Kama mtu anaamini kwamba mtu mwingine amemkosea, uhusiano unakuwa umeharibika. Anapaswa aende kwa huyo mtu aliyemfanyia ubaya kwa unyenyekevu na upole na aonyeshe kwamba uhusiano ni kitu muhimu sana kwake. Anaweza akasema neno kama hili: Ndugu yangu, nathamini baraka ulizonazo katika kanisa. Wewe ni rafiki muhimu. Lakini nina wasiwasi kwa sababu ninahisi ulinifanyia mabaya. Ninazungumza na wewe peke yako katika jambo hili kwa sababu ninataka uhusiano wetu uwe wa kweli." Elezea hilo jambo ulilofanyiwa ubaya, lakini kuwa mwangalifu usiwe mkali sana au mwenye kulaumu. Kuwa tayari kusikiliza. Kuwa tayari kusamehe.

Kwa mujibu wa maelekezo ya Yesu, kama mtu kiuhalisia ametenda ubaya na hataki kukiri kosa, mtu mwingine atazungumza naye tena akiwa na mtu mmoja au wawili wenye heshima zao. Kwa mara nyingine tena, sisitiza kwa aliyekukosea kwamba yeye anapendwa na kwamba uhusiano ni jambo muhimu.

Kama mtu aliyekukosa ataendelea kukataa kukiri kosa lake, itabidi taarifa zake zipelekwe kwa viongozi wa kanisa. Watatakiwa wazungumze na yeye. Kama bado ataendelea kukataa kusikiliza, kanisa likubaliane kwa pamoja kumwona kama mtu asiyeamini.

Kumwona mtu kama asiyeamini haimaanishi kwamba ni kumtendea ukatili. Inamaanisha kwamba hatakuwa tena mshirika au mwanachama wa kanisa au wa huduma yeyote ya kanisa. Hawezi akashiriki katika Meza ya Bwana kwa sababu anachukuliwa kama ni mtu wa mataifa (aya ya 17). Kanisa litapaswa limjulishe kwamba hawamtambui tena kama mwamini wao na kwamba bado wanamwombea ili aweze kutubu.

Baada ya maelekezo haya yote, Yesu alitoa somo lililohusiana na msamaha (Mathayo 18:21-35). Kama mtu akikiri makosa yake na kutubu, tunapaswa tuwe tayari kusamehe.

► Je, utazungumzaje na mtu ambaye amekukosea wakati unapojaribu kurejesha uhusiano?

### Maelekezo kutoka kwa Paulo kuhusu Nidhamu ya Kanisa

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 5 kwa ajili ya kikundi. Je, kuna hali gani ambayo Paulo ameielezea katika sura hii?

Mtume Paulo alitoa maelekezo ya nidhamu ya kanisa kwa ajili ya kadhia maalumu iliyokuwa katika kanisa la Korintho. Mwanachama mmoja katika kanisa alikuwa kwenye uhusiano wa uasherati.

Paulo aliwaambia kwamba Nidhamu ya kanisa siyo kwa ajili ya watu walioko nje ya kanisa, bali kwa wanachama hai wa kanisa (11-12). Kanisa lilikuwa lichukue hatua katika umoja

("mkiwa mmekusanyika pamoja"). Walipaswa wamwondoe huyu mtu kutoka kwenye ushirika wao.

Ikiwa mtu anayeitwa ndugu anafanya dhambi kama wale walioorodheshwa katika mstari wa 11, Wakristo wakatae kabisa kuwa kwenye ushirika pamoja naye. Kusudi ni kuhakikisha kwamba mtu huyo anatambua kuwa yeye siyo Mkristo (hajaokoka) na ni kwa ajili ya dunia itambue kwamba mtu huyu siyo sehemu ya kanisa tena. Hii ni pamoja na kumwondoa katika nafasi yeyote ya uongozi aliyo nayo katika kanisa. Hawezi kushiriki Meza ya Bwana kwa sababu hiyo itamaanisha kwamba yuko karibu sana kwenye ushirika wa Kikristo kuliko hata kushiriki chakula kwa pamoja.

Paulo alikusudia malengo mawili katika kitendo hiki. Lengo moja lilikuwa kanisa liweze kuwa safi (6-7). Haiwezekani kanisa liwe kwenye umoja kama wanachama wake ni watenda dhambi.

Lengo la pili ni kumrejesha mwenye dhambi kwenye wokovu ("roho yake iokolewe").[8] Kama kanisa litaendelea kumkubali kuwa mwanachama wakati akiendelea kutenda dhambi, atajiona kwamba yuko tu sawasawa hana tatizo na uwezekano wa kutubu hautakuwepo. Uwezekano wa kutubu utakuwepo kama hatua za nidhamu ya kanisa zitatekelezwa.

Hatua hii inaitwa "kumpa Shetani mtu huyo" Kulikuwa na kadhia nyingine ambapo Paulo aliwatoa kwa Shetani waalimu wa uongo wa mafundisho ya imani (1 Timotheo 1:20). Mwenye dhambi anapaswa ajitambue kwamba hayuko chini ya baraka na ulinzi wa Mungu. Kama mtenda dhambi yuko nje ya kanisa na ni mtumwa wa Shetani. Maisha ya dhambi yatamharibu kabisa kama hatataka kutubu.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Tito 3:10-11 kwa ajili ya kikundi.

Kama mtu atakuwa anafundisha mafundisho ya uongo ya imani, kanisa linapaswa lijaribu kumrekebisha angalao mara mbili kuhusu mafundisho hayo. Baada ya hapo, inabidi akataliwe. Biblia inatueleza sisi kwamba mtu kama huyu anakuwa tayari ameshakiuka dhamira yake mwenyewe.

Mafundisho ya imani potofu siyo mambo madogo ya mabadiliko katika mafundisho ya imani. Ni a fundisho potofu la imani linalopingana na misingi ya mafundisho ya msingi ya imani ya Biblia. Tusiwe wepesi kumshutumu mtu kwa mambo ya kusikia. Mtu anaweza akawa mpotoshaji kwenye baadhi ya mafundisho yake ya imani na bado akawa anaendelea kuwa ni mfuasi mwaminifu wa Kristo.

► Angalia katika 2 Wathesalonike 3:6, 14-15. Toa ufafanuzi wa maelekezo yaliyotolewa katika aya hizi.

---

[8] 1 Wakorintho 5:5 NENO: Neno: Bibilia Takatifu 2025

## Nidhamu kwa Mchungaji

Mara nyingi wachungaji ni wa kulaumika. Wachungaji mara nyingi wanakuwa kwenye mazingira ambayo wanaweza kushutumiwa kwa uongo. Ni muhimu kwa mchungaji kujenga imani ya watu wake kwa siku zote kuwa mfano mzuri wa kuigwa.

Mashitaka dhidi ya mchungaji hayapaswi kuchukuliwa maanani isipokuwa kuna mashahidi wawili au watatu (1 Timotheo 5:19). Viongozi wa ushirika wa kanisa au dhehebu wana jukumu la kuwafanya wachungaji wawajibike na wanapaswa kuhusika endapo kutahitajika kumchunguza mchungaji au kumuondoa. Wanaweza wakasaidia katika kulifanya kanisa liwe kitu kimoja wakati huduma ya kanisa inapokuwa katika walakini.

► Je, kwa nini dhambi ya mchungaji ni jambo zito sana?

## Mchakato wa Urejesho

Tunapaswa tukumbuke kwamba lengo moja la nidhamu ya kanisa ni kumrejesha mwanachama kwenye wokovu na ushirika. Hakuna ulazima wa kanisa wa kuhakikisha kwamba mwanachama aliyetenda dhambi ameadhibiwa vya kutosha. Wakati mwanachama amejitoa kukiri dhambi yake na kutubu, kanisa linapaswa lianze mchakato kwa ajili ya urejesho.

Katika baadhi ya makosa, kama mwanachama amekiri haraka bila kupoteza nafasi makosa yake na kuirekebisha tabia yake, ataweza kuendelea na ushiriki wake katika kanisa. Makosa mengine mazito yameorodheshwa katika 1 Wakorintho 6:9-10, ikiwa ni pamoja na uasherati, wizi, na ulevi. Mwanachama wa kanisa anayetenda uovu katika mojawapo ya dhambi hizi atapaswa aondolewe kwenye uanachama na nafasi yeyote ya uongozi aliyokuwa nayo.

Mchakato wa urejeshaji huanza wakati mwanachama anapotubu dhambi yake. Kwenye shauri la dhambi nzito zaidi, hawezi kwa mara moja akarudishwa kwenye nafasi yake ya uongozi au ushiriki kama uanachama. Wakati mwingine panahitajika mchakato wa urejeshaji ulio mkamilifu:

### (1) Kukiri

Mwanachama anapaswa kukiri kosa lake kwa wale aliowajeruhi, kwa wale walioshiriki kutenda kosa pamoja naye, na kwa wale walio na mamlaka ya kiroho juu yake.

### (2) Kutengwa

Mahusiano mabaya ni lazima yakomeshwe. Mahusiano ambayo yana ushawishi mbaya ni lazima pia yakomeshwe. Vitu vyote ambavyo vinatumika tu kwa ajili ya kutenda dhambi ni lazima vitupwe. Inawezekana kuna vitu ambavyo vimetumiwa vibaya kusababisha dhambi navyo pia vitahitajika vitupwe. Mwanachama anayehusika anapaswa aonyeshe kwamba hakusudii  tena kurejea kwenye dhambi.

**(3) Kuwajibika**

Hii ni hatua inayochukua muda mrefu. Mwanachama aliyeko katika mchakato wa kurejeshwa anapaswa atoe taarifa mara kwa mara kwa mamlaka ya kiroho ya kanisa, ambayo inaweza ikawa ni mchungaji au baraza la mashemasi. Atapaswa aweze kutoa taarifa ya ushindi dhidi ya majaribu. Atapaswa aonyeshe kwamba yuko makini na mwangalifu katika kutoangukia tena kwenye majaribu.

Uwajibikaji unatakiwa uimarishwe kwa kukutana mara nyingi zaidi na mshauri wa kiroho aliyethibitishwa na mamlaka ya kiroho. Mshauri atakuwa anazungumza na mwanachama mara kwa mara, ikiwezekana kila siku kwa muda. Mshauri atapaswa awe wa jinsia moja na yule anayeshauriwa.

Uwajibikaji utatakiwa uwe angalao miezi kadhaa. Kwenye suala la dhambi ya kimaadili ambayo iliwahusisha wengine, na hasa kama dhambi iliyotendwa iliendelea kwa muda mrefu, uwajibikaji itabidi pia uwe wa muda mrefu zaidi. Kwenye kipindi hiki, mwanachama hataruhusiwa kuongoza au kufundisha kwa njia yeyote ile. Ataruhusiwa kushiriki Meza ya Bwana kama kutubu kwake kumethibitika kwamba kulikuwa ni kweli.

Sababu za kuwepo kwa muda wa uwajibikaji haimaanishi kwamba mwanachama siyo Mkristo. Kama atakuwa ameshatubu, amesamehewa na ameokoka. Muda uliowekwa ni kwa ajili ya kumwezesha kupona kutokana na madhara ya dhambi, kujenga nidhamu thabiti ya kiroho, na kudhihirisha maisha endelevu ya Kikristo.

Biblia inatueleza kwamba mtu hapaswi kuwa kiongozi hadi hapo atakapokuwa na mtazamo wenye sifa njema kwa watu wa nje ya kanisa (1 Timotheo 3:7, 10). Kama mtu atakuwa ameokoka kutokea kwenye maisha ya dhambi ya wazi, dunia inapaswa imwone waziwazi kama Mkristo kwa muda kabla hajaweza kupewa uongozi. Vinginevyo, itaonekana kwamba kanisa linachagua watenda dhambi kuwa viongozi. Kanuni hii inatumika pia kwa mtu ambaye amerejeshwa baada ya kuwa ameanguka katika dhambi.

**(4) Kuthibitishwa**

Huu ni urejesho mkamilifu. Mwanachama sasa anao uhakikisho wa kanisa na anaweza kushiriki kikamilifu kama mwanachama katika jambo au shughuli yeyote ambayo kanisa litampatia afanye. Muda mrefu unaweza kuwa ni muhimu kwa nafasi za uongozi wa juu, hasa kwenye jukumu la mchungaji.

► Elezea muda wa uwajibikaji. Ni kwa jinsi gani unafanya kazi, na lengo lake ni nini?

## Yanayohitajika kwa Unachama wa Kanisa.

Makanisa mengi yana matamko ya mafundisho ya imani ambayo yanapitiliza hata misingi ya mafundisho ya imani ya Ukristo. Maelezo haya ya mafundisho ya imani yanalitofautisha kanisa na makanisa mengine. Makanisa yenye mafundisho ya imani yanayotofautiana wazi yanatambulika kwa majina kama Methodisti, Presbyteriani, Lutherani, Baptisti, au

mengineyo. Kwa kawaida tofauti zilizopo katika makanisa siyo mafundisho ya imani potofu, na mtu hapaswi kuitwa mwenye dhambi kwa sababu tu ya tofauti hizo.

Makubaliano kuhusu maelezo ya mafundisho ya imani ni muhimu kwa ajili ya wanachama wa kanisa kuweza kuabudu pamoja na kushirikiana katika huduma. Kwa hiyo, kanisa linaweza kuwataka wanachama wake kuunga mkono tamko lake la mafundisho ya imani. Hawapaswi kusema kwamba mtu ni lazima aamini mafundisho yao ya imani ili aweze kuwa Mkristo, lakini ni ili kuwa katika umoja na hilo kanisa fulani la mahali au mtaa.

Kama mtu hawezi kuamini mafundisho ya imani ya kanisa fulani, kanisa hilo lina haki ya kumkataa kuendelea kuwa mwanachama wake. Kama mwanachama atafundisha au atataka kuingiza mafundisho ya imani yaliyo kinyume na ya kanisa, anaweza akaondolewa uanachama wa kanisa.

Kama mwanachama ataondolewa kwa sababu ya tofauti za mafundisho ya kiimani ambayo siyo ya msingi kwa Ukristo, hiyo haitakuwa sawa na nidhamu ya kanisa kwa sababu ya mafundisho ya uzushi na dhambi ya asili. Kanisa halipaswi kusema kwamba mtu siyo Mkristo kwa sababu tu hajatimiza masharti ya uanachama.

> "Maandiko Matakatifu yana mambo yote tunayohitaji kwa ajili ya wokovu, ili kwamba chochote ambacho hakitasomwa hapo ndani, au hakiwezi kuthibitika kutokea hapo ndani, hapaswi kuhitajika mwanadamu yeyote kuamini kwamba hicho ni kifungu cha imani au ifikiriwe kwamba kinahitajika au ni muhimu kwa ajili ya wokovu."
>
> \- *Kanuni za dini za Kanisa la Uingereza*

Kama kanisa lina masharti ya uanachama yanayohusisha pamoja na sheria za mavazi, sherehe, au tabia nyingine zozote, mwanachama anaweza kuondolewa kwa kukataa kutimiza masharti hayo. Hii siyo sawa na nidhamu ya kanisa iliyo kwa ajili ya dhambi ya wazi. Kanisa halipaswi kusema kwamba mtu fulani siyo Mkristo kwa sababu tu hayuko tayari kujihusisha na masharti ya uanachama.

► Je, kuna mifano gani ya masharti ya uanachama yameshikiliwa na baadhi ya makanisa lakini hayajashikiliwa na makanisa mengine?

## Uongozi wa Ibada na Ushiriki

Ibada za kuabudu za kusanyiko la kanisa kwa kawaida zinatakiwa ziwe wazi kwa mtu yeyote. Watu wanahitajika waalikwe kuhudhuria.

Kanisa haliwezi kumruhusu mtu mwenye tabia ya kuvuruga aingie humo, kwa mfano mtu ambaye ni mlevi. Kanisa pia haliwezi kuruhusu kuingia mtu aliyevaa mavazi yasiyokuwa na heshima na yaliyovaliwa kwa njia ambayo kwa kweli yanatia au yanaleta aibu. Hata hivyo, ni muhimu kwamba watu wasitengwe kwa sababu ya uvaaji unaotokana na umaskini wao au kwa sababu hawajawa wazoefu na mazingira ya tabia sahihi ya kanisa. Ni janga kubwa wakati watu wanapohisi kwamba hawawezi kuhudhuria kwenye kanisa kwa sababu hawana mavazi mazuri ya kuvaa.

Kama mtu anakuwa ni wa vurugu wakati wa ibada, mchungaji au mtu mwingine yeyote aliyechaguliwa na mchungaji anapaswa kuzungumza naye. Kama atakataa kutoa ushirikiano unaohitajika, asiruhusiwe kuendelea kuwepo kwenye ibada za kanisa.

Wakati mwingine kanisa huruhusu mtu fulani kupiga vyombo vya muziki au kuongoza kuimba ingawaje maisha yake hayana mfano mzuri wa kuigwa. Mtu yeyote anayeongoza kuimba au kupiga vyombo vya muziki mbele ya watu katika kanisa anawakilisha tabia ya kanisa lilivyo. Kama anaishi kwenye dhambi, watu watafikiri kwamba kanisa linamkubali kama Mkristo sahihi, ingawaje anatenda dhambi.

► Je, kanisa linapaswa liwe na mahitaji au masharti ya aina gani kwa ajili ya watu wanaoongoza katika ibada?

## Hitilafu za Kuepuka

Kuna Hitilafu tatu ambazo watu wa kanisa ni lazima waziepuke wakati wanaposhughulikia matatizo yanayojitokeza katika kanisa.

### (1) Kutowiana

Dhambi zingine huonekana zina uzito zaidi kuliko zingine. Wakati mwingine tofauti huonekana kwa sababu ya mitazamo ya kitamaduni. Kanisa linaweza likawa na tabia ya kushughulikia kwa kumaanisha baadhi ya dhambi lakini likaonesha uvumilivu kwa dhambi zingine. Mungu ameliita kanisa kusimama katika ukweli wa maandiko na siyo tu kwa ajili ya kujali maadili ya utamaduni.

Pia kuna kutowiana katika njia ambazo makanisa yanashughulikia watu mbalimbali kwenye kusanyiko la kanisa. Kama mtu anatoka kwenye familia yenye umashuhuri, viongozi wanaweza wakawa waangalifu zaidi katika njia ambayo wanashughulika na tatizo lake; lakini Biblia inatuonya kwamba tusiwe watu wenye kupendelea watu wengine kwa sababu ya hali au hadhi zao (Yakobo 2:1-9).

### (2) Kukosa subira

Wakati mwingine watu katika kanisa hufikiri kwamba tatizo halitatuliwi haraka inavyowezekana. Wanaanza kuongea kuhusu tatizo hilo kwa watu wengine mbalimbali, hata watu walioko nje ya kanisa. Wanakuwa na malalamiko kwamba viongozi wao hawashughuliki na tatizo lililopo. Hali hii inaleta matatizo mengine mapya katika kanisa kwamba inaumiza na kuleta madhara kwenye ushawishi wa kanisa.

### (3) Kukosa upendo

Baadhi ya watu hufurahia kutafuta matatizo kwa watu wengine. Ni wepesi kuamini taarifa za matendo ya uovu yaliyofanyika. Wanawahukumu watu wengine kwa haraka, bila ya kutaka kuelewa. Hawana masikitiko au na majuto kwa dhambi za wanachama wa kanisa. Wamejawa furaha kwamba wanazo taarifa mbaya za kwenda kuelezea. Hawana cha kujali wala masikitiko kuhusu madhara ya ushuhuda wa kanisa.

Kila mchungaji na mwalimu wa Neno anapaswa kuzungumza dhidi ya dhambi ya umbea. Anatakiwa awafundishe watu wake kuchukia umbea au udaku na kukataa kuusikiliza.

Kama mtu anampenda Mungu, kanisa, na ndugu zake wa kiume na kike katika Kristo, atapaswa aione dhambi kama janga. Atapaswa awe na imani kwamba taarifa ya dhambi inayotolewa siyo ya kweli. Na kama taarifa ni ya kweli, atapenda kuona aliyetenda dhambi hiyo akirejeshwa tena. Atatakiwa asaidie katika kuzuia madhara yasilipate kanisa. Hatasambaza taarifa za kupitiliza zisizokuwa na umuhimu.

**Taarifa Saba kwa Muhtasari**

1. Nidhamu ya kanisa ina malengo manne ambayo ni kwa ajili ya kulinda umoja wa kanisa, kusimamia ukweli, kulilinda kusanyiko kutokana na ushawishi mbaya, na kumrejesha tena mwanachama aliyeanguka dhambini kwenye wokovu na ushirika

2. Mwanachama anayetenda dhambi na hataki kutubu hapaswi kutambuliwa kama ni muumini wa kanisa.

3. Kusudi la nidhamu ya kanisa siyo adhabu, bali masahihisho na marejesho.

4. Kanisa halipaswi kumfikiria kila mtu ambaye hakubaliani na mafundisho ya imani yanayotofautiana, na asiyekuwa na sifa ya uanachama kwamba ni mtenda dhambi.

5. Hatua za urejeshaji ni kukiri, kutengwa, kuwajibika na kuthibitishwa.

6. Urejeshaji huchukua muda kwa sababu mwanachama ni lazima apone kutoka katika madhara ya dhambi yake, ajenge nidhamu ya kiroho iliyo na nguvu, na adhihirishe maisha endelevu ya Kikristo.

7. Kanisa ni lazima lijihadhari au lijilinde na kutofuata utaratibu, kukosa subira, na kukosa upendo.

**Kazi za kufanya Somo la 12**

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 12. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.

2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.

3. Kazi ya Kuandika: Marejeo ya maandiko hapa chini yatapaswa yagawanywe miongoni mwa wanafunzi wa darasa. Kila mwanafunzi atahitajika aandike ibara moja inayoelezea aya yake inatueleza sisi tufanye nini.

    - 1 Timotheo 5:13
    - Tito 2:3
    - Wagalatia 5:15, 26
    - Wagalatia 6:1
    - Wakolosai 3:8-9
    - Wakolosai 3:12-15
    - Wafilipi 4:8
    - Waefeso 4:29-32

# Somo la 13
# Tabia ya Kiongozi wa Kikristo

## Changamoto ya Uongozi wa Kikristo

Andiko tunalokwenda kujifunza katika somo hili linahusika mahususi kwa wachungaji na mashemasi, lakini pia kwa viongozi wengine katika kanisa. Mtu yeyote anayefundisha darasa, anayeongoza katika nyumba ya kanisa, au anayeongoza ibada pia ni kiongozi. Watu hao wote ni mfano wa aina ya watu wa kuigwa waliothibitishwa na kanisa. Kwa hiyo, ni muhimu kwamba wawe ni mfano mzuri wa tabia ya Kikristo.

Tabia binafsi ya kiongozi ni muhimu zaidi kuliko hata uwezo wake wa asili alio nao. Mungu humpa kiongozi wa Kikristo uwezo unaohitajika kwa ajili ya huduma.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Timotheo 3:1-7 kwa ajili ya kikundi.

Siyo vibaya kwa mtu kuwa na matamanio ya nafasi ya uchungaji kama anakuwa anayo nia sahihi. Kama atakuwa ni mtu anayetaka apewe heshima na mamlaka au nafasi ya kujipatia faida ya fedha, mtu kama huyu hana moyo wa kichungaji. Anapaswa atamani nafasi ya kuhudumu.

Tuna aya mbili za maandiko kuhusu sifa za wachungaji na mashemasi. Ziliandikwa na mtume Paulo kwa Timotheo na Tito. Timotheo alikuwa kiongozi wa makanisa yaliyokuwepo Efeso; Tito alikuwa kiongozi wa makanisa ya Krete. Walikuwa na kazi ya kuteua wachungaji kwa ajili ya kila kanisa la mtaa.

Jaribu kufikiria ilikuwaje kwa mtu kuwa mchungaji katika karne ya kwanza ya kanisa! Alikuwa hajawahi kuwa na mafunzo ya kitaaluma. Hakukuwa na vitabu kuhusiana na huduma kwa ajili yake ili ajifunze. Hakuwahi kuwa na nafasi ya kuangalia wanavyofanya wachungaji wengine. Hakuwahi kuwa hata na nafasi ya kuangalia maisha ya kanisa kwa muda mrefu kwa sababu kanisa lilikuwa jipya. Hata sehemu kubwa ya Agano Jipya ilikuwa bado kuandikwa.

Paulo alimwambia Timotheo jinsi ya kupata heshima kutoka kwa watu wake. Alimtaka awe kielelezo katika usemi, na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi (1 Timotheo 4:12). Mchungaji hapewi heshima kwa kudai aheshimiwe.

► Je, ni kwa jinsi gani mchungaji hupata heshima?

Mtume aliwaeleza Timotheo na Tito sifa zinazohitajika kwa ajili ya kuwa mchungaji. Sifa nyingi zimerejea kwenye tabia na kukomaa Kikristo kuliko vipaji au uwezo binafsi wa mtu. Kwa hiyo, kila Mkristo anapaswa kutiwa moyo kusitawisha sifa hizo.

## Sifa za Wachungaji

**(1) Asiye na lawama**

Mchungaji hapaswi kuwa mtu anayeonekana na hatia au anayetenda mambo ya uovu. Mchungaji hawezi kumwongoza mtu mwingine afanye jambo sahihi kama yeye mwenyewe hafanyi mambo yaliyo sahihi. Mchungaji ni lazima awe mtu ameonyesha tabia endelevu ya Kikristo kwa kipindi cha muda mrefu. Jambo hili ni muhimu ili kwamba kanisa liweze kumwamini na kuwa na ushuhuda mzuri katika jumuiya.

**(2) Mume wa mke mmoja**

Katika maeneo mengi ya dunia, ndoa ya wake wengi ni utamaduni wa kawaida. Mpango wa Mungu ni kwa mwanamume kuwa na mke mmoja. Wachungaji wanapaswa waweke mfano huo.

**(3) Kuwa Macho**

Mchungaji ndiye mlinzi wa kusanyiko lake. Anapaswa awe makini na mafundisho ya dini ya uongo na ushawishi mbaya. Ni lazima awafundishe watu wake ili waweze kuwa salama katika mafundisho yao mbalimbali ya imani. Ni lazima awe tayari kuwaonya watu wake kuhusiana na hatari yeyote ya kiroho.

► Je, itatokea nini kama mchungaji hana habari na hatari za kiroho wanazokutana nazo watu wake?

**(4) Anayejitawala**

Mchungaji ni lazima awe makini kuhusiana na huduma yake. Hapaswi awe mtu anayelipuka ambaye hufanya maamuzi ya pupa au ya haraka sana. Anapaswa awe na uwezo wa kufikiri akiwa ametulia kuhusu masuala nyeti. Hapaswi kuruhusu akili yake ivurugwe na mambo ya binafsi, starehe, au majaribu.

**(5) Anayeheshimika**

Mchungaji anapaswa awe na tabia ya utaratibu. Hapaswi kuonyesha tabia ambayo haistahili. Anapaswa ajifunze jinsi ya kuonyesha heshima na unyenyekevu kwa misingi ya tamaduni za mahali ambapo huduma yake ipo.

> "Kuhubiri injili, pamoja na uangalizi wa kichungaji ambao unahusiana na ofisi ya huduma, ni njia ya kiungu iliyowekwa kwa ajili ya kuwabadilisha wenye dhambi na ujenzi wa maadili wa kiroho wa waumini. Kwa hiyo ni sababu kuu muhimu kwamba Mungu anahitaji kufanya uteuzi wa maajenti wake mwenyewe, na hasa kuwaita kwenye huduma yake."
>
> - John Miley, *Christian Theology*

**(6) Mkarimu**

Mchungaji anatakiwa awe mtu anayewajibika na mahitaji ya watu wengine. Anapaswa awe tayari kushirikishana katika mambo ya ukarimu. Anapaswa awe rafiki na mwenye msaada kwa watu hata kwa watu ambao anakutana nao kwa mara ya kwanza.

**(7) Ajuaye kufundisha**

Mchungaji ni lazima awe na uwezo wa kuelezea ukweli ili watu waweze kuulewa. Ni lazima achukue jukumu la kusoma na kujielimisha yeye mwenyewe.

**(8) Asiwe mlevi**

Mchungaji asiruhusu yeye mwenyewe kushawishiwa na vinywaji vya kulevya. Hapaswi kamwe kufanya kama mtu ambaye ana uraibu na ulevi. Kanuni hii inahusiana na kitu kingine chochote ambacho kina madhara yanayofanana.

**(9) Asiwe mgomvi bali awe mpole**

Mchungaji asitake kupeleka suala kwa njia vitisho vya kutumia nguvu. Hapaswi kuwa tayari kumwumiza mtu yeyote anayemuudhi au anayemkosea. Ona pia 2 Timotheo 2:24-25.

► Je, ni njia zipi sahihi kwa mchungaji za kuweza kuonyesha aina sahihi ya hasira au ghadhabu anayoweza kuwa nayo?

**(10) Asiwe na tamaa wala mpenda fedha**

Watu wa dunia hii hubadili wayasemayo ili kupata faida. Watu kwenye nafasi zao mbalimbali kama wanasheria, wafanyabiashara, au wanasiasa wanajaribiwa kuubadili ukweli kwa ajili ya kuwafurahisha watu. Mchungaji pia hujaribiwa, kwa sababu ukweli wa Neno la Mungu haumfurahishi kila mtu. Mchungaji ni lazima awe mwaminifu kwenye ukweli aidha kama unamfaidisha kifedha au la.

Mchungaji atapenda kuona huduma ya kanisa ikiwezeshwa kifedha. Ni lazima aongoze kanisa kufanya kazi kama familia inayojali kwa ajili ya wanachama wake, kuliko kila siku kufikiria ni nini watakachoweza kumpa.

**(11) Aweze kuisimamia nyumba yake mwenyewe vizuri**

Uwezo wa mchungaji wa uongozi ni lazima uthibitike kuanzia nyumbani. Atapaswa awe na uongozi kwa watoto wake. Kama hawezi kuiongoza nyumba yake mwenyewe, hatakuwa na uwezo wa kuliongoza kanisa. Hii haijumuishi watoto ambao wameshakuwa watu wazima wanaojitegemeza wenyewe na ambao hawako kwenye mamlaka yake kwa sababu bado hawawajibiki kwa ajili yao tena.

> "Mwenyezi Mungu, Baba yetu wa mbinguni, ambaye amekupa wewe mapenzi mema ya kufanya mambo haya yote, akupe pia nguvu na uwezo wa kutimiza mambo yote; na kwamba akamilishe ndani yako kazi njema ambayo ameianza, na kwamba uweze kupatikana mkamilifu na usiyelaumika katika wakati ujao, kupitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Amen."
>
> - "Kusimikwa kwa Maaskofu,"
> *Kitabu cha Sala ya jumuiya*
> *(Book of Common Prayer)*

**(12) Asiwe mtu aliyeokoka karibuni.**

Kama mtu atawekwa kwenye nafasi ya mamlaka kwa haraka sana, ni rahisi kushawishika kuwa na kiburi. Kiburi ndiyo dhambi iliyomsababisha

Shetani kuanguka. Upandishwaji kwenye ngazi nyingine ya mamlaka unapaswa ufanyike polepole ukiambatana na uzoefu.

► Je, kunakuwa na uharibifu gani kama atawekwa kwenye mamlaka kwa haraka na akawa hafanyi vizuri?

**(13) Awe na sifa njema**

Kabla mtu hajateuliwa kuwa mchungaji, ni lazima awe mtu mwenye sifa njema miongoni wa watu nje ya kanisa. Wanapaswa waelewe kwamba ni mtu wa ukweli na mwaminifu katika yote ayafanyayo. Kama atakuwa ni mtu ambaye hakuwa na sifa nzuri kabla ya kuokoka, patahitajika awe na muda maalumu wa kutengeneza sifa zake kabla hajafanyika kuwa mchungaji.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Tito 1:5-11 kwa ajili ya kikundi.

Sifa nyingi za mchungaji zilizoorodheshwa katika Tito pia zimeorodheshwa kwenye kifungu cha kuanzia 1 Timotheo.

► Je, kuna sifa gani nyingine za ziada za mchungaji zilizoko kwenye kifungu kilichoko katika Tito?

Kifungu kinasisitiza juu ya uwezo wa mchungaji kudhibiti mafundisho potofu ya imani. Mchungaji ni lazima awe ameelimishwa vizuri na kwa upeo mkubwa kuhusu mafundisho ya imani ya kweli na awe na uwezo wa kuyaelezea kwa ushawishi mkubwa. Lengo ni kuwasahihisha wale walioko kwenye mafundisho ya imani potofu, na jambo lililo muhimu zaidi ya hapo, ni kulilinda kusanyiko katika kuingizwa kwenye upotofu.

## Sifa za Mashemasi

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Matendo 6:1-6 kwa ajili ya kikundi. Je, kuna tatizo gani lililoelezwa kwenye kifungu hiki?

Mashemasi wa mwanzo waliochaguliwa mara tu baada ya Pentekoste. Mitume walihitaji kuwa na fokasi yao kwenye maombi na kuhubiri. Watu wapatao saba waliteuliwa katika mambo ya kulisimamia kanisa. Shemasi humsaidia mchungaji katika mambo yote yanayohusiana na huduma ya kanisa. Shemasi anaweza akawa ni mhubiri, lakini pia siyo lazima.

► Je, sifa za mashemasi wa mwanzo zilikuwa ni nini?

Sifa za mashemasi wa mwanzo zilikuwa kwamba walikuwa na sifa ya kuwa watu wa ukweli na waliojazwa na Roho Mtakatifu na hekima. Wangekuwa wanasimamia pesa kwa ajili ya kanisa, kwa hiyo sifa ya kuwa mkweli ilikuwa muhimu. Kazi zao zilikuwa na matokeo ya kiroho katika kanisa, kwa hiyo ilikuwa ni muhimu kwao kuwa watu waliokuwa wamejazwa Roho Mtakatifu kwa ajili ya kupata uongozi wake, kupokea upako, na usafi. Walishughulika na hali nyingi zilizokuwa ngumu, kwa hiyo hekima ilikuwa jambo la muhimu.

Mtume Paulo aliorodhesha baadhi ya sifa kwa ajili ya mashemasi:

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Timotheo 3:8-13 kwa ajili ya kikundi.

**(1) Anayeheshimika**

Shemasi anapaswa awe mtu ambaye anaheshimika kwenye mahusiano yake na familia, marafiki, na jumuiya.

**(2) Mkweli na mnyofu**

Shemasi anapaswa awe mtu ambaye anaaminika katika yale anayosema. Atasikia malalamiko kuhusu watu ndani ya kanisa na atasikia maoni mengi sana kuhusu matatizo ndani ya kanisa. Anapaswa awe mtu ambaye ni mkweli.

**(3) Asiye mlevi**

Shemasi hapaswi awe mtu ambaye amedhurika na ulevi. Tabia yake inabidi iwe ya kuheshimika na iliyo thabiti.

**(4) Asiye na tamaa**

Shemasi atawajibika kutunza fedha kwa ajili ya kanisa na kujali mahitaji ya watu walioko ndani ya kanisa. Hapaswi awe mtu ambaye anajaribu kujipatia faida yeye mwenyewe kutoka katika huduma yake.

**(5) Anayeshika imani kwa dhamira safi**

Wakati mtu anapoanguka katika dhambi, mara nyingi huanza kuamini mafundisho potofu ya imani. Kama mtu anaishi kwenye ushindi wa kiroho, atakuwa na nafasi kubwa zaidi ya kushikamana na mafundisho ya kweli ya imani.

**(6) Apimwe kwanza uwezo wake au uzoefu wake**

Kabla mtu hajapewa nafasi ya kuwa Shemasi, anapaswa awe na nafasi ya kuonyesha kwamba ana hekima na ni mwaminifu katika huduma. Viongozi wenye hekima watawapa watu wao nafasi za kutumika kabla ya kuwapa nafasi za mamlaka.

► Je, kuna mifano gani ya njia ambazo mtu anaweza kusaidia huduma ya kanisa bila ya kuwa amepewa nafasi ya mamlaka?

**(7) Awe na mke mwaminifu.**

Huduma ya Shemasi inapata madhara kama mke wake atakuwa ni mtu wa uvumi na siyo mfano wa Mkristo mwema.

**(8) Awezaye kusimamia nyumba yake vyema**

Kama ilivyo kwa mchungaji, Shemasi anapaswa aweze kuimiliki familia yake vyema.

### Kipaumbele cha Kikundi kinachojituma.

Kanisa ni kikundi cha watu walioamini ambao wameweka msimamo wao kwa Mungu na kila mtu na mwenzake, wakijipanga kwa ajili ya kusudi la kukamilisha kazi ya umisheni ya kanisa la mtaa. Kazi na rasilimali za kufanya huduma iendelee hutoka katika kikundi hicho. Pasipokuwepo na kikundi hicho, kanisa halipo.

Mgeni ambaye anaingia katika eneo la biashara ni muhimu kwa sababu anaweza kuwa mteja. Vivyo hivyo, mgeni yeyote anayeingia kwenye kanisa ni muhimu kwa siku zijazo, anaweza kuwa sehemu ya kikundi kinachojituma. Mtu muhimu sana kwenye biashara ni yule mteja wa kila siku. Mtu muhimu sana kwenye kanisa ni yule ambaye anajitoa kwa kanisa.

Kwa hiyo, nafasi za wafanyakazi katika kanisa zinapaswa kutumikia kikundi kilichojitolea. Kila mchungaji na mwalimu atakuwa na kusudi la kuwatumikia wanachama wa kikundi na kuwavutia watu wengine wengi wajiunge nacho. Kikundi hukua katika idadi wakati watu wanapokuwa wanaokoka na wamejituma kwa kanisa, au wakati ambao watu waliokwishaokoka wanapojitambua kwamba wanahitaji wajiunge na kikundi hicho. Wafanyakazi wa kanisa watapaswa wajifunze mahitaji ya wanachama wa kikundi na kufanya uanafunzi au ufuasi, mwelekeo wa kiroho, mafunzo ya huduma, na aina nyingine zote kwa ajili ya ushirika. Watapaswa wakiongoze kikundi katika kufanya kazi kwa pamoja ili kukidhi mahitaji yote ya wale walioko kwenye kikundi.

**Kama familia ya watu wenye imani, kanisa wanatumia rasilimali watu na kupata rasilimali za Mungu vya kukidhi mahitaji ya kila aina kwa ajili ya wale walioko kwenye ushirika, wakidhihirisha kwa ulimwengu hekima ya Mungu katika kila kipengele cha maisha na kuwakaribisha watu ambao hawajaokoka ili waokoke na kuingia kwenye familia.**

► Je, itaonekanaje kwa viongozi wa kanisa kuwa na kipaumbele cha kukuza kundi la waumini ambalo linajitoa kwa kwa kila mmoja?

### Kipaumbele cha Kiroho cha Kanisa.

Ingawaje masuala ya kifedha ni muhimu kwa ajili ya kanisa (kwa ajili ya uwezeshaji wa shughuli za kichungaji, uangalizi wa kusanyiko, na shughuli nyingine za huduma za ndani), kanisa linapaswa kimsingi kulenga kwenye vipaumbele vya kiroho vya uinjilisti na kuwafanya watu kuwa wanafunzi au wafuasi. Kimsingi mchungaji anapaswa awe ndiye kiongozi wa kiroho. Hii ina maana kwamba mchungaji asibebe mzigo mzito kupita kiasi wa kufanya biashara. Jambo lililo bora ni kwa wanachama wa kanisa kuwa wafanyakazi au biashara ambako wataweza kutoa zaka. Kwa biashara zinazoendeshwa na kanisa, mashemasi waaminifu wanaokubalika watapaswa wachukue jukumu kubwa la kuwajibika katika biashara hiyo. Mashemasi wa mwanzo waliteuliwa ili mitume waweze kutumia muda wao mwingi kwenye maombi na kwa ajili ya huduma ya Neno (Matendo 6:2-4).

## Sifa za Mchungaji Anayeliongoza Kanisa Vizuri

► Jadili umuhimu wa kila sifa, ukianzia na swali, "Je, kwa nini sifa hii ni muhimu?"

1. Uaminifu wake haujagawanyika kwa mashirika mengine.
2. Yuko tayari kujenga timu ya huduma na kutumia uwezo na vipaji vya watu wengine.
3. Anaongoza kusanyiko lake kushirikishana maisha kama familia ya kiroho, inayowajibika na mahitaji yote.
4. Analihudumia kanisa lake kwa upendo kwa ajili ya Mungu na watu, na siyo kwa ajili ya faida binafsi.
5. Vipaumbele vya kiroho kama vile ibada, uinjilisti, na kukua kiroho ni lengo la huduma yake.
6. Watu wake wanamwamini na kuwa na uhakika naye.
7. Yuko tayari kulijenga kanisa kama taasisi ya kudumu ambayo siyo mali yake
8. Analiongoza kanisa katika kukua, akifundisha kuhusu zaka na ushirika wenye kujali mahitaji ya wengine.
9. Ni mkweli katika mambo yote, ikiwa ni pamoja na matumizi ya fedha.
10. Anaonyesha uwezo wa kumiliki fedha pamoja na watendakazi.

## Sifa za Kiongozi wa Mradi wa Huduma

Mtu anayechaguliwa kuongoza mradi wa biashara wa kanisa anapaswa awe na sifa hizi. Viongozi wa kanisa wanapaswa wafanye kazi ya kukuza sifa hizi kwa wanachama wake ambao wataweza kusaidia katika jukumu la kanisa na waingizwe kwenye timu ya viongozi.

► Jadili umuhimu wa kila sifa, ukianzia na swali, "Je, kwa nini sifa hii ni muhimu?"

1. Ni mwaminifu kwa kanisa la mtaa kwa mahudhurio yake, hutoa zaka, anashiriki na anao ushuhuda wa Kikristo unaoaminika.
2. Tayari anakuwa amewekeza juhudi zake na shauku yake katika kanisa la mtaa.
3. Anao uaminifu wa kutosha na hisia ya hali ya juu ya maadili.
4. Tayari anakuwa ameshaonyesha uwezo wa kuanzisha mambo na motisha wa kufanya vizuri kwa kadri inavyowezekana.
5. Binafsi ni mtu mwenye nidhamu, amehamasika, na siku zote akiendelea kuwa mzuri zaidi.
6. Anadhihirisha uwezo wake na kipaji cha kupanga na kuwaongoza watu wengine, siyo tu uwezo wa kufanya kazi wakati anapoelekezwa na mtu mwingine.

7. Anao uzoefu wa kutosha wa kutekeleza jukumu lake linalomhusu katika huo mradi.

## Taarifa Saba kwa Muhtasari

1. Tabia binafsi ya kiongozi ni muhimu zaidi kuliko hata uwezo wake wa asili aliyo nao.
2. Mtu anapaswa aoneshe sifa za Ukristo kwa kipindi cha muda fulani kabla ya kuwa kiongozi.
3. Mtu aliye na majukumu katika kanisa ni mfano wa tabia kwa ajili ya kanisa.
4. Usimamizi wa fedha za kanisa ni muhimu kwa ajili ya kanisa, kumwezesha mchungaji, kuwasaidia wahitaji kwenye kusanyiko, na kusaidia huduma nyingine za ndani.
5. Kanisa kimsingi linapaswa kulenga kwenye vipaumbele vya uinjilisti na kufanya uanafunzi au ufuasi.
6. Viongozi katika kanisa wanapaswa kulenga katika kuendeleza kikundi cha watu ambao wamemaanisha na wamejitoa kabisa kwa ajili ya kanisa.
7. Kanisa ni lazima liwe imara kama taasisi ya kudumu ambayo ni mali ya kusanyiko.

## Kazi za kufanya Somo la 13

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 13. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.
2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.
3. Kazi ya Kuandika: Tafakari Ezekieli 34:1-10 kisha andika sentensi chache ambazo zinatoa muhtasari wa ujumbe wa kifungu hiki.

# Somo la 14
# Karama za Kiroho

**Tafsiri ya Karama za Kiroho**

Karama ya kiroho ni uwezo aliopewa mtu aliyaemini kutoka kwa Roho Mtakatifu kwa ajili ya matumizi katika huduma ya kanisa. Ni kazi ya Roho Mtakatifu kupitia kwa mtu aliyeamini, lakini bado mtu aliyeamini hufanya uchaguzi wa jinsi ya kutumia karama yake na inawezekana pia akaitumia kwa njia isiyofaa. Karama ya kiroho siyo sawa na uwezo wa asili wa mtu, lakini karama zinaweza zikaambatana na uwezo wa asili wa mtu husika na hauwezi kutofautishwa kirahisi.

## Kuorodhesha Karama za Kiroho

Karama za kiroho na majukumu ya huduma yameorodheshwa katika maeneo mbalimbali ya Agano Jipya. Orodha hizi ziko sawa lakini hazifanani. Biblia haijatupa sisi orodha ya karama zote za kiroho

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Waefeso 4:7-12 kwa ajili ya kikundi.

Aya za 7-8 zinatuambia kwamba neema ya Mungu inatolewa kwa kila mtu kwa njia ya karama za kiroho. Inavyoonekana mtume hazungumzi kuhusu neema ya wokovu, kwa sababu kwenye aya ya 11 ameorodhesha majukumu ya huduma mbalimbali ambazo Mungu ametoa.

Mungu anawaita watu kwa huduma maalumu na anatoa karama za kiroho wanazozihitaji. Paulo aliorodhesha baadhi ya huduma, badala ya kuorodhesha karama za kiroho kama alivyofanya katika 1 Wakorintho. Majukumu ya huduma yaliyoorodheshwa ni mtume, nabii, mwinjilisti, mchungaji na mwalimu. Kwa hakika, haijamaanisha kuwa hii ni orodha kamili iliyokamilika ya majukumu ya huduma zote.

### Mtume

Mitume walikuwa wanachaguliwa maalumu kuliendeleza kanisa baada ya huduma ya Yesu kukamilika hapa ulimwenguni. Walijulikana kwa miujiza iliyotendeka katika huduma zao (2 Wakorintho 12:12). Wote walimjua Yesu kibinafsi wakati wa huduma yake hapa ulimwenguni (1 Wakorintho 9:1, Matendo 1:21-22).

Katika kitabu cha Ufunuo tulisoma kwamba misingi kumi na miwili ya jiji iliwakilisha mitume kumi na wawili, ikimaanisha kwamba walikuwa ni watu wa kipekee kabisa katika historia ya kanisa (Ufunuo 21:14). Aya nyingine zinazoonyesha kwamba kuna mitume kumi na wawili tu ni Mathayo 10:2 na Matendo 1:26. Yuda 17 anaonyesha kwamba mitume walikuwa ni kwa siku zilizopita. Hakuna tena mitume walio hai kwa wakati wa sasa.

**Nabii**

Baadhi ya watu wanadhania kwamba unabii ni utabiri wa mambo yajayo, lakini Agano Jipya linarejelea kwenye kuhubiri kama unabii. Kwenye Agano la Kale, unabii mara nyingi ulijumuisha utabiri, kwa sababu hiyo ilikuwa ndiyo njia mojawapo ambayo nabii alithibitisha kwamba ujumbe wake ulikuwa unatoka kwa Mungu. Kwenye nyakati za Agano la Kale, mambo mengi yaliyoko kwenye Biblia yalikuwa bado hayajaandikwa.

Nabii ni mtu anayepokea ujumbe kutoka kwa Mungu, ambao unaweza au usiweze kujumuisha utabiri. Mamlaka ya ujumbe wake kwa kawaida ni Biblia.

**Mwinjilisti**

Neno *mwinjilisti* linatokana na neno *injili.* Mwinjilisti ni mtu anayewasilisha injili, aidha kwa watu binafsi au kwenye kusanyiko. Kila Mkristo anapaswa kushirikisha injili, lakini baadhi wamejaliwa kipekee kupata karama kwa ajili ya kazi hiyo. Mchungaji anapaswa kufanya uinjilisti kama sehemu ya huduma yake (2 Timotheo 4:5).

**Mchungaji**

Mchungaji siyo tu mhubiri, bali pia ni mtu ambaye hutoa malezi ya kiroho kwa kundi maalumu la watu.

**Mwalimu**

Katika kanisa, mwalimu ni mtu anayeelezea ukweli wa kibiblia na wa kiroho kwa watu wengine. Kila mchungaji anapaswa awe mwalimu (1 Timotheo 3:2, Tito 1:9), lakini watu wengine ambao siyo wachungaji wamejaliwa pia kupata karama za kuwa waalimu.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma Warumi 12:6-8 kwa ajili ya kikundi.

Hapa mtume anasema kwamba mtu anapaswa kuelekeza juhudi zake katika karama ambayo Mungu amempa, badala ya kutawanya juhudi zake na muda wake kwenye huduma nyingi tofauti.

Baadhi ya maelekezo maalumu hutolewa kwa ajili ya aina fulani ya huduma. Kwa mfano, mtu anayeongoza ni lazima awe na bidii, na siyo kuongoza tu anapotaka kufanya hivyo, bali kuhakikisha kwamba majukumu yanatekelezwa wakati wote. Mtu anayetoa hapaswi kufanya hivyo katika njia inayomfanya aonekane bali atoe katika njia ya kawaida. Mtu anayeonesha huruma, kwa ajili ya kusaidia na hitaji la dharura anapaswa afanye hivyo kwa furaha, na siyo kwa shingo upande.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 12:28 kwa ajili ya kikundi.

Inaonekana Paulo hakukusudia kutoa orodha kamili ya karama zote au majukumu ya huduma zote katika aya hii. Kwa mfano, hakuwataja wachungaji kwenye orodha hii, ingawaje aliwataja kwenye orodha iliyoko kwenye Waefeso.

Mitume, manabii na waalimu walishajadiliwa mwanzoni katika somo hili.

Baadhi ya watu wanaitwa kwenye huduma za miujiza na uponyaji. Kila mtu aliyeamini ana fursa ya kuomba kwa ajili ya miujiza, na Mungu atajibu kwa ile imani. Hata hivyo, baadhi ya watu walioamini wanazo karama za kutambua mapenzi ya Mungu na kutumia imani kwa ajili ya miujiza.

Baadhi ya watu wanazo karama za usaidizi. Wanaona mahitaji kwa haraka zaidi kuliko watu wengine. Wanatambua nafasi za kutoa msaada kwa mahitaji ya watu binafsi au kwa kazi ya kanisa. Wanakuwa na uwezo wa aina mbalimbali wa kivitendo.

Baadhi ya watu wamepewa uwezo wa aina mbalimbali wa kuongoza na kutawala. Watu wengi wanafikiri kwamba viongozi ni watu muhimu zaidi, lakini uongozi utakuwa hauna thamani bila ya karama nyingine katika kanisa.

Karama ya lugha imeorodheshwa mwisho. Inawezekana mtume alitaka kusahihisha wale wanaofikiria kwamba hiyo ilikuwa ni karama muhimu sana kuliko nyingine.

## Kanuni kutoka kwa Petro

Mtume Petro alielezea kwa kifupi kanuni muhimu zaidi kuhusu karama mbalimbali za kiroho.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Petro 4:10-11 kwa ajili ya kikundi.

Tunaweza tukaangalia angalau pointi sita muhimu kuhusu karama za kiroho katika aya hizi.

1. Waumini wameaminiwa karama za kiroho na Mungu. Kwa hiyo, wanawajibika kuzitumia kwa ajili ya Mungu na siyo kama wamiliki binafsi. Tunawajibika kwa Mungu kwa ajili matumizi yetu ya karama za kiroho.
2. Karama za kiroho zinahitajika zitumike kwa ajili ya watu wengine. Haziko kwa ajili ya kujikuza binafsi au kupata faida.
3. Neema za Mungu ni za namna tofauti ("namna nyingi"). Kuna mchanganyiko wa aina nyingi wa karama.
4. Kuzungumza kwa mtu kunatakiwa kuendana sawa na Biblia.
5. Mtu anapaswa ategemee nguvu kutoka kwa Mungu anapokuwa anafanya huduma.
6. Huduma zote zinapaswa ziwe na lengo la kumtukuza Mungu.

## Kanuni kutoka kwa Paulo

Kanisa la Korintho lilikuwa limebarikiwa kuwa na karama za kiroho nyingi. Walikuwa na kutoelewana, kwa hiyo, mtume Paulo akawapa ufafanuzi kuhusu karama za Roho Mtakatifu kwenye 1 Wakorintho 12-14.

Sura hizi za Maandiko zinatufundisha sisi kanuni nyingi kuhusu karama za kiroho. Kanuni chache zifuatazo zimeandikwa hapa kwa ajili yetu kujifunza.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 12:1-3 kwa ajili ya kikundi.

**(1) *Kanuni ya kupima fundisho la imani.* Mambo ya kiroho yanayofanyika yanatakiwa kufanyiwa tathmini kwa ule ukweli tunaoufahamu.**

Waumini wa Korintho kabla ya hapo walikuwa wanaabudu miungu. Miungu haina uwezo wa kuongea lakini mapepo *(au maroho machafu)* yanaongea. Wafuasi wengi wa dini za kipagani wanajiweka wazi wenyewe kwa ajili ya matendo ya mapepo. Wanaelekea kufikiri kwamba uzoefu wowote wa kiroho ni mzuri. Wanatafuta kupagawa na kupoteza akili au mihemuho ya kiuwazimu. Wanafurahia kuwa chini ya mapepo, hata kama itawafanya kuongea au kufanya matendo kwa njia ambayo ni ya kichaa au maneno machafu.

Mtume alionya kwamba hakuna mtu yeyote anayeongea kwa Roho Mtakatifu atakayesema mambo mabaya kuhusiana na Yesu. Kama maroho machafu yakichukua umiliki wa ibada, itawasababishia watu kutomheshimu Mungu kwa mambo wanayofanya na kunena. Roho Mtakatifu hawezi kuongoza katika njia ambayo haitamheshimu Mungu.

Hatupaswi kudhania kwamba shughuli za kiroho ni kitu kizuri kwa sababu tu ni za kupita akili zetu. Kipimo hapa ni kulinganisha na 1 Yohana 4:1-3. Kama roho anasema kitu kilicho kinyume na Neno la Mungu, hakipaswi kukubalika.

> "Siyo kila mtu aongeaye katika Roho ni nabii, ila kama tu yuko katika njia za Bwana. Kwahiyo kutokana na njia zake nabii wa uongo na wa ukweli atajulikana."
>
> \- *Didache*
> (iliandikwa kwenye karne ya kwanza ya kanisa)

► Je, ni dini gani zinazoruhusu mapepo au maroho machafu kumiliki watu waabuduo?

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 12:4-11 kwa ajili ya kikundi.

**(2) *Kanuni ya karama mbali mbali:* Roho Mtakatifu anafanya kazi kwa kila mtu aliyeamini, lakini katika njia zinazotofautina.**

Aya hizi zinaweka msisitizo kwamba Roho Mtakatifu aliye mmoja tu hufanya kazi kwa kutumia njia mbalimbali. Anachagua jinsi ya kugawa karama za kiroho. Kila mtu aliyeamini ana angalau karama moja ya kiroho. Hakuna hata mtu mmoja mwenye kuwa na kila karama.

Mwanachama wa kanisa anapaswa atumie karama yake ili kuupa faida mwili wa Kristo. Mungu hakutoa karama kwake kwa ajili ya kujifaidisha yeye mwenyewe.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 12:12-26 kwa ajili ya kikundi.

**(3) *Kanuni ya mwili*: Kila mwanachama wa kanisa ni muhimu, na kila mmoja anamhitaji mwenzake.**

Mtume alilinganisha wanachama wa kanisa na viungo vya mwili. Wana uwezo na makusudi tofauti. Hakuna kiungo cha mwili kinachofikiria kwamba ni lazima kifanane na kingine ili kiwe katika mwili. Kwa mfano, sikio haliwezi kufikiri ni lazima liwe jicho ili liweze kuwa

kwenye mwili. Hakuna karama fulani ambayo mtu ni lazima awe nayo kwa ajili ya kuwa kwenye mwili.

Hakuna mwanachama wa kanisa anayepaswa kufikiri kwamba kwa sababu ya karama zake hawahitaji tena wanachama wengine. Mwili hauwezi kufanya kazi bila ya kuwa na viungo vyake yote.

Karama nyingine hupata nafasi ya kujulikana zaidi kuliko karama nyingine. Watu hufikiri kwamba karama fulani za kiroho ni alama au ishara ya hadhi ya kiroho. Mungu huchagua ni kwa jinsi gani atoe hizo karama za kiroho. Hakuna mtu aliye bora au muhimu zaidi kuliko mtu mwingine kwa sababu ya zawadi fulani aliyo nayo.

► Je, utasemaje kwa mtu anayefikiri kwamba mtu anayehubiri ni wa kiroho zaidi kuliko mtu anayeshughulika na kufanya usafi wa jengo la kanisa?

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 12:27-31 kwa ajili ya kikundi.

**(4) *Kanuni ya majukumu ya huduma*: Mungu humpa kila mwanachama wa kanisa kile anachokihitaji kwa ajili ya kukamilisha kusudi la huduma yake maalumu.**

Sehemu hii ya maandiko inatoa muhtasari wa sura ya 12. Mungu anawaita watu kwa kusudi la kukamilisha huduma mbalimbali. Huduma haiko kwa ajili ya mtu kuitumia kwa kujikuza yeye mwenyewe, bali kwa kulihudumia kanisa.

*Mwalimu wa darasa atapaswa asome maswali yaliyoko katika 1 Wakorintho 12:29-30, na darasa linapaswa litoe majibu. Kwa mfano, wakati kiongozi wa darasa anapolisoma swali "Je! Wote ni mitume?" darasa linatakiwa lijibu: "Hapana."*

Kwa kuwa huduma zinatofautiana, karama nazo ni tofauti. Paulo aliuliza msururu wa maswali, kila moja likitoa jibu kwamba ni "Hapana." Anaelezea kwa uwazi kwamba hakuna karama inayotegemewa kukaa kwa kila mtu aliyeamini.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 13 kwa ajili ya kikundi.

**(5) *Kanuni ya Upendo*: Upendo ni kipaumbele cha milele, na karama za kiroho siyo za kudumu.**

Aya tatu za mwanzo zinaonyesha kwamba upendo ukikosekana hatuwezi tukafidia kwa vipaji vya asili, karama za kiroho, na dhabihu binafsi.

Kwa kujipima wewe mwenyewe, jaribu kuliweka jina lako badala ya upendo kwenye aya ya 4-7 na uangalie ni kwa jinsi gani hapo unaingia vizuri.

Aya ya 11 siyo wito wa kukua. Mtume alilinganisha maisha yetu ya hapa duniani na wakati wa utotoni na akalinganisha maisha ya mbinguni na wakati wa utu uzima. Upo wakati fulani ujao ambao tutakuwa hatuhitaji vitu ambavyo tunavihitaji kwa sasa. Unabii na karama au vipawa vya maarifa vinahitajika kwa sasa kwa sababu ufahamu wetu bado haujakamilika. Kwenye umilele, karama za kiroho zote zitakuwa hazihitajiki tena na zitawekwa mbali kama

vile ni "vitu vya utotoni." Hata imani na matumaini kuna siku ambayo vitakuwa havina umuhimu tena kwa sababu kila kitu kitakuwa kimekamilishwa, lakini upendo utakuwa bado ni wa thamani kuu.

**Sura ya 14 ya 1 Wakorintho inaweka msisitizo kwenye kanuni moja: kanuni ya mawasiliano.** Kweli nyingine zote zimefundishwa kwenye sura hii, lakini mara nyingi mtume alifafanua na kuelezea kwa mifano au vielelezo kuhusu kanuni hii.

**(6) *Kanuni ya mawasiliano*: Huduma hutegemea mawasiliano ya kweli katika njia ambayo inaeleweka.**

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 14:1-5 kwa ajili ya kikundi.

**Kuhubiri ni jambo muhimu zaidi kuliko hata kuongea kwa lugha nyingine.**

Kutoa unabii haimaanishi tu kwamba ni kutabiri kuhusu mambo yajayo. Unabii ni kuhubiri. Kwenye Agano la Kale, unabii mara nyingi ulijumuisha utabiri, kwa sababu hiyo ilikuwa ndiyo njia mojawapo ambayo nabii alithibitisha kwamba ujumbe wake ulikuwa unatoka kwa Mungu. Kwenye nyakati za Agano la Kale, mambo mengi yaliyoko kwenye Biblia yalikuwa bado hayajaandikwa.

Kwa wakati wa sasa mtu anaweza kuhubiri kutoka kwenye Biblia na akaonesha kwamba ujumbe wake unatoka kwa Mungu. Bado kuna vipengele visivyo vya kawaida ya kibinadamu ambavyo Mungu humpa mhubiri ufahamu maalumu wa kuutumia ukweli kwenye mazingira mbalimbali.

Kuongea hakuwezi kusaidia hadi pale watu watakapokuwa wameelewa lugha inayozungumzwa. Kama mtu atazungumza katika lugha ambayo watu wengine hawaielewi, ni Mungu peke yake atakuwa anamsikia.

Watu wengine huchukulia maneno "hakuna mtu anayemwelewa" [9] wakimaanisha kwamba msemaji hata yeye mwenyewe hajielewi, lakini hiyo siyo maana asilia ya sentensi hii. Kama Mjerumani atatoa ushuhuda katika kanisa letu na baadaye tukaanza kusema, "Hakuna mtu aliyemwelewa," haitakuwa tumemaanisha kwamba yeye mwenyewe hakujitambua.

Kama maneno hayatakuwa yamefafanuliwa, kanisa litakuwa halijajengeka kimaadili.

► Je, mchungaji afanye nini kuhusu mtu anayeongea mara nyingi katika kanisa katika lugha ambayo hakuna mtu anayeielewa na hakuna mtu anayeitafsiri?

Kwenye aya ya 5, Paulo anasema kwamba litakuwa ni jambo jema kama wote kwa pamoja wangekuwa wanaweza kunena kwa lugha; lakini ona pia kwenye 1 Wakorintho 4:8 na 1 Wakorintho 7:7. Alisema kwenye aya ya 4:8 kwamba litakuwa ni jambo jema kama wangetawala kama wafalme, lakini kwa uhakika hakuwa na mategemeo kwamba wawe hivyo kwa sababu hata mitume wenyewe walikuwa wanapitia kwenye mateso. Alisema

[9] 1 Wakorintho 14:2 NENO: Neno: Bibilia Takatifu 2025

kwenye 7:7 kwamba ingelikuwa ni jambo lililo jema kama wote kwa pamoja wangekuwa mabikira wasioolewa kama yeye; lakini alisema kwamba sio watu wote walioitwa kuwa katika hali hiyo, na tunajua kwamba ndoa ni mpango wa Mungu kwa watu wengi. Kwenye 14:5 anathibitisha tu kwamba litakuwa ni jambo lililo jema kama kila mtu angeweza kuwa na karama ya kunena kwa lugha; lakini haimaanishi kwamba kila mtu ataweza kuwa hivyo. Kwenye 12:29-30, anaelezea kwa uwazi kwamba hakuna aina fulani ya karama ambayo kila mtu anapaswa awe nayo.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 14:6-19 kwa ajili ya kikundi.

**Hotuba haina thamani kama itakuwa haieleweki.**

Kwenye aya ya 6, mtume aliuliza swali, "Je, "nitawafaidia nini?" Endapo itakuwa kitu hakieleweki, halitakuwa na faida yeyote. Hata vyombo vya muziki ni lazima vipigwe kutokana na mfumo fulani au mlingano wa sauti au vinginevyo havitakuwa na maana yeyote, isipokuwa kelele za sauti tu. Tarumbeta zinatumika kwa ajili ya ishara kwenye jeshi. Kama tarumbeta itatoa makelele ambayo hayako kwenye mpangilio wa kutoa ishara, hakuna mtu atakayejua kama ni ishara ya kumfukuzia adui au kama ni ya kuanua mahema. Mawasiliano ndiyo msisitizo wa sura hii yote.

> "Ni jambo linalopingana waziwazi na Neno la Mungu na desturi ya kanisa la kwanza kuwa na maombi ya hadhara kanisani au kuendesha sakramenti kwa lugha isiyoeleweka na watu."
>
> \- *Articles of Religion of the Methodist Church*

Maneno ambayo hayaeleweki ni kwamba "hewani" tu (9). Hii ni kusema kwamba maneno kama hayo hayana thamani kabisa.

Paulo alisema kwamba kama watu hawataelewana, wanakuwa kama watu ambao kila mmoja anamwona mwenzake hana ustaraabu (11). Kama mtu atataka kuendelea kuongea tu bila ya kuwa anaeleweka, atakuwa halijengi kanisa katika maadili bali anataka kukamilisha baadhi ya malengo yake mwenyewe (12).

► Je, kutakuwa na sababu gani za mtu kuongea mambo ambayo hakuna mtu yeyote anayeelewa?

Paulo alisema kwamba kama mtu ataongea katika lugha ambayo haieleweki kwa watu wengine, anachokielewa yeye mwenyewe hakina matunda (14). Paulo alikuwa hasemi kwamba mtu hawezi akajifahamu yeye mwenyewe, lakini kujifahamu kwake mwenyewe tu hakutasababisha uwepo wa jambo lolote zuri kwa watu wengine.

Alisema kwamba njia nzuri ni kufanya huduma katika Roho na kuwa na uelewa kwa wakati mmoja (15). Kuwa katika Roho haimaanishi kwamba mtu hawezi akaeleweka.

Alisema kwamba mtu ambaye hajaelimika ana uwezekano mkubwa wa kutoweza kuelewa kile kinachosemwa (16). Hii inathibitisha kwamba anazungumzia kuhusu lugha mbalimbali za kawaida. Alisema hatupaswi kusema, "Amen" kwa kitu tusichokielewa.

Paulo alisema kwamba alikuwa anafurahia kuwa na uwezo wa kuongea mchanganyiko wa lugha nyingi. Hata hivyo, alisema kwamba maneno matano tu yanayoeleweka ni bora zaidi kuliko maneno elfu kumi yasiyoeleweka (18-19).

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 14:20-25 kwa ajili ya kikundi.

**Maneno yenye upako wa Roho na yanayoeleweka yanampa Mungu utukufu.**

Kusudi la kunena kwa lugha ni kuwasilisha injili (ona Marko 16:15-17).

Baadhi ya watu huamini kuwa kipawa cha kunena kwa lugha ni ishara kuwa mnenaji ana Roho Mtakatifu, lakini aya ya 22 husema kuwa kipawa cha kunena kwa lugha si ishara ya kuthibitisha chochote kwa waamini. Hii humaanisha kuwa kipawa cha kunena kwa lugha haithibitishi chochote kwa mtu aliye nacho au kwa waamini wanaokiona kipawa hicho. Ni ishara kwa wasioamini pale tu ambapo kitatumika kufikisha injili kwa namna inayo eleweka kwa wasioamini.

Inawezekana kuwa kipawa cha kiroho kikaendelea kufanya kazi kwa mtu kama ataanguka tena dhambini na kuvunja uhusiano wake na Mungu. Hivyo basi, kipawa cha kiroho hakithibitishi kuwa mtu huyo anatenda sahihi au kuwa ameokoka

Kama mgeni katika kanisa akisikia watu wote wakinena kwa lugha na haelewi chochote kinachosemwa, atafikiria kwamba watu wamepagawa. Lakini kama mtu aliyeamini akisikia ukweli unaomhukmu moyo wake, atatambua kwamba Mungu yuko mahali pale.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 14:27-35 kwa ajili ya kikundi.

**(7) *Kanuni ya utaratibu*: Kanisa ni lazima liweke utaratibu katika ibada.**

Mtume aliuliza, "Kwa nini kila mtu anafikiri kwamba wanahitaji kufanya jambo fulani kwenye ibada?" Waumini wa Korintho walifikiri kwamba mtu alikuwa muhimu kama akisema kwa lugha au akiongoza ibada, kwa hiyo kila mtu alitaka awe na kitu cha kufanya.

Alisema kwamba kama mtu anazungumza katika lugha ambayo watu wengine hawaielewi, ni lazima itafsiriwe. Hawapaswi watumie muda mrefu wakati wa ibada kwa ajili ya vitu vinavyoweza kutafsiriwa (27).

Mtu anayeongea lugha ambayo watu wengine hawaijui, hawapaswi kuongea kama hakuna mtu wa kuweza kuitafsiri (28).

Kamwe haipaswi kuwe na watu wawili wanaoongea kwa wakati mmoja (31). Inavyoonekana ni kwa sababu kila mmoja anataka aongee, baadhi ya watu walikuwa wakiongea kwa pamoja kwa wakati mmoja. Ibada ilikuwa ni ya machafuko.

Baadhi yao inawezekana walikuwa wanasema hawawezi kuwa chini ya sheria kwa sababu wakati roho anapokuwa amejidhihirisha kwao wanakuwa hawawezi kujizuia wenyewe. Paulo alisema kwamba mtume anaweza kujizuia mwenyewe (32). Akisema kwamba Mungu

hawezi akaleta machafuko kwenye kanisa (33). Roho Mtakatifu hawezi akamwongoza mtu kufanya kitu ambacho ni kinyume na mafundisho ya Biblia.

► Je, kuna taratibu gani nzuri za kuiweka ibada iwe kwenye utaratibu wakati wa ibada?

Inavyoonekana, wanawake wa kanisa la Korintho walikuwa wanasababisha mtafaruku. Walikuwa wanaweza kuwa wanauliza maswali na kubishana, kwa sababu Paulo alisema wanapaswa wawe chini ya mamlaka na wangojee wakaulize maswali yao wakiwa nyumbani. Katika mazingira yaliyo bora zaidi, wanawake wanaweza wakaruhusiwa kuwa na huduma na kushiriki ibada, lakini wakiwa katika hali ya unadhifu.

► Mwanafunzi atapaswa kusoma 1 Wakorintho 14:36-40 kwa ajili ya kikundi. Je, Paulo alikusudia nini kuhusu uhusiano wao na makanisa mengine?

**(8) *Kanuni ya kitume:* Kila kanisa linatakiwa kutii mafundisho ya asili ya imani ya mitume.**

Waumini wa Korintho walikuwa wamebarikiwa kuwa na karama za kiroho. Inawezekana walianza kufikiri kwamba hawakuwa na hitaji la kusikiliza mamlaka nyingine yeyote. Paulo aliwakumbusha kwamba injili ilikuwa imekuja kwao kupitia kwa watu wengine. Walitakiwa watii mafundisho ya imani ya kanisa lote la Mungu. Kama mtu atajinadi kwamba anajua zaidi kuliko maelekezo ya mtume, ni mjinga na anapaswa achukuliwe kama mtu asiyekuwa na hekima wala asiyekuwa wa kiroho.

Paulo aliwaambia kwamba wasikataze matumizi ya lugha mbalimbali. Kunena kwa lugha ni muhimu, hasa katika maeneo ambayo lugha tofauti tofauti hutumika; lakini, karama hiyo ni lazima itumike katika njia ambayo Biblia inaelekeza.

## Mashindano ya Kanisa na Nguvu ya Kiroho.

Kuna baadhi ya makanisa ambayo hujaribu kuleta mvuto kwa kutumia udhihirisho wa nguvu ya kiroho. Wanaamini kwamba matendo ya miujiza karama za kiroho hulitambulisha vyema kanisa. Wanajinadi kwa matendo mengi ya miujiza ya uponyaji. Baadhi ya wanachama wanadai kupokea mara kwa mara maneno ya ufunuo kutoka kwa Mungu. Huduma zao za ibada zinaelekeza kwenye kulenga udhihirisho wa karama za kiroho kuliko ilivyo kwenye Biblia. Wanaamini kwa kila mkristo anapaswa kuwa na karama ya kunena kwa lugha, wanahitaji karama hii kujidhihirisha katika ibada zao za kuabudu. Wanahamasiaha sana watu kuwa na mpango katika ibada za kuabudu ili kwamba ibada zao ziwe zenye machafuko.  Viongozi wao wanajitahidi wajulikane kwamba wao ni maarufu, wakijivunia kuhusu uwepo wa nguvu ya kiroho na kulaumu makanisa mengine.

Matatizo mbalimbali huonekana kwenye makanisa yanayoshindana kwa udhihirisho wa nguvu ya kiroho. Wengi wa wanachama wake, na hata viongozi wao, huishi maisha ya dhambi za wazi. Hawaelelwi kuhusu kukua kiroho kunakodhihirishwa kwa njia ya imani ambayo huleta kustahimili matatizo ya maisha. Wengi wa viongozi ni vijana ambao hawaishi kwa ushindi dhidi ya dhambi, na hawawaheshimu waumini wazee na walio waaminifu.

Wanakuwa na matendo yasiyokuwa ya kibiblia ya kunena kwa lugha. Watu wao wengi kwa uhakika hawajawahi kuwa na uzoefu wa miujiza, lakini wana mategemeo ya kuwa nayo.

Kanisa ambalo lina upako wa kweli wa Roho Mtakatifu linapaswa kudhihirisha imani na karama za kiroho kufuatana na matendo ya kimaandiko. Kanisa linatakiwa liongoze wanachama wake wakue katika imani ambayo hustahimili nyakati ngumu za matatizo na inayoleta ushindi dhidi ya dhambi. Kuliko kutaka kudhihirisha karama za kiroho kama maonyesho, kanisa linapaswa litumie karama za kiroho katika kukidhi mahitaji ya familia ya imani.

► Je, kuna dalili gani za kanisa ambalo linajaribu kushindana na makanisa mengine katika kudhihirisha nguvu ya kiroho?

### Taarifa Saba kwa Muhtasari

1. Karama ya kiroho ni uwezo unaotolewa na Roho Mtakatifu kwa mtu aliyeamini kwa ajili ya kutumia kwa huduma ya kanisa.
2. Kila mtu aliyeamini hupokea karama za kiroho, lakini siyo kila mtu anayeweza kutegemewa kuwa na karama fulani moja.
3. Wanachama mbalimbali wa kanisa wanapaswa wafanye kazi kwa pamoja kama mwili mmoja kwa kila karama inayohitajika na umhimu wake.
4. Karama za kiroho huambatana na wito wa huduma mbalimbali.
5. Maneno yaliyotamkwa hayana thamani kama hayaeleweki.
6. Mtu aliyeamini ni lazima atumie kwa uangalifu karama zake katika kumletea Mungu utukufu na kuliimarisha kanisa.
7. Upendo kwa ajili ya Mungu na watu ni jambo la muhimu na la kudumu milele.

**Kazi za kufanya Somo la 14**

1. Kariri taarifa Saba kwa Muhtasari kwa ajili ya somo la 14. Andika aya moja inayoelezea maana na umuhimu wa kila kipengele katika hizi Taarifa Saba kwa Muhtasari (jumla aya saba) kwa mtu ambaye siyo wa darasa lako. Wakilisha kwa kiongozi wako wa darasa kabla ya kuanza kwa kipindi cha darasa kinachofuata. Kuwa tayari kushirikisha aya moja kwa kikundi kama kiongozi wa darasa atakutaka ufanye hivyo wakati wa majadiliano. Andika Taarifa hizi kutoka kwenye ufahamu wako bila ya kuangalia mahali popote mwanzoni mwa kipindi cha darasa kinachofuata.

2. Kumbuka kutengeneza ratiba ya nafasi yako mwenyewe ya kufundisha kwa wakati ambao utakuwa nje ya darasa na utoe mrejesho wako kwa kiongozi wa darasa baada ya kuwa umemaliza kufundisha.

3. Mtihani: Kwenye mwanzo wa kipindi kingine cha darasa, unahitajika kuandika kutoka katika kumbukumbu za ufahamu angalao kanuni saba miongoni mwa kanuni nane kutoka kwa Paulo kuhusu karama za kiroho.

# Somo la 15
# Maswali kuhusu ukomavu kwa Kanisa

## Utangulizi

Somo hili linatoa tabia za kanisa lililokua katika mfumo wa maswali. Kanisa linapaswa lifikirie au lizingatie maswali haya kwa ajili ya kuwa na ufahamu wa jinsi wanavyohitajika kuendelea.

*Kundi la wanafunzi katika darasa hili wanaweza wasiwe wote wanatoka katika kanisa moja na wanaweza wasiweze kufanya maamuzi kuhusu mabadiliko katika kanisa. Wanaweza wakatumia maswali haya kwa ajili ya kufanya tathmini ya kiwango cha ukuaji wa kanisa na kuweka malengo kwa ajili ya huduma zao wenyewe.*

*Kwa kila swali lililoko hapa chini, jadili swali linamaanisha nini, ukitumia maelezo ya ufafanuzi yaliyotolewa. Kisha, fikiria ni kwa jinsi gani kanisa linaweza kuendeleza tabia linazozihitaji.*

## Maswali kuhusiana na Kukua kwa Kanisa.

### (1) Vikundi vidogo vinavyoleta uhai wa kiroho kwa kanisa viko wapi?

Kanisa lililo na nguvu na lenye uhai lina aina fulani ya vikundi vidogo ambapo maisha endelevu ya kiroho yanasimamiwa. Vikundi hivi vinaweza kuwa ni makanisa ya nyumbani, madarasa ya Jumapili, au vikundi vya aina nyingine. Vikundi hivi vinaweza kuwa ni vile vilivyoandaliwa au vile vinavyojitokeza vyenyewe. Uamsho wa kiroho kwa kawaida huanzia kwenye vikundi vidogo. Maisha ya kiroho ya kanisa hayaendelezwi au kuhuishwa tu katika huduma za ibada. Uwajibikaji wa kiroho na mabadiliko ya maisha kwa kawaida hutokea katika vikundi vidogo. Viongozi wa kanisa wanapaswa wahakikishe kwamba vikundi vidogo vinakuwepo na vinatekeleza haya malengo. Kama muundo uliopo ndani ya kanisa hauwezeshi uwepo wa maisha ya kiroho, mabadiliko yanahitajika.

### (2) Nani mmiliki wa kanisa?

Kanisa halitakuwa limekua isipokuwa kumekuwepo na kikundi cha wanachama waliomaanisha na waliojitoa kabisa kwa ajili ya kanisa ambao huchukua jukumu kwa ajili ya huduma ya kanisa na uwezeshwaji wake wa kifedha.

Endapo huduma ya kanisa inaendeshwa kama ni biashara binafsi ya mchungaji, kamwe kanisa halitakaa likue. Kama jengo la kanisa ni la kupangisha, kanisa halitakuwa limekua kama mtu binafsi au shirika la nje ndio wanaolipia kodi ya jengo.

Kwa kweli, jengo na huduma ya kanisa vinapaswa viwe vinamilikiwa na kikundi cha wanachama wa kanisa. Kama jengo litakuwa limekodishwa, kusanyiko linatakiwa lichukue jukumu la pamoja kwa ajili ya kulipa kodi ya jengo.

Huduma ya kanisa la mtaa inatakiwa ianzishwe ili iendelee kama shirika hadi hapo atakaporudi Kristo.

**(3) Ni kwa jinsi gani huduma ya mtaa inawezeshwa kifedha?**

Hali ya kifedha iliyo nzuri sana kwa ajili ya kanisa inapasa isaidiwe na utoaji wa zaka kwa wanachama wake. Kama kanisa linawezeshwa na shirika la kutoka nje hilo siyo kanisa komavu na liko hatarini. Kama linawezeshwa na mchungaji au na watoaji wachache na siyo kusanyiko lote kwa ujumla, hili kusanyiko litakuwa halijafikia katika kiwango cha familia ya imani iliyokua.

Utoaji wa zaka ni mpango wa Mungu wa kusaidia katika uwezeshaji wa kanisa la mtaa. Viongozi wa kanisa wanatakiwa wafundishe kuhusu utoaji wa zaka na hatua kwa hatua wajenge uwezeshaji wa ndani kwa ajili ya huduma ya kanisa. Kanisa halipaswi litegemee uwezeshwaji kutoka nje kwa ajili ya utendaji wa shughuli zake. Msaada wa nje unatakiwa utumike katika miradi ya kujenga uwezo wa kanisa.

**(4) Je, kanisa linatoa uwezeshaji kwa mchungaji anayetumika kwa muda wote?**

Mpango wa kibiblia kwa ajili ya mchungaji ni kwamba anautoa muda wake wote kwa ajili ya huduma yake. Wakati mwingine hilo siyo rahisi kwa kanisa jipya, lakini kanisa linapaswa liwe na lengo la kukuza uwezeshaji ambao utamruhusu mchungaji kuendelea kuweka malengo yake kwenye huduma yake bila ya kuwa na wasiwasi wa mahitaji ya kifedha.

**(5) Je, ni mfumo gani unaotumika kwa ajili ya kuwajibika kifedha?**

Sadaka zinatakiwa zikusanywe na zihesabiwe na zaidi ya mtu mmoja. Watu kadhaa walioaminika wanapaswa wahusike katika kuweka vipaumbele vya kifedha na kanuni za kanisa. Washirika wanapaswa wajue ni kwa jinsi gani mfumo wa kifedha wa kanisa unavyofanya kazi.

**(6) Je, ni njia gani zinazotumika kupeleka injili kwa watu walioko nje ya kanisa?**

Jukumu la kwanza la kanisa ni kuhudumia washirika wa kanisa waliomaanisha na waliojitoa kabisa kwa ajili ya kanisa katika kusanyiko. Hata hivyo, kanisa ni lazima liweze kuwafikia watu walio majirani na wanaolizunguka kanisa. Kanisa ni lazima liwe na shughuli ambazo watu walioko nje watakuwa na hakika na kazi zinazofanywa na kanisa pamoja na kuisikia injili. Baadhi ya shughuli hizi zinaweza kuwa zisizotarajiwa na zisizopangwa. Viongozi watahitaji

> Miongoni mwa njia zote za kiungu ambazo zimewekwa kwa ajili ya kukamilisha umisheni wa Ukristo ni kupitia kwa watu wa eneo fulani maalumu waliopewa jukumu kwa ajili ya kuhubiri Injili."
>
> \- John Miley, *Christian Theology*

kuandaa shughuli zingine, pia. Washirika walio na uwezo wanapaswa waalikwe na wapewe mafunzo kwa ajili ya kuendesha shughuli hizo.

**(7) Je, ni kwa jinsi gani kanisa linawajibika na mahitaji ya watu wanaolizunguka kanisa?**

Kanisa linatakiwa litafute njia za kushughulika na mahitaji ya watu majirani wanaowazunguka. Kipaumbele kinapaswa siku zote kiwe ni kuonyesha upendo wa Mungu na kudhihirisha kanuni za kibiblia.

**(8) Je, kunao watu wa kabila fulani au wengine wenye viwango fulani vya kiuchumi wasiohusishwa kwenye mpango wa kanisa wa kuhubiri nje?**

Je, watu maskini hujisikia kukaribishwa kuhudhuria katika kanisa na hali ya nguo zao walizo nazo? Je, watoto walioko katika jumuiya hukaribishwa kuhudhuria hata kama wazazi wao hawapo? Je, kunalo kundi lolote la watu wa kabila fulani wanaojihisi kwamba kanisa halipo kwa ajili yao?

**(9) Je, wageni wa kanisa wanasalimiwaje?**

Kanisa linapaswa liwape mafunzo watu wake jinsi ya kusalimia wageni wanaotembelea kanisa. Lengo kuu la msingi la kusalimia watu ni kumfanya mgeni ajisikie amekaribishwa vizuri na katika njia ya kustarehesha. Watu kadhaa watapaswa washikamane na kuzoeana na mgeni. Hatapaswa tu kualikwa aje kwenye ibada nyingine, lakini pia akaribishwe ajiunge kwenye kikundi kidogo cha nyumbani au wanapokutanika kusanyiko la nyumbani mahali ambapo anaweza kujifunza na kuuliza maswali.

**(10) Je, kanisa linatumia mfumo gani wa kuwaingiza kwenye uanafunzi mara moja watu wapya waliookoka?**

Wakati mtu anapookoka, aidha akiwa katika kanisa au mahali pengine popote, hapaswi tu kualikwa kuhudhuria kwenye ibada, bali kwenye mfumo wa haraka wa kuwafanya kuwa wanafunzi. Jambo hili linaweza kuanza kwa ziara binafsi za mchungaji za kutembelea. Anaweza akaalikwa kwenye kikundi kidogo kinachokutana kila wiki. Kanisa linapaswa liwe tayari kuwahudumia watu wapya wanaookoka.

**(11) Je, kanisa linaweza kuelezeaje kuhusu kukua kiroho?**

Je, watu ambao wamekua kiroho wanaonekanaje? Kusanyiko linatakiwa lifundishwe tabia za kukua kiroho. Tabia hizi siyo kwamba siku zote zinaambatana na uwezo wa uongozi au vipaji, bali watu walio na tabia hizi watapaswa waheshimike kama mifano.

**(12) Je, kuna mfumo gani uliopo wenye kusudi la kuendeleza ukuaji endelevu wa kiroho?**

Jukumu kubwa na muhimu la kanisani kusaidia katika ukuaji endelevu wa kiroho wa washirika wake wa kanisa (Waefeso 4:11-13). Viongozi wa kanisa hawawezi wakawa ni watu wa kutegemea tu kwamba maendeleo ya kiroho yanatokea. Hawapaswi kuwa ni watu

tu wa kuhubiri kwenye makusanyiko na kuacha mambo mengine yote ya maendeleo ya kiroho kuwa ni juhudi ya mtu binafsi. Wachungaji wanapaswa wawe na mfumo kwa ajili ya kuwatia moyo watu kutumia nidhamu za kiroho (mf maombi, utoaji, kusoma maandiko nk). Wanapaswa watoe majukumu ya uwajibikaji kwa watu wote wanaokubaliana nayo. Mambo haya yanaweza kufanyika kupitia mazungumzo ya binafsi, vikundi vidogo, uwepo wa madarasa na njia nyingine zozote zitakazoweza kutumika.

**(13) Je, kuna muundo wowote wa uanachama ambao unawapa watu njia ya kuwa na msimamo na kujitoa kabisa kwa kanisa?**

Watu wanaotaka kuweka msimamo na kujitoa kabisa kwa kanisa wanahitaji hasa kujua msimamo wao huo una maana gani. Baadhi ya makanisa yanadai kwamba hayana muundo wa uanachama, lakini kila kanisa lina njia ya kujua watu wake. Kila mmoja anahitaji kujua watu wanaolifanya kanisa liwepo ni watu wa namna gani.

> "Yesu alilianzisha kanisa kwa yeye mwenyewe kuwaita na kuwakusanya pamoja watu wa kufanya utume waliokuwa karibu na yeye mwenyewe, akiwapa mafunzo, nidhamu, na kuwasimika kwenye huduma ya kulitangaza au kulieneza Neno na kushirikisha sakramenti, akieleza wazi nia yake isiyoweza kutenguliwa ya kujenga jumuiya endelevu ambayo itasimikwa ikiwa na nguvu na mamlaka ya kubatiza, kuhubiri, kutunza nidhamu, na kusherehekea chakula cha Pasaka pamoja na Bwana aliyefufuka.
>
> - Thomas Oden,
> *Life in the Spirit*

**(14) Je, vigezo vya uanachama au mshirika viko wazi na kujulikana kwa watu wote?**

Kila mtu anatakiwa afahamu ni vigezo gani muhimu kwa ajili ya uanachama. Vigezo pamoja na maelekezo ya mchakato wa kuweza kuwa mwanachama unapaswa uchapishwe.

**(15) Je, vigezo vya uanachama vinaruhusu mtu mpya anayeokoka kuanza kushiriki kwa haraka?**

Mtu ambaye ameokoka na yuko tayari katika msimamo na kujitoa kabisa kwa kanisa anahitajika aweze kulisaidia kanisa haraka inavyowezekana. Hiyo haimaanishi kwamba atahitajika kupewa nafasi fulani ndani ya kanisa au majukumu ya uongozi, lakini atapaswa ajue kwamba yeye ni sehemu ya kanisa.

**(16) Je, ni kikundi gani chenye jukumu la kuweka thamani na viwango kwa ajili ya kanisa?**

Kunakuwepo na kikundi cha wanachama wenye msimamo miongoni mwa kusanyiko la kanisa ambao hutathmini hali na mwenendo wa kanisa. Wanaweza wakawa ni baraza la mashemasi, au wanaweza wakawa ni wanachama wenye hadhi ya kupiga kura ambao wanaweza wakaitwa ni baraza la uongozi. Viongozi ni lazima waweke umakini mkubwa katika kukuza kikundi hiki. Mabadiliko kwenye kikundi hicho yatakuwa ndicho kipimo cha hali ya baadaye ya kanisa. Mchungaji ni lazima awajibike kwao na kuwa anawapa taarifa

wakati wote. Wao pamoja na timu ya uongozi ya kanisa ni lazima wawe na vipaumbele vinavyofanana kwa ajili ya kanisa.

**(17) Je, kanisa linashirikisha majukumu yake kwa njia ya maono yaliyo wazi?**

Mchungaji, timu ya uongozi, na kikundi cha wanachama wenye wajibu ni lazima watumie muda wao mwingi katika kujadili kusudi na malengo ya kanisa. Watapaswa waendeleze maono kwa ajili ya kanisa ambayo wanaweza wakatoa msaada wao. Kusanyiko linahitajika liwe na uzoefu na maono ya kanisa.

**(18) Je, washirika wa kanisa wanajua vyema mafundisho ya imani ya kanisa?**

Kanisa ni lazima lifanye jambo la ziada kwa ajili ya watu wake kuliko tu kuongoza ibada na kuwa na uzoefu wa kiroho. Wakati mtu aliyeko nje ya kanisa atakapouliza, "Kanisa lako linaamini nini?" mshirika wa kanisa anapaswa awe na jibu zuri la kumjibu. Washirika wa kanisa wanapaswa wawe na uwezo wa kuelezea misingi ya mafundisho ya imani ya Kikristo na mafundisho ya imani yaliyo maalumu ya kanisa.

**(19) Je, washirika wa kanisa wanaelewa uhusiano uliopo baina ya kanisa na dhehebu lao?**

Kanisa linapaswa liwe linatimiza ahadi zake kwa shirika au dhehebu lake. Ushirika wa kwenye shirika au dhehebu unaweza ukasaidia katika kutegemeza mafundisho ya imani ya kanisa. Watu wa kanisa wanatakiwa watiwe moyo wa kushiriki kwenye matukio ya shirika au dhehebu.

**(20) Je, ni kwa jinsi gani ibada zinapangwa na kufanyiwa tathmini?**

Viongozi wanatakiwa waombe sana katika kupanga ibada. Kama Roho Mtakatifu ataongoza ibada katika njia isiyotegemewa, litakuwa ni jambo zuri sana; lakini vinginevyo, viongozi ni lazima wawe na mpangilio wa kufuata. Inapaswa kuwepo na vikao ambavyo viongozi mbalimbali wa kanisa hufanya kazi ya pamoja ya kuandaa dondoo kwa ajili ya huduma za ibada.

Kama kanisa lina ibada nzuri ya kuabudu, kusanyiko linahusishwa na linavutiwa. Kanisa linatakiwa lijaribu kutumia watu wengi tofauti kwenye sehemu mbalimbali za ibada ili kusaidia kuwaweka watu kwenye mvuto na kuwajibika.

**(21) Je, ubatizo na Meza ya Bwana vinafanyika kwa mujibu wa maandiko na kwa njia yenye maana?**

Kila mtu aliyeokoka kiukweli anatakiwa awe tayari amebatizwa au awe yuko kwenye mpango wa kubatizwa karibuni. Meza ya Bwana inapaswa kutolewa kwa wale walio na ushuhuda wa neema. Meza ya Bwana inapaswa itolewe katika njia ambayo itasaidia washiriki katika kuabudu.

**(22) Je, kanisa linatendea kazi nidhamu ya kanisa ya kibiblia?**

Kanisa ni lazima liwe kinyume na dhambi. Kama mshirika wa kanisa amepatikana na hatia ya kutenda dhambi, ni lazima akabiliwe katika dhambi yake. Lengo liwe kumleta kwenye toba na kumrejesha kwenye ushindi wa kiroho.

**(23) Je, iko timu inayoshirikisha majukumu ya huduma?**

Huduma haitakua kama itakuwa haijajenga timu ya uongozi. Kila mtu ana mipaka kwenye kiasi fulani cha watu anachoweza kuwashawishi na majukumu anayoweza kuyabeba. Huduma ya kanisa haipaswi iwe ni huduma ya mtu mmoja.

**(24) Je, kuna mfumo gani wa kuchagua, kufunza, na kuongeza washirika kwenye timu ya huduma?**

Huduma haiwezi ikakua bila ya kuendeleza wanachama wapya kwa ajili ya uongozi wa timu. Wanachama katika timu wanatakiwa wachaguliwe kwa makini sana, lakini kanisa ni lazima siku zote liwe linafanya kazi katika kutafuta na kuendeleza watu ambao wataweza kuchukua majukumu ya baadaye.  Ukuaji wa huduma unategemeana na uendelezaji wa viongozi wengi zaidi.

> "Mwili huo mmoja unaofanana unapigana na mamlaka na nguvu za kipepo, na kwamba unategemea hata madhara mengine makubwa zaidi kwa siku za baadaye, ndiyo kwa wakati huo huo tayari uko na ushindi kutokana na uwezo wake wa sasa wa kuungana na kichwa kwenye jiji la mbinguni, kwa mategemeo ya furaha iliyokamilika katika Bwana ambako wote walio waaminifu watamtukuza Mungu kwa pamoja kwenye mwisho wa nyakati."
>
> - William Pope,
> *Ufupisho Kamili wa Teolojia ya Kikristo (A Compendium of Christian Theology)*

**(25) Je, kuna mfumo gani wa kushughulikia migogoro na matatizo ndani ya kanisa?**

Migogoro ambayo haijapatiwa ufumbuzi hulidumaza kanisa. Kusanyiko linatakiwa lifundishwe jinsi ya kutatua migogoro binafsi kwa watu. Viongozi wa kanisa hawapaswi kupuuza migogoro lakini uwe tayari kusaidia kuleta upatanisho.

**(26) Je, kanisa linatoa msaada kwa huduma za umisheni kwa ushirikiano na makanisa mengine?**

Kama kwa ukweli kanisa lina matarajio ya kutaka kuundeleza ufalme wa Mungu, halitahusika katika kufanya tu kazi ya kutaka lijulikane na kupata ushawishi katika mtaa, lakini litatoa msaada kwa huduma nyingine. Kanisa hudhihirisha kwamba ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu wakati linapojitolea kwa ajili ya huduma ambayo haitakuwa ni faida kwa ajili yake peke yake.

**(27) Je, kanisa linatoa msaada kwa kanisa lingine jipya linaloanza?**

Kanisa lililokua au lililokomaa linapaswa liwe linasaidia kanisa lingine jipya linaloanzishwa katika eneo hilo la karibu. Kanisa hilo jipya litaweza kuwafikia watu ambao hawangeweza kufikiwa na kanisa lililopo.

**(28) Je, huduma ya kanisa inahudumia watu wa marika yote na aina zote za watu katika kusanyiko?**

Mahitaji ya watoto, wazee, vijana, familia changa, wanaume, watu ambao hawajaolewa, na wengine wanapaswa wawe watu muhimu katika kanisa. Kanisa linapaswa pia lifikirie kuhusu mahitaji ya watu wa ngazi zote za ukuaji wa kiroho.

**(29) Je, watu katika kusanyiko wanafanya kazi kwa pamoja katika kuangalia mahitaji ya washirika wa kanisa?**

Kanisa ni lazima liweze kujali kuhusiana na mahitaji ya kifedha ya watu walio wahitaji katika kusanyiko. Mahitaji mengi yanapaswa yatolewe na watu walio tayari kusaidia watu wengine pasipokuwepo na usimamizi wa viongozi wa kanisa. Kama washirika wengi wa kanisa hawatajisikia kuwa na jukumu la kuwasaidia watu wengine walio wahitaji katika kanisa, watakuwa bado hawajatengeneza kanisa lililokomaa.

**(30) Je, ni kwa jinsi gani kanisa linahakikisha kwamba mahitaji ya watu walio na uhitaji ya kifedha katika kusanyiko yanashughulikiwa?**

Kanisa linapaswa liwe na mashemasi ambao watahakikisha kwamba mahitaji ya wahitaji katika kanisa yanatambulika. Kanisa katika kitabu cha Matendo liliwachagua mashemasi wa kwanza kwa ajili ya huduma hii.

# Fomu kwa ajili ya Kumbukumbu ya Kazi za Kufanya

Jina la Mwanafunzi ______________________________________

Weka sahihi yako wakati unapokuwa umemaliza kila kazi ya kufanya uliyopewa. Mitihani yote huhesabika kwamba “imekamilika” wakati mwanafunzi anapokuwa amepata matokeo ya alama 70% au zaidi. Kazi zote ulizopewa kufanya ni lazima zikamilishwe kwa ukamilifu ili uweze kupatiwa cheti cha kuhitimu kutoka Shepherds Global Classroom.

| Somo | Taarifa Saba & Aya | Masailiano | Kuandika | Mtihani |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |
| 8 | | | | |
| 9 | | | | |
| 10 | | | | |
| 11 | | | | |
| 12 | | | | |
| 13 | | | | |
| 14 | | | | |
| Mafundisho nje ya darasa | | | | |

Maombi kwa ajili ya kupewa Cheti cha Kufuzu kozi kutoka Shepherds Global Classroom yanaweza kukamilishwa kupitia ukurasa wetu wa wavuti www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitatumwa kwa mfumo wa kidigitali kutoka kwa Rais wa SGC kwenda kwa wakufunzi na wawezeshaji ambao watakamilisha maombi hayo kwa niaba ya mwanafunzi (au wanafunzi).